Humanitarian Exchange

Nambari 87
Agosti 2026

# Uongozi wa ndani katika mfumo wa kibinadamu unaobadilika



Humanitarian Practice Network

ODI Global

# Humanitarian Exchange

Toleo la 87 Agosti 2026

Humanitarian Practice Network

## Kuhusu HPN

Mtandao wa Utendaji wa Kibinadamu (HPN) ni jukwaa huru la kimataifa watendaji wa masuala ya kibinadamu na watafiti wanaohusikana watafiti walioko katika maeneo ya mwitikio wa majanga, kwa lengo la kuchapisha maarifa, uchambuzi na uzoefu wa kimaeneo. HPN inachangia katika kuboresha utendaji wa hatua za kibinadamu kwa kuwezesha ubadilishanaji wa maarifa na kuchangia katika ujifunzaji wa mtu binafsi na wa kitaasisi. Maoni na mitazamo inayotolewa katika machapisho ya HPN haiwakilishi wala kuakisi ile ya Humanitarian Policy Group au ODI Global.

**Humanitarian Practice Network**
ODI
Four Millbank
London SW1P 3JA
United Kingdom

Simu +44 (0)20 7922 0330
Barua pepe: hpn@odi.org
Tovuti: www.odihpn.org

Picha ya jalada: Mfanyikazi wa Asylum Access akiendelesha warsha nchini Tanzania kwa kundi la wanajamii wakimbizi.
Picha kwa hisani ya: Gabriel Diamond

## Yaliyomo

7
Ujanibishaji katika maneno, ujumuishaji katika vitendo: kwa nini viongozi wa maeneo ya ndani bado hawaongozi
**Rajeev Jha**

12
Uongozi wa kibinadamu nchini Syria: uwezo wa mashirika ya ndani unajengwaje?
**Moriab Gerges Haddo, Narges Ardwan and Muhammad Al-Kajak**

19
Mtendaji wa usaidizi wa kijamii asiyetambulika: mikakati inayoongozwa na wakimbizi katika eneo la Asia-Pasifiki na kwingineko
**Baqir Bayani**

24
Uongozi unaoongozwa na wakimbizi katika eneo la Cox Bazar
**Khair Ullah and Ahtaram Shin**

29
Zaidi ya Mwitikio: wanawake wanaoongoza hatua za kibinadamu nchini Palestina
**Ohaila Shomar and Majeda Saqqa**

35
Kuanzia data hadi utawala: kuwaweka wanawake waliohamishwa kutoka kwa makazi yao katika nafasi kuu za maamuzi ya tabianchi na masuala ya usaidizi wa kibinadamu
**Anila Noor and Madina Yuni**

40
Kuzisaidia jamii badala ya kuzibadilisha: mabadiliko katika mwitikio unaoongozwa na jamii nchini Syria
**Sara Bahsass**

Iliagizwa na kuchapishwa na the **Humanitarian Practice Network (HPN) katika ODI**

46
Kutoka kwa 'walioathiriwa na mgogoro' hadi viongozi: jinsi wakimbizi wa syria walivyoongoza mwitikio wa kibinadamu usio na kifani nchini Uturuki
**Areej Al-Mohammad**

52
Kutoka kwa 'walioathiriwa na mgogoro' hadi viongozi: jinsi wakimbizi wa syria walivyoongoza mwitikio wa kibinadamu usio na kifani nchini Uturuki
**Subin Mulmi**

58
Uliobuniwa kutenga: jinsi mifuko ya ufadhili iliyounganishwa inavyofichua hali halisi ya ujanibishaji katika utekelezaji
**Amrita Paul**



Kikundi cha kijamii kinakarabati na kuboresha bustani ya umma katika eneo la Hama, kwa usaidizi kutoka kwa shirika la Survivor and Community-Led Crisis Response. Picha ni kwa hisani ya: Kituo cha Asasi za Kiraia na Demokrasia (CCSD)

# Njia tofauti ya kufanya kazi

Kila toleo la *Humanitarian Exchange Magazine* huanza kwa swali: je, ni mitazamo ya nani inayoongoza mijadala inayoathiri hatua za kibinadamu? Mara nyingi sana, wale walioathirika zaidi na migogoro hiyo hualikwa kutoa mifano au kuthibitisha mijadala iliyopo, lakini ni nadra sana kupewa nafasi ya kuamua ajenda yenyewe. Toleo hili linalenga kufanya mambo kwa namna tofauti. Badala ya kuchagua mada ndani ya Mfumo wa Utekelezaji wa Masuala ya Kibinadamu (HPN), mtandao huu uliwaalika washirika wake – Muungano wa Kuimarisha Ushirikiano **(A4EP), Mtandao wa Haki za Wakimbizi Asia na Pasifiki (APRRN), Mtandao wa Kibinadamu wa Kifeministi (FHN), na Kituo cha Asasi za Kijamii na Demokrasia (CCSD)** – kuongoza mchakato huo. Kupitia majadiliano kadhaa, walibainisha mada kuu ya toleo hili kutokana na vipaumbele vya utekelezaji, *uongozi wa ndani katika usanifu wa kibinadamu unaobadilika*, na kuwaleta pamoja waandishi kutoka katika mitandao yao nchini Bangladeshi, Indonesia, Kenya, Palestina, Syria, Thailand na Uturuki. Jukumu la HPN halikuwa kuweka ajenda, bali kuandaa mazingira ya ajenda hiyo kujitokeza kupitia mazungumzo, ushirikiano na ubadilishanaji kati ya nchi zinazoendelea Kwa kufanya hivyo, toleo hili linaakisi azima endelevu ya HPN ya kukuza maarifa yaliyo jumuishi zaidi, ya ushirikiano na yasiyo ya kikoloni, yanayoimarisha ujifunzaji wa watu binafsi na taasisi katika sekta ya kibinadamu.

Aidha, wahusika wa ndani mara nyingi hutarajiwa kuchangia utaalamu wao, mahusiano yao na uzoefu wao bila malipo. Hata hivyo, kufanya hivyo kunahitaji muda, utaalamu na nyenzo za kitaasisi. Kwa toleo hili, waandishi na mitandao ya washirika walipokea msaada wa kifedha kwa michango yao. Huu ulikuwa utambuzi wa makusudi kwamba utaalamu wa ndani una thamani na kwamba ushirikiano wa usawa unapaswa pia kuzingatia usawa katika kutambua na kutuza michango.

Upatikanaji na ujumuishi pia ilikuwa misingi iliyoongoza kazi hii yote, kwani tulijitahidi kuwaalika waandishi kuandika katika lugha waliyohisi ni rahisi zaidi kwao, huku tukitoa msaada kutoka kwa wahariri wenye utaalamu wa kimuktadha na kiisimu. Hali hii ilisababisha makala kuandikwa kwanza kwa Kiingereza na Kiarabu, kabla ya kutafsiriwa kwa Kiarabu na Kiswahili pale ilipohitajika.

## Ndani ya Toleo Hili

Kama ilivyoelezwa awali, mada ya toleo hili ni uongozi wa ndani katika mfumo wa kibinadamu unaobadilika, na imekuja kwa wakati muafaka. Mchakato mpya wa mfumo wa kibinadamu umeanzisha tena wito wa kuwepo kwa mwitikio unaoongozwa na wahusika wa ndani na kuungwa mkono na jumuiya ya kimataifa. Hata hivyo, mashirika mengi ya ndani na ya kitaifa bado hupokea sehemu ndogo tu ya ufadhili wa kibinadamu na huendelea kutowakilishwa ipasavyo katika maeneo ya kufanya maamuzi. Makala katika toleo hili yanavuka mipaka ya mijadala ya kawaida na kuchunguza namna uongozi wa ndani unavyoonekana katika utekelezaji halisi. Yanaonyesha jinsi jamii na mashirika ya ndani yanavyokabiliana na mazingira yanayobadilika ya mfumo wa kibinadamu, yakipinga miundo ya mamlaka iliyopo na kufikiria upya namna

ushirikiano unavyoweza kujengwa. Kwa pamoja, makala haya yanatoa sio tu taswira ya usanifu unaobadilika wa mfumo wa kibinadamu, bali pia yanatoa maarifa muhimu kuhusu jinsi mustakabali wenye usawa zaidi na wenye ufanisi zaidi wa hatua za kibinadamu unavyoweza kuwa.

Toleo linaanza na makala ya **Rajeev Jha** kutoka **A4EP** anayechunguza vikwazo vya kimuundo vinavyoendelea kuzuia uongozi wa ndani hata wakati wa mchakato wa kuanzisha tena mfumo wa kibinadamu. **Moriab Gerges Haddo**, **Narges Ardwan** na **Muhammad Al-Kajak** kutoka **CCSD** wanaendelea kuchambua pengo lililopo kati ya kauli kuhusu ujanibishaji na utekelezaji wake, wakitumia uzoefu wa miaka mitatu wa kusaidia zaidi ya mashirika 50 ya Syria.

Makala mawili yanayofuata yanaangazia simulizi za jamii zilizohamishwa pamoja na mashirika yanayoongozwa na wakimbizi, ambayo mara nyingi hupuuzwa katika mijadala inayohusu ujanibishaji. **Baqir Bayani** kutoka **APRRN** anachunguza jinsi mifumo iliyopo ya ujanibishaji inavyoendelea kuyaweka pembeni mashirika yanayoongozwa na wakimbizi, licha ya jukumu lao kama wahudumu wa kwanza na wadau wanaoaminiwa na jamii katika nchi kama vile Indonesia na Thailand. Huku **Khair Ullah** na **Ahtaram Shin** kutoka **APRRN** wanategemea uzoefu wa mashirika yanayoongozwa na wakimbizi huko Cox's Bazar, Bangladeshi, kuonyesha mchango wao katika mwitikio wa dharura, elimu na ulinzi huku wakibainisha vikwazo vya kimuundo vinavyowazuia kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi.

Licha ya changamoto hizi, makala kadhaa yanaonyesha jinsi wahusika wa ndani wanavyoendelea kuongoza katika hatua za mwitikio. **Ohaila Shomar** and **Majeda Saqqa** from **FHN** wanatafakari kazi ya mashirika yanayoongozwa na wanawake nchini Palestina na jinsi yalivyorekebisha programu na huduma zao ili kukabiliana na kuongezeka kwa vurugu, uhamishaji wa watu na mahitaji ya kibinadamu. **Anila Noor na Madina Yunis kutoka FHN** wanaonesha mbinu ya Kente Threads inayojaribiwa nchini Kenya, ambayo inaonyesha jinsi wanawake wa Kenya waliohamishwa wanavyozalisha na kutumia data zao wenyewe ili kufanya maamuzi yanayohusu mabadiliko ya tabianchi na hatua za kibinadamu.

Viongozi wa ndani wa kibinadamu pia wanajitokeza kupitia watu ambao mara nyingi huonekana tu kama wapokeaji wa misaada. **Sara Bahsass** kutoka **CCSD** anachunguza mbinu inayoongozwa na jamii nchini Syria inayowezesha jamii kutambua mahitaji yao na kuyashughulikia. **Areej Al-Mohammad** kutoka **CCSD** anaangazia wakimbizi wa Syria nchini Uturuki na jinsi walivyobadilika kutoka kuwa wapokeaji wa misaada hadi kuwa wahusika wa hatua za kibinadamu. Makala haya yanapinga mtazamo wa kawaida unaotenganisha watoa misaada na wapokeaji wa misaada, na yanaonyesha kwamba watu walioathiriwa si washiriki tu wa mwitikio wa kibinadamu, bali pia ni viongozi kwa uwezo wao wenyewe.

Toleo hili pia linachunguza juhudi za kubadilisha mahusiano ya ufadhili. **Subin Mulmi** kutoka **APRRN** anachambua Mfuko wa Kimataifa wa Kukabiliana na Ukosefu wa Uraia, ambao hutoa ufadhili unaobadilika, wa miaka mingi na usio na masharti kwa makundi yasiyo rasmi ya ngazi ya jamii yanayoshughulikia tatizo la ukosefu wa uraia, ambayo huenda hayajasajiliwa rasmi au hayana uwezo wa kufikia njia za kawaida za ufadhili. **Amrita Paul** kutoka **APRRN** anachunguza nafasi ya mtandao huo katika kusaidia mashirika yanayoongozwa na wakimbizi na yale yanayotegemea jamii kupata na kusimamia fedha za pamoja, akionyesha fursa zilizopo pamoja na vikwazo vinavyoendelea kuwepo ndani ya mifumo ya ufadhili wa kibinadamu.

## Mafunzo muhimu

Ingawa makala haya yanatokana na simulizi kutoka mazingira mbalimbali—kuanzia Syria na Palestina hadi Kenya, Bangladesh na eneo la Asia-Pasifiki—yanaafikiana kuhusu ujumbe mmoja wa msingi: uongozi wa ndani tayari upo. Jamii, mashirika yanayoongozwa na wakimbizi, mipango inayoongozwa na wanawake na asasi za kiraia za ndani hazisubiri kutambuliwa kimataifa; tayari zinaongoza hatua za mwitikio, zinabuni suluhisho, zinajirekebisha na kuzisaidia jamii zao kustahimili migogoro. Kinachoendelea kuwazuia si ukosefu wa uwezo, bali ni usanifu wa mfumo wa kibinadamu ambao mara nyingi hujikita katika kuelekeza ufadhili, kufanya maamuzi na kutoa uhalali katika taasisi za kimataifa.

Katika makala yote, waandishi wanabainisha vikwazo vinavyojirudia, ikiwa ni pamoja na mifumo ya ufadhili isiyobadilika, kutengwa katika maeneo ya uratibu na utawala, masharti mazito ya uzingatiaji wa taratibu, pamoja na vizuizi vya kisheria na kisiasa vinavyozuia wahusika wengi wa ndani kupata rasilimali moja kwa moja. Wakati huo huo, makala haya yanatoa mifano yenye ushawishi ya mbinu mbadala, yakionyesha jinsi ufadhili unaobadilika, ushirikiano unaotegemea uaminifu, ufanyaji wa maamuzi kwa ushirikiano, mwitikio unaoongozwa na jamii na utambuzi wa thamani ya uzoefu wa maisha unavyozalisha hatua za kibinadamu zenye ufanisi zaidi, uwajibikaji mkubwa na uendelevu. Kwa pamoja, michango hii inaipa sekta ya kibinadamu changamoto ya kufanya zaidi ya lugha ya ujanibishaji pekee na kuelekea katika ugawaji wa kweli wa mamlaka, rasilimali na maarifa, ambapo uongozi wa ndani unatambuliwa sio kama matarajio ya baadaye, bali kama uhalisia uliopo tayari unaostahili kuunda mustakabali wa hatua za kibinadamu.

### Shukrani

Toleo hili limekuwa zao la ushirikiano wa kweli. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa mashirika washirika wetu na waandishi wote ambao kwa ukarimu walishiriki maarifa yao, uzoefu wao na tafakuri zao. Tunawashukuru kwa namna ya pekee timu yetu ya uhariri pamoja na watafsiri, **Tamarind Language Services Ltd** na **Hashem el Hashem**, ambao utaalamu wao wa kimuktadha na kiisimu ulihakikisha kwamba mawazo yaliyowasilishwa hapa yaliwafikia wasomaji wa Kiarabu, Kiswahili na Kiingereza huku yakihifadhi uhalisia na sauti ya kila mchango.

**Catherine Komuhangi**
Meneja wa Uratibu wa HPN

**Serena Abi Khalil**
Mkuu wa Maendeleo na Ushirikiano wa HPN

# Ujanibishaji katika maneno, ujumuishaji katika vitendo: kwa nini viongozi wa maeneo ya ndani bado hawaongozi

Rajeev Jha


Watendaji wa maeneo yanayopokea usaidizi wa kibinadamu hawawezi kuongoza katika kutoa mwitikio kwa masuala ya usaidizi wa kibinadamu hasa kwa sababu mfumo wa usaidizi wa kibinadamu haukuundwa kwa ajili yao hapo awali. Kihistoria, ukuzaji wa mfumo huu ulianza mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa na ukaongeza kasi baada ya Vita vya Kwanza na vya Pili vya Dunia, hali iliyosababisha kuanzishwa kwa mashirika kadhaa ya kimataifa yaliyolenga miktadha ya usaidizi wa kibinadamu na maendeleo. Ukuzaji huu ulijikita katika mfumo unaozingatia usaidizi ambao kimsingi ulihakikisha mtiririko wa rasilimali au fedha katika muundo wa kuanzia juu hadi chini. Hii pia huchangia katika uwajibikaji, ambao kihistoria umeupa kipaumbele uwajibikaji kwenda juu kwa wafadhili na serikali badala ya uwajibikaji kwenda chini yaani uwajibikaji kwa jamii zilizoathiriwa. Hata hivyo, ujanibishaji uliendelea kusisitizwa Mkutano wa Kimataifa wa Masuala ya Kibinadamu ulichangia katika uzinduzi wa mapatano ya Grand Bargain. Tangu wakati huo, ujanibishaji umechunguzwa, kujadiliwa na kufikiriwa upya. Lugha imebadilika - kutoka 'ufadhili wa moja kwa moja' hadi 'ubia sawa', kutoka 'lengo' hadi 'mifumo', na kutoka 'kushiriki' hadi 'uongozi' Hata hivyo, pengo kati ya matarajio na hali halisi bado lipoo. Makala haya yanachunguza kwa nini pengo hili linaendelea kuwepo.

## Muundo wa kibiashara, vikwazo vya utaratibu na mtiririko wa fedha

Muundo wa kibiashara wa mfumo wa usaidizi wa kibinadamu umeundwa kwa kiasi kikubwa kulingana na muundo wa mashirika ya kimataifa na mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGOs), ambayo yanaendelea kutawala mtiririko wa ufadhili na usimamizi wa programu. Licha ya juhudi za miaka mingi zilizofanywa kupitia mapatano ya Grand Bargain ili kuongeza uwiano wa ufadhili kwa watendaji wa kieneo na kitaifa, ufadhili wa usaidizi wa kibinadamu unaendelea kutolewa kwa watendaji wa kimataifa na Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Serikali (INGOs). Alliance for Empowering Partnership (A4EP) ina wanachama kote Asia, Afrika na Mashariki ya Kati. Wanachama walioshirikishwa katika kifungu hiki walionyesha kuwa ni idadi ndogo tu iliyopokea ufadhili wa moja kwa moja kutoka kwa wafadhili au mashirika ya kimataifa. Hii ni kwa sababu mashirika ya ndani na ya kitaifa, ambayo mara kwa mara yapo kwenye mstari wa mbele wa utekelezaji, mara nyingi hukabiliana na vikwazo vya kiutaratibu wakati wa kujaribu kupata ufadhili moja kwa moja. Vikwazo hivi ni pamoja na kupitia wito wenye ushindani wa kutuma maombi ya ufadhili, kuzingatia mahitaji makubwa ya uchunguzi wa kina, kufikia viwango vikali vya ununuzi na usimamizi wa fedha, na kuzingatia majukumu magumu ya kutoa ripoti. Kwa mfano, miongozo ya ukaguzi wa kina ya Ofisi ya Mambo ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Uingereza inataka viashiria muhimu vya utendakazi vinavyoweza kupimika kutoka kwa washirika wote. Hata hivyo, watendaji wa ndani mara nyingi wanatatizika kufikia viwango hivi kutokana na uwezo mdogo katika ufuatiliaji na tathmini, ukosefu wa wafanyakazi waliojitolea kwa ajili ya ukusanyaji wa data, na changamoto katika kufanya tafiti za msingi, kufuatilia viashiria na kuripoti. Marie-Rose Romain Murphy, Mwanzilishi Mwenza wa Wakfu wa Jumuiya ya Haiti, alitoa tathmini ya wazi: 'kuzingatia miongozo iliyowekwa kunaendelea kuwa changamoto kwa watendaji wengi wa ndani'.

Mara nyingi, ufadhili hupitia ngazi mbalimbali za kati yakiwemo mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali, kabla ya kufikia mashirika ya ndani na yale yanayojikita katika jamii.

**Kielelezo 1 Kielelezo cha ufadhili wa usaidizi wa kibinadamu**




Kumbuka: Katika kila hatua ya mchakato huu, sehemu ya ufadhili inazuiliwa ili kufidia gharama za usimamizi na malipo ya ziada, ambazo hupunguza kiasi ambacho hatimaye huwafikia watendaji wa ndani.

## Mfumo wa makundi – uratibu au kutengwa

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (UNOCHA) inatumika kama kitovu cha kimsingi cha kuratibu mwitikio wa kimataifa kwa masuala ya usaidizi wa kibinadamu. Uianishaji upya wa usaidizi wa kibinadamu unaoendelea umepunguza idadi ya makundi kutoka 11 hadi 8. Ingawa mabadiliko haya yanaweza kuongeza ufanisi wa utendakazi, hakuna uhakika kama yataendeleza ajenda ya ujanibishaji. Utaratibu wa uratibu pia unaonyesha ukosefu wa usawa katika ushiriki na ushawishi ndani ya mfumo wa usaidizi wa kibinadamu. Ushahidi unapendekeza kwamba Mashirika ya Kitaifa yasiyo ya Serikali (NGOs) mara nyingi huwa hayajumuishwi kikamilifu katika michakato ya uratibu na kwamba mchakato wa kufanya maamuzi na maandalizi ya mikakati mara nyingi huendelezwa na vikundi vidogo vya watendaji ambavyo huamua ni vipaumbele vipi vinaendelezwa na jinsi rasilimali zinagawanywa.

Katika ngazi ya kitaifa, Timu za Nchi za Usaidizi wa Kibinadamu kimsingi zinaongozwa na kutawaliwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa, mara nyingi yakiweka ajenda na kuamua nani atazungumza na kusikilizwa. Kutengwa huku kunathibitishwa mara kwa mara katika mikutano ya mwaliko pekee, ambayo kwa kawaida huwahusisha wakuu wa mashirika ya kimataifa pekee. Zaidi ya hayo, vizuizi kama vile hitaji la ustadi wa Kiingereza, uhifadhi wa kina wa nyaraka na violezo vya mapendekezo vlivyowekwa vinaweza kuwatenga watendaji kadhaa wa ndani kutoka kwa muundo wa uratibu.

Licha ya changamoto hizi, kuna matukio ya mazoea ya uratibu jumuishi zaidi ambayo yanastahili kutambuliwa na kuchunguzwa. Kwa mfano, wakati wa kuidhinishwa kwa kundi la Uratibu wa Kambi ya Kimataifa na Usimamizi wa Kambi na serikali ya Ethiopia mnamo 2021, shirika la ndani, Action for the Needy, liliteuliwa kama Mshirika wa Uratibu wa Kundi pamoja na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji na Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) kama mashirika yanayoongoza. Kama ilivyoripotiwa na Humanitarian Action, kuna ongezeko dogo la majukumu ya uongozi yanayochukuliwa na mashirika ya kitaifa yasiyo ya serikali katika uratibu wa makundi kati ya 2021 na 2023, karibu 3% hadi 5%. Ingawa mifano kama hiyo ni michache na adimu, inaonyesha kuwa ushirikiano wa kweli katika uongozi kati ya wadau wa ndani na wa kimataifa katika uratibu wa makundi unawezekana. Vikwazo vikuu vya kufikia ushirikiano huu wa uongozi, kama ilivyoelezwa na Meschac Nakanywenge, Mkurugenzi Mtendaji wa Union for Promotion Protection, Human Rights Defense and the Environment katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo 'si vya kiufundi bali ni vya kisiasa na kimfumo, yaani, upinzani dhidi ya mabadiliko kutoka kwa wadau wa kimataifa pamoja na hamu yao ya kudumisha udhibiti wa rasilimali na mamlaka'.




**Kikundi Kazi cha Mkataba au Mabadiliko katika Hoteli ya Bassin Du Congo mjini Goma, Mkoa wa Kivu Kaskazini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Picha ni kwa hisani ya: UPDDHE**

## Vikwazo vya ndani, kaida za kijamii na kitamaduni

Vikwazo vya kimuundo pia huathiri utendakazi ndani ya nchi katika ngazi ya mashirika ya kitaifa na yale madogo ndani ya mataifa, mengi yakiwa yanapatikana katika nchi zinazokuwa na zenye kipato cha chini na yanafuata sheria za kitaifa kuhusu usajili, kanuni, ukaguzi na mahitaji mengine ya uzingatiaji wa sheria. Mijadala mingi kuhusu ujanibishaji hutokea katika ngazi ya kimataifa, lakini utendakazi wa watendaji wa ndani huongozwa na kanuni, taratibuna sheria za ndani za eneo au nchi ambayo wamejikita. Kwa mfano, Tangazo la Serikali ya Ethiopia la mwaka 2009 la Kuwezesha Usajili na Udhibiti wa Mashirika ya Uhisani na Vyama (CSP), liliweka vikwazo fulani katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za mashirika ya kiraia (CSOs). 'Ibara ya 57 inaipa serikali mamlaka ya kukataa kusajili mashirika ya kiraia (CSOs) ambayo malengo au shughuli zake zinakinzana na maadili ya umma.' Zaidi ya hayo, 'Ibara ya 75(1) ya Tangazo la Mashirika ya Kiraia inayataka mashirika yapate idhini ya maandishi kutoka kwa Wakala wa CSO ili kufungua akaunti ya benki.'.

Sheria iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria ya Tanganzo la Sheria ya Mashirika ya Kiraia Nambari 1113/2019, ilipitishwa Januari 2019, na ilikuwa uboreshaji wa sheria ya awali. Hata hivyo, mpito kuelekea kwa sheria hiyo mpya ulihitaji mamia ya Mashirika ya Kiraia na Kijamii (CSOs) yajiandikishe upya chini ya mfumo uliorekebishwa, na kuweka mzigo mkubwa wa kiutawala kwa mashirika ambayo tayari yanafanya kazi kwa rasilimali na uwezo mdogo. Kwa mashirika madogo ya ndani yenye miundo finyu ya usimamizi, kukamilisha taratibu changamano za usajili na uzingatiaji wa kanuni kunaweza kudhoofisha kama ilivyo upungufu wowote wa ufadhili. Mara nyingi, mashirika ya ndani hayawezi kufanya kazi kwa kujitegemea, kwani yanabaki kutegemea mashirika ya kimataifa kwa usaidizi wa ufadhili - safu ya kati ambayo ujanibishaji unanuia kupunguza au kuukwepa. Utegemezi huu si wa kifedha tu; ni wa kimuundo na kimfumo, unaoimarishwa na usanifu wa kimataifa wa usaidizi wa kibinadamu na mazingira ya kisheria ya ndani ambayo watendaji wa ndani lazima wafanyie kazi zao.

Vikwazo vya kijamii na kitamaduni vinavyoathiri kazi katika ngazi za kitaifa na viwango vidogo katika taifa vinazuia kwa kiasi kikubwa ujanibishaji, hasa katika nafasi za uratibu na uwezo wa watendaji wa ndani kuinua hadhi ya taasisi zao. Kiutendaji, ufasaha katika Kiingereza, ujuzi wa lugha ya usaidizi wa kibinadamu, na ukaribu na vitovu vya uratibu vya mji mkuu vimekuwa alama zisizo rasmi za uaminifu na kitaaluma. Hii imechangia kuibuka kwa 'wasomi wapya wa ndani' katika mfumo wa usaidizi wa kibinadamu - mashirika yasiyo ya kiserikali ya mijini yanayozungumza Kiingereza ambayo yapo katika nafasi nzuri ya kufikia majukwaa ya uratibu, fursa za ufadhili na ushirikiano. Wakati huo huo, mashirika ya vijijini, ya mashinani na ya kijamii, licha ya ukaribu wao na watu walioathiriwa, yanabaki kutengwa kwa kiasi kikubwa na majukwaa haya na ufikiaji wa moja kwa moja wa rasilimali.

## Mapendekezo

Watia saini wa Grand Bargain na wafadhili wakuu wa taasisi wanapaswa kupitisha sera zinazoweza kutekelezwa zinazohitaji mipangilio iliyopangwa kwa wakati kama njia inayoaminika kuelekea kufikia ahadi zilizopitwa na wakati kwa mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani na kitaifa.

Mfuko wa Pamoja wa UNOCHA wa Nchi, ambao uliongeza ufadhili kwa watendaji wa ndani hadi 31% katika mwaka 2023, unatoa mfumo wa uwazi wa mgao wa ufadhili ambao unapaswa kupitishwa kwa upana zaidi. Katika ngazi nyingine, kuna haja ya kuanzisha ufadhili wa pamoja wa kikanda, kama vile mifuko ya ufadhili wa pamoja ya Asia Kusini, mifuko ya majanga ya Chama cha Kimataifa ya Kusini-Mashariki mwa Asia na Mfuko wa Usaidizi wa Kibinadamu wa Umoja wa Afrika. Hata hivyo, CBPFs hazikosi utata, kwa kuwa zinategemea chanzo kimoja cha ufadhili. Ufadhili wa nchi ya Marekani wa bilioni $2 kwa UNOCHA unaibua maswali mazito kuhusu uendelevu wa mfumo huo.

## Hitimisho

Mageuzi ya kimuundo yanaweza kuwa yamepangwa vizuri, lakini hayawezi kufikia matokeo yanayotarajiwa bila mabadiliko yanayolingana katika utamaduni wa mashirika, kanuni na mienendo ya kijamii ambayo imekuwepo tangu asili ya kikoloni ya mfumo wa usaidizi wa kibinadamu. Ufadhili unaendelea kutiririka kupitia miundo ya washirika wa kati wenye utabaka, na nafasi za uratibu mara nyingi hutumika kama utaratibu wa ulinzi, hali inayoruhusu mashirika teule pekee kushiriki kwa mwaliko.

Zaidi ya hayo, vikwazo vya ujanibishaji havizuiliwi na kizuizi kimoja tu, bali vimepachikwa katika mfumo mzima. Mazingira ya udhibiti wa ndani huathiri kiwango ambacho mashirika ya ndani yanaweza kufanya kazi kwa kujitegemea, na kaida za kijamii na kitamaduni huathiri anayetambuliwa, kusikilizwa na kufadhiliwa ndani ya mfumo.

Kwa pamoja, vikwazo hivi vinaonyesha kwamba ujanibishaji unabaki kuwa mdogo si kutokana na ukosefu wa kujitolea au uwezo miongoni mwa watendaji wa ndani, bali kwa sababu ya jinsi mfumo wa usaidizi wa kibinadamu ulivyoundwa na hufanya kazi katika hali halisi. Kuwepo kwa uzinduzi wa urekebishaji wa usaidizi wa kibinadamu, juhudi za kuendeleza ujanibishaji zitahitaji kuwa zaidi ya ahadi rasmi na marekebisho ya kiufundi na badala yake ushughulikie masuala ya kimuundo katika usanifu katika sekta nzima ya usaidizi wa kibinadamu.

Makala haya yanawakilisha tathmini ya kina ya mifumo yenye maslahi yao ya kitaasisi, ikiwa ni pamoja na motisha zinazowachochea watendaji wa kimataifa kudumisha udhibiti, hata wanapotetea hadharani uongozi wa ndani.

**Rajeev Jha** ni mtaalamu wa maendeleo mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 19 huko Asia Kusini, anayeshughulikia masuala ya kupunguza hatari za maafa, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, riziki thabiti na ujenzi wa ustahimilivu unaotegemea jamii. Akiwa amejitolea sana kwa ujanibishaji wa jamii na uongozi wa jamii, Rajeev anashirikiana kwa karibu na mashirika ya mashinani, serikali za mitaa na mitandao ya asasi za kiraia ili kukuza mikakati endelevu na ya muda mrefu ya ustahimilivu.

# Uongozi wa kibinadamu nchini Syria: uwezo wa mashirika ya ndani unajengwaje?

Moriab Gerges Haddo, Narges Ardwan na Muhammad Al-Kajak

Katika muongo mmoja uliopita, Syria imeshuhudia moja ya migogoro migumu zaidi ya kibinadamu ya enzi ya kisasa, ambayo athari zake zimegusa na kubadilisha maisha ya mamilioni ya raia. Kutokana na hali hii, uongozi wa mitaa umeacha kuwa suala la vitendo tu. Umekuwa ni hitaji la kimsingi, njia hasa ambayo msaada unawafikia wale wanaouhitaji zaidi.

Makala hii imejikita katika uzoefu wa moja kwa moja wa miaka mitatu wa kufanya kazi na zaidi ya mashirika 50 ya ndani kutoka sekta mbalimbali,[1] kupitia programu ya "Kusaidia mashirika kuboresha mwitikio wa kibinadamu, maendeleo na ujenzi wa amani nchini Syria," inayotekelezwa na Kituo cha Asasi za Kiraia na Demokrasia (CCSD).



**Washiriki wakati wa Kongamano la Uratibu na Ushirikiano lililofanyika Qamishli, katika Mkoa wa Al-Hasakah, Syria. Picha kwa hisani ya: Shirika la DemoS**

1 Sekta hizi zinajumuisha kujenga amani, kutoa misaada, kuhudumia, na uimarishaji wa uwezo wa makundi mbalimbali kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Makala hiyo inatokana na uchambuzi kadhaa uliofanywa katika kipindi chote cha mpango huo. Data zilizokusanywa kupitia programu zinaonyesha kuwa asilimia 81 ya mashirika ya ndani yaliweza kufikia maeneo ambayo mashirika makubwa ya kimataifa hayakuweza kuyafikia kutokana na vikwazo vya kiusalama na kiutawala. Takwimu hiyo pekee inaweka wazi ukweli usiopingika: ukaribu wa mashirika ya ndani na jamii, kwa kuzingatia eneo la kijiografia na mahusiano ya kijamii, ndiyo sababu kuu inayowezesha kuokoa maisha ya watu.

Hata hivyo, licha ya kuongezeka kwa mchango wao, mashirika ya ndani bado yanaendelea kufanya kazi katika mfumo wa kibinadamu ambao si mara zote huwapa nafasi wanayohitaji ili kuongoza. Katika utafiti wa ndani uliofanywa na programu, asilimia 82 ya wakurugenzi watendaji wa mashirika ya ndani waliripoti kuwa kikwazo kikubwa wanachokabiliana nacho si ukosefu wa uwezo wa kiutendaji, bali ni fursa finyu za kupata ufadhili wa moja kwa moja pamoja na kutoshirikishwa kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi. Changamoto hizi haziakisi udhaifu katika uwezo wa wahusika wa ndani, bali zinaonyesha kuwepo kwa pengo la kimuundo katika namna mfumo wa kimataifa wa kibinadamu ulivyopangwa na jinsi majukumu yanavyogawanywa ndani yake.

## Kwa nini uongozi wa ndani ni muhimu? Takwimu Zinasimulia kisa hicho

Katika miaka ya karibuni, mjadala kuhusu *ujanibishaji wa mwitikio wa kibinadamu* umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Dhana hii inahusu kuhamisha wajibu, uongozi na rasilimali kwa wahusika wa ndani katika nchi zilizoathiriwa na migogoro, badala ya kutegemea mashirika ya kimataifa au ya nje. Hata hivyo, pengo kati ya matamshi na utekelezaji wake halisi bado ni kubwa. Ingawa data zetu zinaonyesha kuwa asilimia 64 ya mashirika ya ndani yaliyoshiriki katika programu yana mahusiano makuu na jamii za wenyeji, yanayozidi kwa kiwango kikubwa uwezo wa kufikia jamii wa washirika wa kimataifa, mashirika hayo hupokea chini ya asilimia 10 ya jumla ya ufadhili wa shughuli za kibinadamu nchini Syria.

Pengo hili halikuwa tu takwimu ya kinadharia iliyoandikwa katika ripoti. Lilikuwa ni uhalisia wa maisha kwa Abdullah al-Yassin, Mkurugenzi wa shirika la Golden Hands (الأيادي الذهبية) linalofanya kazi katika mkoa wa Idlib na ambalo lilikuwa mshiriki wa programu hii. Al-Yassin alituambia katika mahojiano kwamba:

> ‘Tulikuwa tukishuhudia kwa macho yetu wenyewe mahitaji mapya yakijitokeza ndani ya muda mfupi kutokana na mashambulizi ya mabomu au watu kulazimika kuhama makazi yao kwa dharura. Tulijua kwa usahihi ni familia gani iliyohitaji msaada gani. Lakini tulilazimika kutumia wiki kadhaa kuandaa na kuwasilisha ripoti kwa wafadhili wa kimataifa ili tu kupata idhini ya kuelekeza upya asilimia 10 ya bajeti ya mradi kwa ajili ya kukidhi mahitaji hayo. Wakati mwingine, kufikia idhini ilipopatikana, familia iliyokuwa inahitaji msaada ilikuwa tayari imehama makazi yake au imekimbia eneo hilo.’Ushuhuda huu unaakisi changamoto za kimuundo: ufadhili usioruhusu mabadiliko. Kupitia programu yetu, tuligundua kuwa mashirika yaliyopata msaada wa kifedha wenye unyumbufu[2] yalikuwa na uwezo wa kushughulikia mahitaji ya dharura kwa haraka mara tatu zaidi ikilinganishwa na yaliyokuwa yakitekeleza shughuli zake chini ya masharti ya bajeti ngumu na zisizobadilika.

Hata hivyo, takwimu pekee hazitoshi kueleza kwa ukamilifu kiwango cha mabadiliko yanayoletwa na uongozi wa ndani. Kwa mfano, tuangalie uzoefu wa shirika la Awda for Development katika maeneo ya vijijini mashariki mwa Deir ez-Zur. Tulipoanza kufanya kazi pamoja miaka mitatu iliyopita, shirika hilo lilikuwa linakabiliwa na changamoto ya kawaida: ufadhili uliokuwa umeelekezwa kwa miradi ya elimu ya muda mfupi pekee, bila uwezo wa kushughulikia vikwazo halisi vilivyowazuia watoto hasa wasichana kuhudhuria shule.

2 Hii ina maana ya kuruhusu ugawaji upya wa asilimia 20–30 ya bajeti bila kuhitaji idhini ya awali kutoka kwa mfadhili.

Ili kufikia chanzo halisi cha tatizo ili, shirika hilo liliandaa mfululizo wa vikao vya mashauriano na jamii. Timu ilithibitisha kile ilichokuwa tayari inakifahamu, upungufu wa vitabu na vifaa vya kufundishia. Hata hivyo, walibaini pia tatizo lingine la kusikitisha zaidi. Amina, ambaye ni mwalimu katika moja ya shule za eneo husika, anaeleza:

> 'Wasichana walikuwa wakikatisha masomo yao si kwa sababu wazazi wao hawakutaka wasome, bali kwa sababu shule haikuwa na vyoo salama. Katika jamii yetu ya kihafidhina, ni vigumu kwa kijana msichana kukaa mahali pasipo faragha au usafi na afya. Matokeo yake, kila mwezi kulikuwa na wasichana waliokuwa wakiacha shule.'

Kutokana na uhalisia huo, na kwa msaada wa ufadhili wenye unyumbufu uliotolewa kupitia programu hiyo, shirika la Awda for Development halikuacha kukarabati madarasa. Lilielekeza sehemu kubwa ya bajeti katika ukarabati wa miundombinu ya maji na usafi, usambazaji wa matangi ya kuhifadhi maji na uwekaji wa milango ya ndani ili kuhakikisha faragha. Lakini cha muhimu zaidi ni namna maamuzi hayo yalivyofanyika. Badala ya mfadhili kuelekeza vipaumbele vya mradi kutoka juu kwenda chini, jamii ilihusishwa katika mchakato wa kufanya maamuzi.

Ahmad, ambaye ni mzazi kutoka kijiji cha al-Jurd al-Sharqi, anasimulia mabadiliko haya:

> 'Tulikuwa tukidhani kwamba mashirika haya yalikuwa yanakuja kutekeleza tu maagizo kutoka nje. Lakini wakati huu, walikaa pamoja nasi, akina baba, walimu wanawake na hata wanafunzi wenyewe. Walituuliza: Ni changamoto gani zinazowafanya watoto wenu kushindwa kuhudhuria shule? Hatukutarajia kwamba maoni yetu yangesikilizwa. Lakini walitusikiliza na wakachukua hatua kulingana na yale tuliyowaeleza.

Matokeo yake? Katika kipindi cha mwaka mmoja, idadi ya wasichana walioandikishwa shuleni katika eneo hilo iliongezeka kwa asilimia 32 na kiwango cha kuacha shule kilipungua kwa karibu asilimia 50. Takwimu hizi haziwakilishi mafanikio pekee, bali zinaonyesha utekelezaji wa kanuni muhimu ya msingi. Wakati wahusika wa ndani wanapopewa rasilimali na nafasi ya kutekeleza majukumu yao, mwitikio hubadilika kutoka afua za dharura na kuwa njia ya kuleta mabadiliko endelevu.

## Changamoto zilizofichika: wakati uongozi wa eneo unapofikia kikomo kisichoonekana

Licha ya mafanikio hayo, safari hiyo haikuwa bila vikwazo. Mojawapo ya mafunzo muhimu zaidi tuliyojifunza kutokana na uzoefu wetu ni kwamba changamoto zinazokabili mashirika ya ndani hazihusiani tu na uwezo wao wa ndani wa kiutendaji. Zinaonyesha kutokuwepo kwa usawa wa kina wa kimuundo uliojengeka katika mfumo wa kibinadamu.

Kwa mfano, data za tathmini ya ndani ya programu zinaonyesha kuwa asilimia 78 ya mashirika ya ndani yaliyoshiriki yalionyesha maboresho makubwa katika mifumo yao ya kifedha na kiutawala kutokana na msaada wa kina walioupata. Hata hivyo, ushiriki wao katika maamuzi ya kimkakati katika ngazi za juu uliendelea kuwa mdogo, huku mashirika ya ndani yakishikilia chini ya asilimia 15 ya nafasi za uongozi katika majukwaa makuu ya uratibu.

Suad al-Aswad, Mkurugenzi wa shirika la Change Makers (صانعات التغيير), linaloongozwa na wanawake na linalofanya kazi kaskazini-magharibi mwa Syria, anaelezea hali hii kinzani:

> ‘Tumejenga mifumo yetu ya ndani kwa kuzingatia viwango vya juu zaidi vya uwazi na weledi. Sasa tuna uwezo wa kuandaa ripoti za kifedha na kiutawala zinazoweza kulingana na zile za taasisi yoyote ya kimataifa. Lakini inapofika wakati wa kufanya maamuzi kuhusu vipaumbele vya mwitikio wa mwaka ujao, tunajikuta tukiwa ndani ya chumba kama watazamaji tu na si washirika. Maamuzi makubwa ya kifedha bado yanafanywa katika miji mikuu iliyo mbali na hutufikia yakiwa tayari yamekamilika.’

Ushuhuda huu unaonesha ukweli muhimu wa msingi. Kuimarisha uwezo wa ndani wa mashirika ya ndani pekee hakutoshi. Ni lazima hatua hiyo iambatane na mabadiliko ya msingi katika mgawanyo wa mamlaka ndani ya mfumo wa kibinadamu wenyewe.

## Uhamasishaji wa jamii na ujenzi wa amani: nguzo mbili za uendelevu

Kuzingatia masuala ya kiutawala na kifedha pekee hakukutosha kuhakikisha athari endelevu za mashirika ya ndani. CCSD ilitambua kwamba kuimarisha uhamasishaji wa jamii na kujumuisha mkabala wa ujenzi wa amani kulikuwa miongoni mwa mambo muhimu yaliyowezesha mashirika kubadilika kutoka kuwa watekelezaji wa shughuli na kuwa taasisi zilizojikita kwa kina ndani ya jamii zao. Badala ya kuwasilisha suluhisho zilizobuniwa tayari, tulishirikiana na mashirika washirika katika kutumia na kuimarisha mifumo ya uhamasishaji wa jamii ili kuhakikisha kuwa watu walioathiriwa wanashiriki kikamilifu katika kubainisha vipaumbele na kutekeleza miradi, jambo linalochochea umiliki wa ndani wa kweli.

Sambamba na hilo, tulijitolea kujumuisha kanuni za ujenzi wa amani kama mkabala wa kina na jumuishi katika hatua zote za programu. Mashirika yalijitahidi kubainisha maeneo ya udhaifu na migogoro iliyojificha ndani ya jamii zao, kisha kuyageuza kuwa fursa za ushirikiano na mshikamano wa kijamii. Mkabala huu wa pande mbili ulikuwa na mchango wa moja kwa moja katika kuimarisha uendelevu wa mashirika. Mashirika yaliyofanikiwa kutumia kwa ufanisi mbinu za uhamasishaji wa jamii na zana za ujenzi wa amani yalionyesha uwezo mkubwa zaidi wa kupanua vyanzo vyao vya msaada wa ndani na kujenga mahusiano ya kuaminiana na jamii pamoja na viongozi wa eneo husika. Hali hii ilisaidia kupunguza utegemezi wao wa kipekee kwa ufadhili wa nje na kuyawezesha kustahimili athari za kusitishwa kwa ufadhili kwa ghafla.

Uzoefu unaonyesha kwamba mashirika yanayowekeza katika kuimarisha mshikamano wa kijamii hujijengea nafasi ya kudumu ndani ya jamii, jambo linaloongeza uwezo wao wa kustahimili changamoto na kuendelea kufanya kazi kwa muda mrefu.

## Sauti kutoka uwanjani: viongozi wanawake wanazungumza

Mojawapo ya vipaumbele vya msingi vya programu ilikuwa kuimarisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi. Tulianza na wazo rahisi: mwitikio wa kibinadamu ambao hauongozwi na wanawake, au ambao wanawake hawashiriki kwa namna  yenye ushawishi, bila shaka utakuwa mwitikio usio kamili. Hatukutarajia kwamba wazo hili lingekuwa mojawapo ya hadithi zenye mafanikio makubwa zaidi za mpango huo.

Diana al-Ali, ambaye alianza kama mfanyakazi wa kujitolea katika kituo cha hifadhi miaka minane iliyopita, leo hii ni mkurugenzi wa shirika la Suryana linalofanya kazi kaskazini-magharibi mwa Syria. Akikumbuka siku zake za mwanzo, anasema:

> 'Mwanzoni, hakuna aliyetutusikiliza. Tulikuwa kundi la wanawake wenye ufahamu wa kina kuhusu jamii zetu, tulijua kuliko mtaalamu yeyote kutoka nje ni nani aliyekuwa akiathiriwa na ukatili wa nyumbani, ni familia zipi zilizokuwa na watoto wenye utapiamlo, na ni wanawake wajawazito gani waliokuwa wanahitaji huduma za haraka za afya. Lakini jukumu letu lilikuwa kutekeleza, si kuongoza.'

Kupitia programu yetu, Diana na timu yake walipata mafunzo mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitatu, yaliyolenga kuimarisha utendaji wa shirika katika nyanja za kiutawala na kiutendaji. Vilevile, alishiriki katika majadiliano yaliyowakutanisha viongozi wanawake wengine kutoka kaskazini-magharibi na kaskazini-mashariki mwa Syria, kama ilivyokuwa kwa mashirika yote 50 yaliyoshiriki katika programu hii.

Diana anazungumzia wakati muhimu uliobadili mwelekeo wa shirika lake:

> 'Kabla ya programu hii, tulikuwa tukisubiri maelekezo kutoka kwa washirika wa kimataifa kuhusu nini cha kufanya na jinsi ya kukifanya. Tulikuwa tukitekeleza mipango iliyoandaliwa na wengine. Mabadiliko ya kwanza ya kweli niliyoyaona yalitokea wakati programu ilipotutaka tuandae mpango wetu wa kimkakati kwa uwezo wetu wenyewe, na baadaye kutupatia zana na msaada wa kuutekeleza. Tulijifunza kuchanganua mahitaji ya jamii yetu si kupitia hojaji zilizotayarishwa mapema, bali kwa kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na wanawake katika mahema na kuwasikiliza kwa makini. Tulianzisha programu ndogo ya msaada wa kisaikolojia kwa wajane, baadaye, ambayo ilipanuka na kuwa mradi wa uwezeshaji wa kiuchumi, na hatimaye ikageuka kuwa jukwaa la utetezi wa masuala yanayowahusu. Leo hii, shirika la Suryana halisubiri tena mtu mwingine atuambie tunachohitaji. Tunakwenda kwa wafadhili na kusema: hivi ndivyo vipaumbele vyetu. Tusaidieni kuvifikia na kuvitekeleza kwa manufaa ya jamii zetu. Hiyo ndiyo tofauti kati ya kuwa mtekelezaji na kuwa kiongozi.'

Diana hakuwa peke yake katika safari hii. Suad al-Aswad, Mkurugenzi wa shirika la Change Makers (صانعات التغيير) mjini Idlib, kwa muda mrefu alikabiliana na hali ya kutengwa iliyosababishwa na kufanya kazi katika mazingira yenye mahitaji makubwa na yenye uongozi unaotawaliwa zaidi na wanaume. Anakumbuka:

> 'Viongozi wa ndani wa kiume walikuwa wakitutazama kana kwamba sisi ni 'shirika la wanawake tu' linalotoa mafunzo ya ushonaji." Mchango wetu haukuchukuliwa kwa uzito katika upangaji wa mikakati na vipaumbele vya mwitikio wa kibinadamu. Kupitia ushiriki wangu katika programu ya CCSD, nilijifunza mengi zaidi ya usimamizi wa bajeti na uandishi wa ripoti. Nilijifunza jinsi ya kujitokeza katika majukwaa ya uratibu wa ndani, jinsi ya kuwasilisha data kutoka kwa jamii yangu na jinsi ya kusimama imara kama mshirika mwenye mchango katika maamuzi, badala ya kuwa sauti inayosikika kutoka pembezoni. Leo hii, ninahudumu kama mshauri wa masuala ya wanawake katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii na ninaona sauti za wanawake sasa zinasikilizwa katika vikao vinavyoamua namna misaada inavyogawiwa.'

## Zaidi ya mafunzo ya jadi: uwekezaji katika mifumo ya ndani iliyounganishwa

Pengine somo muhimu zaidi tulilojifunza ni kwamba kuimarisha mashirika ya ndani hakumaanishi tu kuandaa warsha na vipindi vya mafunzo. Mara kwa mara, tulishuhudia mashirika yakipeleka wafanyakazi wao kwenye mafunzo ya kina, lakini athari za mafunzo hayo zikipotea mara tu waliporejea katika mazingira ya kazi ambayo hayakutoa msaada wa kuendeleza mabadiliko.

Kutokana na hali hiyo, tuliamua kutumia mkabala unaojikita katika ujifunzaji wa vitendo na uimarishaji wa mitandao ya ushirikiano kati ya mashirika. Badala ya kutegemea warsha za mara kwa mara zisizo na muunganiko, tuliunda majukwaa ya kudumu yaliyowawezesha viongozi wa mashirika ya ndani kukutana mara kwa mara, kujifunza kutoka kwa uzoefu wa kila mmoja na kutafuta suluhisho za pamoja kwa changamoto zinazofanana.

Ahmed Kallo, Mkurugenzi wa shirika la Green Heart (منظّمة القلب الأخضر) katika mji wa Aleppo, anasimulia kuhusu uzoefu huu:

> ‘Tulikuwa tukionana kama washindani katika kugombea ufadhili mdogo uliokuwepo. Leo hii, tuna jukwaa la WhatsApp ambapo tunashirikishana habari, fursa na ushauri wa kitaalamu unaotusaidia kuimarisha kazi zetu kama mashirika ya ndani.

Mitandao hii isiyo rasmi ilidhihirisha umuhimu wake wakati wa nyakati za migogoro. Wakati wa ongezeko la hivi karibuni la mapigano kaskazini-magharibi mwa Syria, mashirika yaliyokuwa sehemu ya mitandao hii yaliweza kuelekeza upya asilimia 45 ya rasilimali zao kwa ajili ya mwitikio wa dharura katika kipindi cha saa 48 tu. Jambo hili liliwezekana kutokana na kasi ya mawasiliano na kubadilishana taarifa kati ya mashirika, kasi ambayo ilizidi kwa kiwango kikubwa ile inayopatikana kupitia njia za jadi na rasmi za uratibu.

## Vikwazo vya kimuundo vinavyoendelea kudumu: kwa nini pengo bado lipo?

Licha ya maendeleo yaliyofikiwa, hatuwezi kudai kwamba changamoto zote zimetatuliwa kikamilifu. Data za programu yetu zinaonyesha kwamba mashirika ya ndani bado yanakabiliwa na vikwazo vya kimuundo ambavyo vinazidi uwezo wao binafsi wa kuviondoa. Vilivyojitokeza zaidi miongoni mwa vikwazo hivyo ni:

1. Uhuru mdogo katika kusimamia fedha na ufadhili Licha ya maendeleo yaliyopatikana, zaidi ya asilimia 85 ya fedha zilizopokelewa na mashirika yaliyoshiriki zilipitishwa kupitia mashirika ya kimataifa ya kati, hali iliyoweka mipaka katika uhuru wao wa kifedha na kuongeza mahitaji ya kiutawala yanayochukua muda na rasilimali nyingi.
2. Vipindi vifupi vya ufadhili: Asilimia 72 ya miradi iliyotekelezwa ilikuwa na muda wa chini ya miezi 12, hali iliyofanya upangaji wa kimkakati wa muda mrefu kutowezekana.
3. Kufanya kazi katika mazingira yenye utata mkubwa: Asilimia 83 ya mashirika yaliripoti kukabiliwa na changamoto za moja kwa moja za kiusalama na kiutawala ambazo ziliathiri uwezo wao wa kutekeleza miradi. Hali hii ilijumuisha changamoto za kupata vibali vinavyohitajika, vikwazo katika utembeaji na wakati mwingine hata kulengwa moja kwa moja.

## Mafunzo yaliyopatikana zaidi ya muktadha wa Syria

Uzoefu huu unatoa mafunzo muhimu kwa sekta ya kibinadamu duniani, miongoni mwao ni haya yafuatayo:

1. Ufadhili wenye unyumbufu si jambo la hiari; ni hitaji la msingi: Mashirika ya ndani yanapopewa nafasi ya kugawa upya rasilimali ndani ya bajeti zao, ufanisi unaweza kuongezeka kwa hadi asilimia 40.
2. Kuimarisha uwezo wa taasisi kunahitaji angalau miaka 3–5: Mafunzo ya muda mfupi pekee hayatoshi.

3. Uongozi wa wanawake sio suala la uwakilishi tu: Mashirika yenye uongozi unaojumuisha jinsia mbalimbali yanaonyesha uwezo mkubwa zaidi wa kuyafikia makundi yaliyotengwa na jamii.
4. Msisitizo wa programu katika kuimarisha uendelevu wa mashirika ya ndani ulichangia kuimarisha nafasi za kiraia na kuendeleza uwepo wao ndani ya jamii.

## Hatima ya uongozi wa kibinadamu

Kwa ujumla, uzoefu huu unabainisha kuwa kuimarisha uongozi wa ndani ni zaidi ya suala la kiutendaji pekee. Ni mabadiliko muhimu katika namna tunavyoielewa kazi ya mwitikio ya kibinadamu yenyewe. Swali si tena kama mashirika ya ndani yana uwezo wa kuongoza, bali kama mfumo wa kibinadamu uko tayari kwa dhati kutoa nafasi kwa uongozi huo.

Mmoja wa wanajamii waliofaidika na miradi midogo iliyotekelezwa na shirika la Sada (صدى) katika kambi ya Nour, kaskazini-magharibi mwa Syria, mama wa watoto watano, anaeleza hali hii kwa maneno yafuatayo:

> 'Sielewi hasa maana ya neno 'ujenzi wa uwezo'. Lakini ninachojua ni kwamba shirika lililonisaidia lilikuwa na watu kutoka mji wangu mwenyewe. Walijua jina langu. Walijua kuwa mwanangu anategemea dawa za matibabu ya muda mrefu. Walielewa kuwa sikuwa na uwezo wa kuondoka kambini peke yangu. Kama timu ya shirika hilo isingekuwa inanifahamu, huenda wangemchagua mtu mwingine kufaidika na mradi ambao mimi ndiye niliouhitaji zaidi.'

Maneno haya yanabeba kiini halisi cha uongozi wa ndani: si suala la ufanisi katika utekelezaji pekee, bali ni uwezo wa kujenga mahusiano ya kibinadamu hata katika mazingira magumu zaidi. Kuwekeza katika uwezo huu hakuongezi tu ufanisi wa mwitikio wa kibinadamu, bali pia huchangia kuhifadhi mshikamano wa kijamii na kuimarisha ustahimilivu wa jamii katika mojawapo ya mazingira yenye changamoto zaidi duniani.

**Moriab Gerges Haddo** ni meneja wa mradi katika shirika la Demos, linaloendesha shughuli zake katika mji wa Qamishli ulioko kaskazini-mashariki mwa Syria. Pia ni mtaalamu wa ujenzi wa amani mwenye uzoefu mkubwa katika kuimarisha ustahimilivu wa jamii, mshikamano wa kijamii na kuzuia vitendo vya siasa kali nchini Syria.

**Narges Ardwan**, kutoka mji wa Derik kaskazini-mashariki mwa Syria, ni mwanaharakati wa asasi za kiraia na meneja wa miradi anayefanya kazi katika nyanja za mwitikio wa kibinadamu, maendeleo na ujenzi wa amani katika shirika la Demos. Ana uzoefu mkubwa katika kubuni na kusimamia mipango ya kijamii na katika kukuza ushiriki wa wanawake na vijana katika majadiliano na michakato ya maamuzi katika ngazi ya kieneo.

**Muhammad Al-Kajak** ni mwanaharakati wa kiraia wa Syria, mwandishi na mhariri wa lugha. Ana stashahada ya uzamili katika Lugha ya Kiarabu kutoka Chuo Kikuu cha Aleppo na amefanya kazi na mashirika mbalimbali ya kimataifa na ya ndani yanayotekeleza shughuli zao kaskazini-magharibi mwa Syria.

# Mtendaji wa usaidizi wa kijamii asiyetambulika: mikakati inayoongozwa na wakimbizi katika eneo la Asia-Pasifiki na kwingineko

Baqir Bayani

Katika mwongo mmoja uliopita, sekta ya usaidizi wa kibinadamu imekuwa ikitoa wito wa mabadiliko kuelekea ujanibishaji. Mashirika ya kimataifa na wafadhili wanazidi kusisitiza ubia na ushirikiano wenye usawa, uongozi kutoka maeneo mahususi na husika, na uhamishaji wa rasilimali na uwezo wa kufanya maamuzi kwa wahusika na watendaji walio karibu na jamii zilizoathirika. Bado katika mazungumzo haya kuna kitendawili cha kushangaza: wakati sekta hiyo inajaribu kuimarisha mwitikio unaoongozwa na wenyeji, jamii zilizohamishwa kwa nguvu kutoka kwa makazi yao zinakosekana kwa kiasi kikubwa katika mifumo ya ujanibishaji.

Kama mweledi na mtu ambaye ameishi maisha ya kulazimishwa kuhama, ninaeleza kuwa mifumo ya ujanibishaji iliyopo inasalia kuwa duni kimuundo kuweza kujumuisha mikakati inayoongozwa na wakimbizi (RLIs). Ingawa mazungumzo ya hivi majuzi kuhusu Grand Bargain yameanza kutambua kwa uwazi mashirika yanayoongozwa na waliohama makazi yao, utangamano wangu na mashirika yenye nguvu unaonyesha kwamba mifumo ya uendeshaji shughuli inaendelea kutafsiri 'watendaji wa ndani' kimsingi kupitia ushirikiano na mashirika ya kitaifa yasiyo ya serikali (NGOs), mashirika ya kijamii ya kiraia ya jamii wenyeji, au taasisi za serikali za mitaa. Jamii za wakimbizi, hata hivyo, hujipanga chini ya hali tofauti za kisheria, kisiasa na kiulinzi. Kwa hivyo, RLIs mara nyingi hutengwa kutoka kwa ufadhili, ushirikiano na nafasi za kufanya maamuzi katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu; licha ya kwamba tayari zina jukumu la kiutendakazi. Ikiwa ujanibishaji utavuka usemi na kuelekea kwa mabadiliko halisi ya uongozi, lazima watendaji wa nje wa usaidizi wa kibinadamu waunganishe rasmi mikakati inayoongozwa na wakimbizi (RLIs) na waunde na watumie mifumo ya ushirikiano ili iendane sambambamba na hali halisi ambazo uongozi wa wakimbizi huibuka.

## Mipango inayoongozwa na wakimbizi kama waitikiaji wa kwanza na watendaji wa karibu

Katika miktadha mingi ya uhamishwaji, wakimbizi wanaishi ndani ya jamii zinazowapokea kwa miongo kadhaa katika hali zisizo na uhakika. Ingawa uhamaji wa kulazimishwa unachukua njia mbalimbali, wakimbizi na watu wanaotafuta hifadhi ambao wamevuka mipaka wanakabiliwa na vikwazo tofauti na vikali zaidi vinavyohusiana na hadhi yao ya kisheria, ajira rasmi, na kupata huduma za umma. Katika muktadha kama huo, RLIs mara nyingi huibuka kama mwitikio wa kijamii kwa hali halisi inayohitaji kushughulikiwa papo hapo. Kuanzia mitandao midogo ya watu wa kujitolea hadi mashirika yenye muundo rasmi, wanapanga programu za elimu, huduma za habari za kisheria, madarasa ya lugha, na mitandao ya usaidizi wa kijamii. Uzoefu kutoka Indonesia na Thailand unaonyesha jinsi mipango hii inavyofanya kazi kwa uhalisi.

### Indonesia

Kwa mfano, nchini Indonesia, ambayo haijatia saini Mkataba wa Wakimbizi wa 1951, wakimbizi hupitia mazingira yenye vikwazo vya kisheria, ambapo Kanuni ya Rais 2016 haizungumzii haki yoyote yakujumuishwa au kupewa ajira rasmi. Kufuatia utetezi wa mashirika ya kiraia wakitumia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto, Tangazo la Wizara ya Elimu la 2019 (nakala iliyopanuliwa katika mwaka wa 2022) liliwaruhusu watoto wakimbizi wenye kadi za Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia

Wakimbizi (UNHCR) kuhudhuria shule za mitaa, bila kuhitaji bajeti ya serikali. Ingawa haya ni mafanikio makubwa, sera hii inatumika kisheria kwa 'watoto wenye umri wa kwenda shule' (*anak usia sekolah*) chini ya mamlaka ya eneo. Wakimbizi wanapomaliza shule ya upili, wanakumbana na changamoto za kufuata taratiburasmi kwa kuwa kujiunga na chuo kikuu ni jukumu lililo chini ya sheria za kitaifa za uhamiaji zinazohitaji wanafunzi wawe na visa rasmi na pasi halali, na hivyo kuwafungia wakimbizi nje ya elimu ya juu.

Hata ndani ya elimu ya msingi, ingawa mabadiliko ya sera yanaweza kufungua milango ya shule za umma kihalali, vikwazo vikuu vya kihalisia vya ujumuishaji vimesalia. Kulingana na mawasiliano yangu na wakimbizi wenzangu, tofauti za lugha ni kikwazo kikuu. Kwa sababu familia nyingi zina matumaini ya kuhamishwa katika nchi inayozungumza Kiingereza, wazazi wanapendelea sana watoto wao wafundishwe kwa kutumia Kiingereza. Kwa hivyo, wanafunzi hawa wanapohamia shule za serikali za mitaa, wanakumbana na vizuizi vya lugha mara moja, ambavyo vinachangiwa zaidi na tofauti za kitamaduni, kutengwa katika jamii na kuonewa.

Kwa sababu mifumo rasmi inasalia kutofikika kwa kiasi kikubwa, kihistoria, RLIs nchini Indonesia zimeingilia kati ili kujaza mapungufu haya muhimu ya kitaasisi, muda mrefu kabla ya mabadiliko hayo ya sera kuanzishwa. Mipango ya kijamii kama vile vituo vya mafunzo vya wakimbizi yaani Refugee Learning Centre, Cisarua Refugee Learning Centre, The Sisterhood Community na vingine vinatoa elimu isiyo rasmi kila siku kwa watoto wakimbizi na watu wazima ambao vinginevyo wangeachwa nyuma. Zaidi ya elimu isiyo rasmi, mipango hii hupanga mafunzo ya kiufundi na shughuli za michezo, hutoa huduma za afya na usaidizi wa kisaikolojia, na huendesha programu za kubadilishana utamaduni na taasisi za eneo husika. Kwa sababu ya ukaribu wao, RLIs hizi hufanya kazi kama wapatanishi wanaoaminika na watoa huduma za kwanza wasio rasmi, wakitambua mahitaji yanayoibuka na kuhamasisha rasilimali za jamii muda mrefu kabla ya mashirika ya nje kuingilia kati. RLIs zinafanya kazi kama chanzo kikuu kinachodumisha mshikamano wa kijamii na ustahimilivu wakati wa usafiri usioisha

## Mpaka wa Thailand na Myanmar

Vilevile, kwenye mpaka wa Thailand na Myanmar, kamati za kambi zinazoongozwa na wakimbizi kwa muda mrefu zimeratibu huduma muhimu kwa wakazi zaidi ya 100,000 wa kambi, zikisimamia majukumu magumu ya kiutawala kwa pamoja na mashirika ya kibinadamu. Kwa utendakazi, hii ina maana kwamba kamati hizi hazifanyi kazi kama njia za usaidizi za kuitisha tu msaada; badala yake, hudumisha sajili kamili za idadi ya watu, huthibitisha idadi ya watu katika maboma, na kutekeleza utaratibu tata unaohitajika ili kusambaza mgao wa chakula wa kila mwezi kwa maelfu ya familia. Mbali na mitandao isiyo rasmi ya kujitolea, mashirika mengine makuu kama Kamati ya Wakimbizi ya Karen na Kamati ya Wakimbizi ya Karenni hufanya kazi kwa uwezo wa kiutawala na ukomavu wa urasmi wa mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyopo. Utawala wao umejikita sana katika uwajibikaji wa kidemokrasia, huku wakazi wa kambi wakipiga kura mara kwa mara kuchagua Kamati zao za Kambi, viongozi wa kanda na viongozi wa sehemu wanazoishi. Mara tu baada ya kuchaguliwa, vyombo hivi vinasimamia muundo rasmi uliogawanywa katika idara maalumu. Uongozi huu unasimamia vyombo vilivyojitolea kwa ajili ya kutoa elimu kamilifu (kama vile Taasisi ya Elimu ya Kamati ya Wakimbizi ya Karen), pamoja na mipango ya wafanyakazi inayosimamia uratibu wa afya ya umma, usalama wa kambi, vifaa vya mgao, na haki na utatuzi wa migogoro katika ngazi ya kambi.

Miundombinu hii tata ya watu waliochaguliwa kidemokrasia inaruhusu viongozi wa wakimbizi kusimamia maisha ya kila siku kwa ufanisi na kutoa huduma tata kwa makumi ya maelfu ya watu waliohamishwa kwa nguvu, ikithibitisha kwamba uongozi wa wakimbikzi tayari upo kama ukweli halisi katika miktadha mingi ya uhamishwaji. Kwa hivyo, mipango inayoongozwa na wakimbizi haipaswi kuchukuliwa kama watendaji wa pembeni au 'watu wanaonufaika' na programu za usaidiizi wa kibinadamu, lakini inapaswa kuthibitishwa kikamilifu na kuungwa mkono kama wachangiaji muhimu kwa mifumo ikolojia ya mwitikio wa ndani.

## Vikwazo vya kimuundo ndani ya mifumo ya ujanibishaji

Kutojumuishwa kwa RLIs kwa kiwango kikubwa si tu suala la ukosefu wa uzingatiaji wenye umakini; bali linaonyesha vikwazo vya kimfumo vilivyowekwa ndani ya sera za ujanibishajiina mifumo ya ushirikiano. Katika nchi nyingi zilizo wenyeji wa wakimbizi, sheria kali za ndani zinakataza wakimbizi kusajili rasmi mashirika, na hili hulazimisha RLIs kufanya kazi bila utaratibu na urasmi. Nchini Indonesia, kwa mfano, Sheria ya Mashirika ya Kijamii (UU Ormas) inawataka waanzilishi wawe na uraia wa Indonesia au vibali rasmi vya ukaazi (KITAS/KITAP), nyaraka ambazo wakimbizi wenye kadi za UNHCR hawana. Ukosefu huu wa msimamo wa kisheria unawaondoa moja kwa moja katika mifumo ya ushirikiano wa usaidizi wa kibinadamu, ambapo mahitaji ya kufuata sheria za wafadhili, michakato ya uchunguzi wa kifedha na mifumo ya ununuzi imeundwa kwa ajili ya mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyosajiliwa yenye uwezo rasmi wa kiutawala.

Masuala ya kuzingatia ulinzi yanawasilisha tatizo la ziada. Viongozi wa wakimbizi mara nyingi hufanya kazi chini ya hadhi isiyojulikana kisheria na wanaweza kukabiliwa na hatari zinazohusiana na jinsi wanavyoonekana na umma, utetezi, au ushirikiano na mamlaka. Miundo ya ushirikiano ambayo inapendelea mazingira ya utendakazi yaliyoimarishwa kisheria mara nyingi huenda ikawatia viongozi wa wakimbizi kwenye uwezekano wa kuathirika zaidi.



**Mfanyakazi wa Asylum Access akiendesha warsha nchini Tanzania kwa kundi la watu kutoka jamii ya wakimbizi. Picha ni kwa hisani ya: Gabriel Diamond**

Hatimaye, uongozi wa wakimbizi wenyewe huundwa kutokakana na hali za uhamaji. Wakimbizi wanaweza kupewa makazi ya kudumu, kuhamishwa kwingineko, kuwekwa kizuizini, kufukuzwa nchini, au kulazimishwa kuendelea mbele huku wakitafuta ulinzi au fursa. Ruwaza hizi za uhamaji zinatoa changamoto kwa mifumo ya ushirikiano inayozingatia uwepo thabiti wa shirika katika ya miktadha thabiti ya kijiografia.

Ingawa mahitaji ya ushirikiano ya kijadi na mahitaji ya kufuata sheria hutimiza madhumuni muhimu ya uwajibikaji, kimsingi yanapingana na hali halisi ya uhamishwaji na wakimbizi. Kwa kuchukulia kwamba washirika wana msimamo wa kisheria, mazingira salama na tulivu ya uendeshaji shughuli na uthabiti wa kijiografia, sekta ya usaidizi wa kibinadamu bila kukusudia huwatenga watendaji wa kijamii wa wakimbizi, hali inayopunguza uwezo wao wa kuendeleza kazi zao au kuongeza athari zao.

## RLIs kama watendaji wa ndani katika mfumo wa usaidizi wa kibinadamu

Licha ya kufanya kazi nje ya mifumo hii rasmi ya kisheria na kitaasisi, RLIs zinasalia kufungamana sana na jamii wanazohudumia, tayari RLIs zinatekeleza majukumu ya kiutendaji ambayo yanaangazia majukumu ya watendaji wengine wa ndani. Kwa hivyo, ikiwa ujanibishaji utakuwa jumuishi, lazima mfumo wa usaidizi wa kibinadamu uendane na hali halisi ya uhamishwaji badala ya kuwaadhibu wakimbizi kwa sababu ambazo hawawezi kuziepuka. Lazima RLIs zijumuishwe kwa uwazi katika ufafanuzi na uelewa wa utendakazi wa 'watendaji wa ndani'. Kuytambua  RLIs kama kategoria ndogo tofauti ni muhimu ili kuhakikisha kwamba juhudi za umiliki wa eneo wa mpango na shughuli hazifutilii mbali uongozi unaoongozwa na wakimbizi bila kukusudia. Hata hivyo, kushughulikia mapengo haya kunahitaji zaidi ya kufafanua fasili tu; kunahitaji mabadiliko ya kimsingi ya mawazo. Lazima mashirika ya kimataifa na wafadhili wabadilike kutoka kuona RLIs kama vikundi visivyo rasmi vya usaidizi wa kijamii hadi kujumuisha hizo RLIs kama washirika muhimu wa kiutendaji wenye faida za kipekee. Ili kupiga hatua kutoka kwausemi tu na kuondoa vikwazo vya kimuundo vinavyoufanya uongozi wa wakimbizi usionekane, lazima sekta hiyo itoe kipaumbele kwa mabadiliko muhimu ya kiutendakazi yafuatayo.

1. **Kubuni upya mifumo ya ushirikiano na ufadhili**. Lazima mifumo ya umiliki wa mipango na ushirikiano katika usaidizi wa kibinadamu iwe na msingi katika kanuni za usawa, uundaji wenye ushirikiano, na uwajibikaji wa pamoja. Mbinu jumuishi zaidi zinahitaji kuachana na mahitaji magumu ya kitaasisi na kukumbatia mabadiliko. Hii inajumuisha mbinu mbadala za ushirikiano, mipango ya ufadhili wa kati au mipango ya ufadhili wa pamoja, uchunguzi sawia kulingana na ukubwa wa ruzuku, na ratiba za programu zinazobadilika zinazokisi vyema hali halisi ya uendeshaji shughuli wa RLIs. Hasa, wafadhili wanapaswa kuchunguza utoaji ruzuku shirikishi na mifumo ya ufadhili wa moja kwa moja ambayo hutupilia mbali kimakusudi taratibu ngumu na nzito za kiutawala zilizowekwa za mashirika ya kijadi ya Umoja wa Mataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa. Kwa kufanyia majaribio mifumo ya uhisani inayotegemea uaminifu iliyoundwa kukidhi uwezo wa watu wa kawaida na mashinani, ufadhili unaweza kufikia RLIs zilizo kwenye mstari wa mbele kwa haraka na kwa ufanisi zaidi. Njia kama hizo zitawezesha RLIs kushiriki vyema katika mwitikio wa usaidizi wa kibinadamu bila kuweka mahitaji ya kimuundo ambayo RLIs haziwezi kuyatimiza.

2. **Fikira upya kuhusu hatari na mifumo ya kufuata sheria**. Mifumo ya jadi ya uchanganuzi wa hatari katika mifumo ya usaidizi wa kibinadamu kwa kawaida hutanguliza usimamizi wa hatari za kifedha na kiutawala. Hata hivyo, mara nyingi hupuuza hatari za ulinzi na za kisheria zinazowakabili viongozi wa wakimbizi wenyewe. Wahusika wa usaidizi wa kibinadamu wanapaswa kuunda miundo ya ushirikiano inayozingatia ulinzi ambao unatambua udhaifu unaohusishwa na uongozi wa wakimbizi. Hii inaweza kuhusisha kujadili hatari zinazoweza kuhusishwa na kuonekana kwenye umma katika mipango ya ushirikiano, kurekebisha fikra za umma ipasavyo ili kuepuka kuwafichua viongozi wa wakimbizi kwa mamlaka, na kurekebisha taratibu za kuripoti ambapo ufichuzi unaweza kuleta hatari za ulinzi.
3. **Jenga ushirikiano unaoweza kubadilika kulingana na uhamaji**. Tofauti na mashirika mengi ya ndani ya jamii wenyeji, RLIs hufanya kazi katika muktadha ambapo uhamaji ni sifa ya asili ya maisha ya jamii. Viongozi wa wakimbizi wanaweza kupewa makazi mapya, kuhamishwa kwingineko, kuwekwa kizuizini, au kulazimishwa kuhamia nchi nyingine, na hivyo kuvuruga mipango ya kawaida ya ushirikiano. Kwa hivyo, watendaji wa usaidizi wa kibinadamu wanapaswa kubuni mifumo ya ushiriki inayoweza kubadilika kulingana na hali ya uhamaji ambayo inaruhusu ushirikiano kuendelea hata wakati viongozi wa wakimbizi wanahama. Hii inahitaji mabadiliko kuhusiana na ucheleweshaji kutokana na mabadiliko katika uongozi, kuanzisha mifumo ya ushirikiano wa mbali, na kusaidia mitandao ya kidijitali inayovuka mipaka ya nchi ambayo inawezesha kushiriki maarifa hata wakati viongozi wanapohama katika muktadha mbalimbali.

## Hitimisho

Kadiri uhamishwaji wa watu katika eneo la Asia-Pasifiki na kimataifa unavyoendelea kubadilika, huenda jukumu la uongozi wa wakimbizi litazidi kuwa muhimu. Tayari RLIs zinachangia pakubwa katika uthabiti wa jamii, uwiano wa kijamii na utoaji wa huduma katika jamii za watu waliohama makwao. Hata hivyo, licha ya michango hii, mifumo iliyopo ya ujanibishaji mara nyingi inashindwa kuyatambua mashirika ya RLIs kama watendaji halali ndani ya mifumo ya kutoa mwitikio wa usaidizi wa kibinadamu. Kutambua RLI katika mifumo ya umiliki na uendeshaji shughuli za usaidizi kwa hivyo si suala la kufuata tu sheria. Ni hatua ya lazima kuelekea kufikiria upya kuhusu uongozi wa usaidizi wa kibinadamu katika usanifu unaobadilika unaowatambua wakimbizi sio tu kama wapokeaji wa misaada, lakini kama viongozi wanaounda mustakabali wa jamii zao wenyewe. Hata hivyo, ujumuishaji wenye maana unahitaji uwajibikaji. Lazima watendaji wa usaidizi wa kibinadamu na wafadhili waunde viashiria vya ujanibishaji mahususi vya wakimbizi - kama vile uwiano wa ushirikiano unaohusisha RLIs au sehemu ya ufadhili wa moja kwa moja na ubora unaotolewa kwao. Bila vipimo hivyo, uongozi wa wakimbizi una hatari ya kubaki bila kuonekana ndani ya ajenda pana ya ujanibishaji wa miradi kwa wenyeji.

**Baqir Bayani** ni mkimbizi, Mkurugenzi Mshiriki wa Ushirikiano wa Kimataifa na Uongozi wa Wakimbizi katika Upatikanaji wa Makazi ya Hifadhi, na mwenyekiti mwenza wa zamani wa Kikundi Kazi cha Ushirikiano wa Usawa katika Pledge for Change.

# Uongozi unaoongozwa na wakimbizi katika eneo la Cox Bazar

Khair Ullah na Ahtaram Shin

Katika eneo la Cox  Bazar, nchini Bangladesh, vijana wa asili ya Rohingya na mashirika yanayoongozwa na wakimbizi (RLOs) ni kitovu cha maisha ya jamii. Vijana hawa wanatekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa  watoa huduma za kwanza wakati wa dharura, kusaidia mifumo ya elimu na kuandika taarifa kuhusu masuala ya ulinzi. Hata hivyo, licha ya jukumu lao kuu, vijana hawa wanaendelea kuchukuliwa kama wasaidizi badala ya viongozi ndani ya mfumo wa usaidizi wa kibinadamu.

Makala haya yanahusu mahojiano na viongozi 50 wa mashirika yanayoongozwa na Warohingya, wanaowakilisha mashirika 50 yenye mamia ya wanachama katika kambi za Cox Bazar. Kulingana na majadiliano na viongozi wa jamii, kuna wastani mashirika 300 yanayoongozwa na wakimbizi (RLOs) yanayofanya kazi katika kambi hizo, mengi yake yalianzishwa baada ya 2017. Mashirika haya kwa kiasi kikubwa yanaongozwa na vijana na yalijitokeza ili kukabiliana na mapungufu katika utoaji wa huduma, uratibu na uwakilishi. Kazi ya mashirika haya inajumuisha  kutoa mwitikio wakati wa dharura, elimu, utetezi, kuweka kumbukumbu ya matukio,  na usaidizi kwa jamii.

Huku wahudumu  wa usaidizi wa kibinadamu wakizidi kusisitiza ujanibishaji na uongozi wa ndani, uzoefu wa RLOs katika eneo la Cox Bazar unaonyesha pengo linaloendelea kudhihirika kati ya matamshi na hali halisi. Makala haya yanachunguza jinsi uongozi unaoongozwa na wakimbizi unavyoonekana katika vitendo, vikwazo vya kimuundo vinavyouzuia, na kile kinachohitaji kubadilika ili uongozi unaoongozwa na wakimbizi utambuliwe na kuungwa mkono kikamilifu.

## Jinsi uongozi wa ndani ya eneo unavyoonekana kwa vitendo

Viongozi wa RLO walieleza kwamba uongozi wa wakimbizi katika eneo la Cox Bazar unamaanisha kusimama na kuunga mkono jamii yao katika hali ambapo serikali za kimataifa au mashirika ya misaada yanaweza kukosa kuelewa kikamilifu hali yao halisi. Kama kiongozi mmoja alivyosema, 'Tunahisi ni jukumu letu kushughulikia masuala yetu wenyewe.'

Uongozi pia unamaanisha kuwa sauti ya watu walio katika mazingira magumu, kutetea haki, kutafuta suluhisho na kutetea watu kurejeshwa nyumbani kwa heshima. Kwa viongozi wengi wa RLO, hii ina maana ya kuwatia moyo wakimbizi kushiriki kama wafanya maamuzi, wapangaji na watekelezaji katika programu za jamii zinazohusiana na elimu, ulinzi na usaidizi wa dharura, hata bila kutambuliwa rasmi kwa kazi yao.

Hata hivyo, viongozi wengi wa RLO walisema mara nyingi wao hushughulikiwa na mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) na mamlaka hasa kama watu wa kujitolea au wasaidizi badala ya viongozi wa jamii. RLOs haziwezi kuwafikia maafisa wa NGO au mamlaka ya kambi kwa urahisi, lakini wanajamii mara nyingi hutafuta msaada na mwongozo wa RLOs.. Kama kiongozi mmoja alivyosema, 'Watu wanatuamini na huja kwetu ili tushughuilikie matatizo yao.'

## Jukumu la mstari wa mbele katika matukio ya dharura

Viongozi wa RLO wana jukumu muhimu wakati wa dharura. Mnamo 2024, wakati vurugu huko Arakan zilipowafukuza maelfu ya watu kuelekea mpaka wa Bangladesh, wanachama wa RLO waliwasaidia watu waliojeruhiwa kufika hospitalini, wakawaokoa watu kutoka kwenye mashua karibu na Teknaf, na kutoa usaidizi wa dharura kwa familia zilizoathiriwa. Pia walituma chakula, dawa na nguo kwa watu waliobaki Arakan.

Ndani ya kambi, RLOs hukabiliana na moto, mafuriko, maporomoko ya ardhi na milipuko ya magonjwa kwa kubadilishana habari haraka na kutambua watu walio hatarini kama vile watoto, wazee na watu wenye ulemavu. RLOs zinakusanya na kusambaza vitu vya kimsingi kutoka kwa jamii na wakati mwingine hufanya tafiti ndogo ili kuelewa mahitaji ya dharura kabla ya NGOs kuitikia.

Hata hivyo, ni nadra sana kwa RLOs kujumuishwa katika upangaji rasmi wa mwitikio wakati wa dharura au uratibu. Kama vile mshiriki mmoja wa RLO alivyoeleza, 'Wao husikiliza maoni yetu kwa makini, lakini mwishowe, maamuzi hufanywa na wengine siku zote.'

## Mifumo ya elimu inayoongozwa na jamii

Katika mwaka wa 2017, kulikuwa na vituo vya kujifunzia vya mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) pekee katika kambi hizo, na hasa kwa ajili ya wanafunzi wa shule ya chekechea. Mashirika haya yalitoa vifaa vya kuchezea na vipindi vya masomo ya msingi ya kusoma, kuandika na kuhesabu. Haikujalisha ikiwa wanafunzi walikuwa watoto, vijana, au watu wazima; mfumo ulibaki kuwa mdogo sana. Baadaye, walimu wa jamii ya Rohingya walianza kutoa masomo ya kibinafsi kwa kupanga wanafunzi kulingana na viwango vya darasa. Hata hivyo, wengi wao walifundisha Kiburma, hisabati na Kiingereza tu. Baada ya muda, juhudi hizi zilikuzwa na kukua hadi vituo vya kijamii vya kujifunzia visivyo rasmi, ambavyo viliendeshwa kikamilifu kwa hiari. Kama vile mwalimu mmoja wa jamii alivyoeleza, 'Wengi wetu hufanya kazi tukiwa walimu wa kujitolea, wawezeshaji wa masomo, au washauri, tukiwasaidia watoto kuendelea na masomo ingawa hatuna nafasi ifaayo, shule, au vifaa vya kujifunzia.'

Mnamo 2020, wakati UNICEF ilipoanzisha Majaribio ya Mtaala wa Myanmar, ilishauriana na shule za jamii na kutumia maoni waliyopata ili kubuni na kutekeleza programu yake ya majaribio. Hata hivyo, programu hiyo ilitumia takriban wanafunzi 10,000 kutoka gredi ya 1 hadi 9. Programu hiyo ilitekelezwa kama mradi wa NGO wenye usimamizi mkali na malipo madogo, hali ambayo ilikatisha tamaa walimu wengi wa jamii waliohitimu kujiunga nayo. Kwa hivyo, walimu wa jamii waliendelea kuendesha shule zao wenyewe kwa kujitegemea kwa kukusanya karo ndogo kutoka kwa wanafunzi ili kuwasaidia walimu na kuendesha shughuli za kimsingi za shule.

Viongozi wa RLO pia wamekuwa wakifanya majadiliano na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Myanmar, katika juhudi za kufanya mitihani ya bodi ya kitaifa ya mitihani ipatikane kwa urahisi zaidi katika Cox Bazar. Kwa mfano, katika mwaka wa 2023, kwa mara ya kwanza shule 26 za jamii zilishirikiana kuandaa mitihani ya bodi na kufanya mitihani ya katikati ya muhula na ya mwisho wa mwaka huo. Katika mwaka wa 2025, walimu waandamizi na viongozi wa jamii walianzisha Bodi ya Mitihani ya Wakimbizi wa Rohingya. Wamefanikiwa kufanya mitihani ya katikati ya muhula na ya mwisho, na mpango huo umepata kuungwa mkono kwa ukubwa na jamii. Hata hivyo, mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) na mamlaka hayajaitambua bodi hiyo na kuiunga mkono rasmi. Shughuli nyingi huendelezwa kupitia michango ya hiari bila ufadhili maalumu au vifaa vinavyofaa.

Wakati baadhi ya vituo vya kujifunzia vya UNICEF na NGO vilipofungwa baada ya kupunguzwa kwa ufadhili katika mwaka wa 2025, shule za kijamii ziliendelea kufanya kazi. Kwa sasa, karibu 95% ya familia za Rohingya hutegemea shule hizi ili kusomesha watoto wao. Baadhi ya RLOs pia huwasaidia wanafunzi kwa kutoa vifaa vya kuandikia na vifaa vya kujifunzia.

Hata hivyo, mapengo kadhaa makubwa yanabaki katika mfumo wa elimu wa kambi za wakimbizi. Changamoto moja kuu ni ukosefu wa ushirikiano kati ya mamlaka ya utawala, NGOs na RLOs. Shule za kijamii na Baraza la Mitihani la Wakimbizi wa Rohingya hazitambuliwi kirasmi, ingawa ziliundwa ili kushughulikia mahitaji halisi ya kielimu. Bila kutambuliwa na kusaidiwa, shule hizi zinakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kujifunzia, madarasa na walimu waliopata mafunzo. Walimu wengi wanaendelea kufanya kazi bila malipo ya kawaida.

### Kurekodimasuala ya ulinzi

Kulingana na wawakilishi wengi wa Rohingya, kuandika na kuhifadhi masuala ya ulinzi na ukiukaji wa haki za binadamu pia ni lengo muhimu la kazi yao. Wanakusanya ushuhuda kutoka kwa watu walioathiriwa, ikijumuisha maelezo kama vile tarehe, saa, eneo na maelezo ya matukio. Ripoti hizi mara nyingi huhusisha masuala ya ulinzi wa watoto, unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi, dhuluma, na upungufu ulio katika utoaji wa huduma. Pia wamesaidia katika kurekodi na kuwasaidizi waathiriwa kuhusiana na michakato ya kimataifa ya kupata haki, kama vile Mahakama ya Kimataifa ya Haki na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Ikumbukwe kuwa RLOs hazifanyi uchunguzi rasmi. Jukumu lao hasa ni kurekodi kwa uwajibikaji na kupeleka kesi kwa mashirika ya haki za binadamu, wahusika wa ulinzi, au mashirika ya kibinadamu.

Hata hivyo, RLOs hukabiliana na changamoto katika uwekaji kumbukumbu na jukumu lao la kupeleka visa mbele kwa watendaji wengine. Changamoto hii hujitokeza katika mfumo wa upinzani kutoka kwa wanajamii na mamlaka za mitaa, ambazo wafanyakazi wa RLO wanaonekana wazi na wanaweza kufikiwa nao. Kwa mfano, mwanachama mmoja wa RLO alieleza kwamba waliporipoti shambulio la tindikali/asidi dhidi ya mfanyakazi wa kutwa kwenye mitandao ya kijamii, mamlaka iliwatishia waondoe chapisho hilo. Hali kama hizo hufanya iwe vigumu sana kwa RLOs kurekodi na kuzungumzia dhuluma.

## Changamoto kuu kwa uongozi wa wakimbizi

Changamoto kuu katika kusajili RLO ni hadhi ya wakimbizi wa Rohingya waliomo nchini Bangladesh. Bangladesh haijatia saini mikataba ya kimataifa ya wakimbizi, na Warohingya wanaruhusiwa kusalia tu nchini humo kwa misingi ya kibinadamu na maelewano ya nchi mbili. Kwa sababu hii, kusajili RLOs kunaonekana kama suala la uhuru wa nchi, kwani mamlaka inaweza kuliona kama kitendo cha utambuzi wa serikali. Kwa hivyo, wakimbizi hawaruhusiwi kisheria kusajili mashirika huru.

Kati ya RLO 50 tulizozungumza nazo, hakuna hata mmoja iliyosajiliwa rasmi katika nchi mwenyeji. Ingawa RLOs zingine zinatambuliwa na UN, haziruhusiwi kupokea usaidizi wa kifedha moja kwa moja kutoka kwa NGOs au wafadhili wa kibinafsi, na hawana vibali vya kisheria vya kufanya kazi. Kwa sababu ya vikwazo hivi, shughuli za RLO zinaendelezwa kwa njia isiyo rasmi ndani ya jamii na ndani ya mipaka ya kambi pekee.

Ni lazima RLOs ziombe ruhusa kutoka kwa Msimamizi wa Kambi ili ziendeshe shughuli yoyote. Kupata kibali ni vigumu sana na kunaweza kuchukua miezi, hata kwa warsha ndogo. Ingawa mamlaka haziwazuii kabisa wakimbizi kuunda mashirika, haziwaruhusu kufanya kazi kwa kujitegemea, wapata ufadhili, wajenga ubia na ushirikiano rasmi, au kujiunga na majukwaa ya uratibu. Hii inazuia mwonekano wao na ushiriki wao katika nafasi za kufanya maamuzi.

Wanachama wengi wa RLOs wana ujuzi, kujitolea, uzoefu wa kuishi na wanaaminika zaidi katika jamii. Ikiwa RLOs zingeruhusiwa kujiandikisha, zingeweza kukuza miradi, kujenga ushirikiano na ubia na mashirika ya misaada, na kuunda fursa za watu wengi kujipatia riziki.

Wafadhili kwa kawaida huhitaji usajili wa kisheria, akaunti za benki na idhini rasmi. Hata hivyo, RLOs za Rohingya haziruhusiwi kutumia mfumo wa benki wa Bangladesi au huduma za kifedha za simu. Kwa sababu hiyo, haziwezi kuomba ruzuku au mikataba mingi ya wafadhili. Mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) pia hayaruhusiwi kutoa ruzuku moja kwa moja kwa RLOs.

Kwa miamala ya kifedha, baadhi ya RLOs hutegemea njia zisizo rasmi, kama vile akaunti za benki katika nchi za kigeni au akaunti za watu wanaoaminika wa Bangladesh. Hata hivyo, mipango hii bado haijulikani na ni hatari. Kiongozi mmoja wa RLO alieleza kwamba:

> Chuo kikuu fulani cha Marekani kiliidhinisha ufadhili kwa shule yetu lakini kiliufutilia mbali ufadhili huo wakati hatukuweza kutoa maelezo ya benki chini ya usajili wetu wa RLO na nchi mwenyeji.'

## Ushirikiano

Kutokana na vikwazo vya kisheria na uhalali, Mashirika yasiyo ya Serikali (NGOs), wadau wa kimataifa, mitandao ya kijamii na mashinani, na wafadhili wakuu kwa ujumla hawawezi kuunda ushirikiano rasmi na mashirika yanayoongozwa na Warohingya katika kambi hizo. Kinyume chake ni kuwa, mashirika mengi ya Warohingya wanaoishi nje ya nchi hupokea ufadhili na usaidizi kutoka kwa nchi wenyeji. Wanaweza kusafiri, kufanya kazi kihalali, kuanzisha ofisi, na kushirikiana na mahakama za kimataifa, wanasheria na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali. Jambo baya ni kwamba RLO za kambi wa wakimbizi hazina fursa hizi.

Baadhi ya NGOs hushirikisha RLOs kwa njia isiyo rasmi kama watu wa kujitolea, wahamasishaji wa jamii, au washirika wa kufikia watu wengine, lakini mwingiliano huu ni mdogo na hauwezi kutegemewa. Ushirikiano kwa kawaida hulenga shughuli maalumu kama vile kampeni za uhamasishaji, kazi ya kujitolea, au kushiriki habari. Kama mwanachama mmoja alivyoshiriki:

> 'INGO moja iliwahi kualika klabu yetu ya sanaa kuonyesha kazi ya sanaa kwenye maonyesho ya kambi na ikachagua watu wawili wa kujitolea kwa mradi wao. Huo ndio ushirikiano wote tulioupata kutoka kwa NGOs.'

Kumekuwepo na ushirikiano mdogo mchache, kama vile ushirikiano wa kilabu ya sanaa mnamo 2025 uliobainishwa kwenye nukuu iliyo hapo juu. Mnamo 2020, Shule ya Filamu ya Omar ilipata msaada kutoka kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) kwa ajili ya mafunzo ya utengenezaji wa filamu na urembeshaji vitambaa, na katika mwaka wa 2021 UNHCR ilitoa usaidizi kwa jarida la Rohingyatographer. Zaidi ya mifano hii, ushirikiano na RLOs unabaki kuwa mdogo sana.



Maonyesho sodezi ya Klabu ya Sanaa ya Rohingya. Picha ni kwa hisani ya: Enayet Khan

Wakati mwingine mashirika yasiyo ya serikali hualika RLOs kwenye matukio au mashauriano, kama vile shughuli zinazoandaliwa kusherehekea Siku ya Wakimbizi Duniani au Siku ya Haki za Binadamu. Hata hivyo, ushirikiano huu mara nyingi hausababisha ushirikiano wa muda mrefu. RLOs pia hazina ofisi au nafasi za kufanyia mikutano, ingawa baadhi ya mashirika mara kwa mara hutoa kumbi za muda.

## Hitimisho na mapendekezo

Mashirika yanayoongozwa na Warohingya katika eneo la Cox Bazar yanaonyesha kwamba uongozi wa ndani ya kambi  tayari upo. Mashirika haya yanatoa mwitikio wakati wa  dharura, yanaendeleza mifumo ya elimu na kuunga mkono  shughuli za ulinzi kwa ajili ya jamii zao - mara nyingi bila kutambuliwa, ufadhili au usaidizi rasmi. Hata hivyo, mfumo wa usaidizi wa kibinadamu unaendelea kuwachukulia kama wasaidizi badala ya viongozi. Mashirika haya hayachukuliwi kama msingi wa kusaidia kuendeleza shughuli zifaazo na kumilikiwa na  jamii. Kuziba pengo hili kunahitaji zaidi ya ahadi za kusaidia jamii. Kunahitaji mabadiliko ya mifumo ya kisheria, mifumo ya ufadhili, miundo ya uratibu, utambuzi wa hadhi ya wakimbizi na mifano ya ubia ambayo kwa sasa haijumuishi wahusika wanaoongozwa na wakimbizi.

Mapendekezo yetu kwa wahusika na wadau wengi wanaohusika katika kambi za wakimbizi za Cox Bazar ni kama ifuatavyo:

- Kutambua na kusajili rasmi RLOs kama washirika halali.
- Kuwajumuisha viongozi wa RLOs katika michakato ya kufanya maamuzi.
- Kuanzisha mifumo imara ya uratibu kwa ajili ya ushirikishi wa wakimbizi katika mipango ya usaidizi wa kibinadamu na mijadala ya sera.
- Kuunda fursa za kujipatia riziki kwa wakimbizi.
- Kuunga mkono mipango ya kujenga uwezo wa vijana na RLOs.
- Kubuni programu kwa ushirikiano na RLOs.
- Kutoa ruzuku ndogo, nafasi ya ofisi, vifaa, na vifaa vya kujifunzia ili kuimarisha mipango inayoongozwa na jamii.

**Khair Ullah**, Mwenyekiti wa Kikundi Kazi cha Asia Kusini cha Mtandao wa Haki za Wakimbizi wa Asia na Pasifiki (APRRN) na mwanzilishi wa Resilience Refugee Alliance, ni mtetezi wa vijana wa jamii ya Rohingya, mtafiti, na mtetezi wa haki za binadamu ambaye kazi yake inakuza sauti za watu wa Rohingya na kutetea haki, elimu, na uwezeshaji wa jamii.

**Ahtaram Shin**, Naibu Mwenyekiti wa Kikundi Kazi cha Kijiografia cha APRRN na mwanzilishi wa Rohingya Youth Club, ni mwandishi, mtafiti, na mwanaharakati wa asasi za kiraia kutoka jamii ya Rohingya, pamoja na kuwa Mhariri Mkuu wa 'Rohingyatographer'.

# Zaidi ya Mwitikio: wanawake wanaoongoza hatua za kibinadamu nchini Palestina

## Ohaila Shomar na Majeda Saqqa

Kote nchini Palestina, mashirika yanayoongozwa na wanawake yanaendelea kudumisha jamii zao wakati wa mizozo ya muda mrefu, mauaji ya kimbari na mzingiro. Uongozi wao unahusisha kutoa mwitikio wa dharura pamoja na huduma za muda mrefu, kushughulikia mahitaji ya haraka ya kuokoa maisha na wakati huohuo kujenga upya maisha ya kijamii na ya jamuiyaa. Uongozi huu umejengwa juu ya uzoefu wa kimaisha, wajibu wa pamoja na uwajibikaji kwa wale walioathirika zaidi.

Makala haya yanazingatia tafakuri kutoka kwa mashirika mawili yanayoongozwa na wanawake, Shirika la Sawa na Chama cha Utamaduni na Mawazo Huru (CFTA), na yanachunguza jinsi uongozi wa kibinadamu unaoongozwa na wanawake unavyoonekana kivitendo na jinsi unavyofanya kazi katika mazingira yenye changamoto nyingi.

## Mwitikio endelevu katika mazingira ya migogoro

Kwa muda mrefu mashirika yanayoongozwa na wanawake nchini Palestina yamekuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na migogoro chini ya utawala wa kijeshi, yakifanya kazi ndani na nje ya mifumo yenye vikwazo ili kukidhi mahitaji ya dharura huku yakiendeleza uthabiti wa jamii. Uongozi wao hauanzi wala kuishia kwenye mwitikio wa dharura. Ni endelevu, hubadilika kulingana na mazingira na umejengwa juu ya uwajibikaji kwa wale walioathirika zaidi.

Hali hii ya sasa ya dharura imetufadhaisha sote na hivyo kuleta na kuongeza viwango vya vurugu zaidi ya ilivyotarajiwa. Imelazimisha timu ya Sawa kutathmini upya sera zilizokuwapo, kuimarisha mipango ya dharura, kufanya maamuzi ya kipekee pale inapobidi, na kutafuta mbinu bunifu za kurahisisha maisha ya watu wanaotafuta usaidizi, hata kwa kiwango kidogo.

### Huduma ya simu ya usaidizi ya Sawa na mafunzo yanayobadilika

Kitovu cha kazi ya Sawa nchini Palestina ni huduma yake ya kitaifa ya simu ya usaidizi isiyotozwa ada, ambayo hutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii, pamoja na ushauri wa kitabibu na wa kisheria. Kwa kutarajia hali mbaya zaidi, Sawa ilijiandaa kwa ajili ya kukatika kwa umeme kwa kuhakikisha inapata paneli za nishati ya jua na vipakatalishi, ili iendelee kutoa huduma ya simu ya usaidizi kutoka majumbani iwapo wafanyakazi hawangeweza kufika ofisini.

Sawa ilibadilisha mafunzo yake ya dharura kadiri idadi ya simu na ugumu wa kesi ulivyoongezeka, huku ikirekebisha mbinu zake ili kuweza kuwajumuisha kwa haraka washauri wenye uzoefu zaidi. Mwanzoni, mafunzo ya Sawa yalifanyika asteaste, kimakusudi na kwa upana. Mpango wa mafunzo wa saa 110 uliwavutia watu wa kujitolea kutoka viwango mbalimbali vya elimu, kuwaweka katika hali ya kuwajibikia jamii zao huku ukiwawezesha kutoa huduma za msingi za usaidizi wa kisaikolojia na kijamii. Hata hivyo, kadiri dharura ilivyozidi kuongezeka,utaratibu wa kazi ulianza kubadilika. Simu ziliongezeka, mahitaji yakawa ya dharura zaidi, na muda wa kuwaandaa washauri wapya ukawa mfupi zaidi. Kutokana na hali hiyo, Sawa ilibadilisha mbinu yake ya kazi. Kozi ya mafunzo ya saa 70 iliandaliwa ili kukidhi mahitaji ya mwitikio wa haraka. Ilibuniwa kwa ajili ya watu ambao tayari walikuwa na uzoefu fulani, ikijikita katika mahitaji ya hatua za mwanzo za dharura na kuimarisha ujuzi wao. Washauri waliwezeshwa kutathmini hali za afya ya akili, kutambua dalili za msongo mkubwa wa mawazo, na kuwajibikia rufaa, huku wakidumisha mbinu inayomlenga zaidi mteja katika huduma zao.

Walibadilisha si tu muda wa mafunzo, bali pia mpangilio na madhumuni yake. Mafunzo yalihamishwa kutoka kujenga msingi mpana wa maarifa hadi kuwezesha mwitikio wa haraka ulio makini na wenye msingi imara,ili kuhakikisha kuwa hata katika hali za dharura, utunzaji uliendelea kuzingatiwa, kuwajibikiwa na wenye ubinadamu. Hii iliwezesha usaidizi wa simu kuitikia wito kwa haraka zaidi na kwa ufanisi zaidi wakati wa shinikizo kubwa.

### Usaidizi endelevu katikati ya mahitaji yanayoongezeka

Jukumu la Sawa katika kuwezesha upatikanaji wa msaada wa vifaa lilikuwa muhimu sana wakati wa mashambulizi dhidi ya Gaza, ambapo mahitaji ya kimsingi ya kuishi yalikithiri katika simu nyingi zilizopokelewa Ili kusaidia hali hiyo, Sawa ilipanua juhudi zake kwa kutafuta rasilimali kutoka sekta mbalimbali na kufanya rufaa 41,457 tangu mwaka 2023. Idadi kubwa ya maombi ilisababisha kuanzishwa kwa nafasi maalumu ya kushughulikia maswali yanayohusu msaada wa vifaa, jambo lililowezesha washauri kujikita katika kutoa huduma bora za afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia na kijamii.

Licha ya usumbufu wa mara kwa mara na mabadiliko ya upatikanaji wa huduma, Sawa iliendelea kudumisha na kusasisha mifumo ya rufaa kwa kushirikiana na mashirika ya ndani na ya kimataifa. Huduma ya simu ya usaidizi iliendelea kufanya kazi bila kukatizwa na iliendelea kuwa ya bure katika eneo lote la Palestina kama inavyofahamika tangu zamani. Tangu kuongezeka kwa mashambulizi, Sawa imepokea simu 390,715 na kujibu simu 245,977 (63%), hali inayoonyesha ukubwa wa mahitaji pamoja na mwitikio endelevu wa shirika hilo katika mazingira yenye changamoto nyingi. "Wapigaji simu wanasema nini?" likawa swali kuu lililoongoza shughuli za kila siku.

Washauri walifanya kazi kwa karibu na familia zilizokuwa zikikabiliwa na maamuzi magumu katika wakati halisi. Mwanzoni mwa mashambulizi ya kijeshi ya Israeli, wapigaji simu walikuwa katika hali ya hofu wakiwauliza wahudumu wa Sawa ni wapi wangeweza kupata usalama: "Je, tufuate amri za kuhama au tusizifuate?" Huduma ya simu ya msaada ilifanya kazi kama sehemu ya mwitikio wa mstari wa mbele, ikiwasaidia watu katika wakati halisi walipokuwa wakikabili maamuzi magumu. (Angalia Kisanduku cha 1).

**Kisanduku cha 1: Mifano ya simu zilizopokelewa na Sawa operators**

- Mama mmoja aliyepiga simu akisema kuwa jeshi la Israeli lilikuwa limekaribia sana na hawakuwa na mahali pa kukimbilia.
- Baba mmoja aliyetupaazia sauti kwa hasira baada ya mwanawe kufariki kutokana na njaa iliyosababishwa na mzingiro uliowekwa na Israeli.
- Mwanamke aliyekuwa akiomboleza wanafamilia wake ambao hawakurudi kutoka katika maeneo ya usambazaji wa misaada yaliyosimamiwa na jeshi la Marekani.
- Mwanafunzi wa kike aliyefadhaika kwa kushindwa kufanya mitihani yake.
- Wazazi waliokuwa wakiwatafuta watoto wao waliopotea.
- Wafungwa walioachiliwa kutoka magereza ya Israeli ambao hawakuweza kupata chakula wala usaidizi.
- Kijana mdogo aliyekuwa akitafuta kazi na misaada ili aweze kuwahudumia ndugu zake
- Mwanamke na mwanamume waliokumbana na unyanyasaji wa kingono kutoka kwa wanajeshi wa Israeli.
- Mlezi aliyekuwa ametishia kujichoma moto pamoja na wanafamilia wake.
- Mwanamke aliyenyanyaswa na mume wake na kupoteza chanzo chake pekee cha usaidizi wa kifamilia.
- Wanawake walioshindwa kabisa na msongo wa mawazo
- Wanaume waliokata tamaa kwa kushindwa kuhudumia familia zao
- Yatima waliokuwa wakiomba msaada.
- Watu wenye ulemavu waliokuwa wakitafuta vifaa vya kuwasaidia kutembea na vifaa vingine vya usaidizi.
- Wakimbizi waliorejea kwenye makazi yao na kukuta nyumba zao na maisha yao yameharibiwa.
- Mwanafamilia pekee aliyebaki hai ambaye hakuwa na uhakika afanye nini baada ya hapo.

## Mwitikio wa Sawa kulingana na mahitaji mengi

Simu hizi hazikuishia katika kusikiliza tu. Zilibadilisha namna Sawa ilivyopanga mwitikio wake kwa wakati halisi. Familia zilipopiga simu zikiwa na hofu, zikiuliza pa kwenda au jinsi ya kuokoka katika masaa machache yajayo, washauri hawakutoa tu msaada wa kihisia, bali pia walieleza huduma zilizokuwa zinapatikana na kuwaunganisha watu na huduma chache zilizokuwa bado zinafikika. Simu nyingi kuhusu njaa, kuhama kwa lazima na ukosefu wa mahitaji ya msingi ziliifanya Sawa kuimarisha mifumo yake ya rufaa na kupanua uratibu wake na waigizaji wa ndani na wa kimataifa, ili kuhakikisha kuna njia za haraka za kupata chakula, malazi na huduma za afya. Katika hali za dharura kubwa, kama vile walezi waliokuwa wakionyesha nia ya kujiua au walipokuwa wakizungumza na manusura wa ukatili, washauri walitumia mbinu za kuingilia hali za dharura, walifanya tathmini za haraka za kiwango cha hatari, na waliendelea kuwa kwenye simu huku wakiratibu rufaa za dharura pale ilipowezekana.

Wakati huo huo, usaidizi wa Sawa si wa mara moja tu. Pale inapowezekana, ni  wa kujenga uhusiano na ni endelevu. Hili linaonekana katika visa kama cha Hiam, mama asiyeona mwenye watoto watatu aliyekuwa akikabiliana na kuhamishwa kutoka kwa makazi yake na kutengwa, ambaye mwanzoni alipiga simu akitafuta tu msaada wa vifaa na hakutaka kuzungumzia hisia zake. Baada ya muda, kupitia mawasiliano ya mara kwa mara na thabiti, huduma ya simu ikawa mahali alipoamini, akirejea si kwa ajili ya usaidizi pekee, bali pia kwa ajili ya kuunganishwa na wengine, kutafakari na kupata nafuu ya kihisia. Alianza kusimulia hadithi yake mwenyewe, akiieleza huduma hiyo ya simu kama mahali pekee ambapo aliweza kushusha mzigo wa moyo wake na kupata utulivu. Mfululizo huu wa utunzaji, ambapo wapigaji simu wanapokelewa tena na tena kwa uwepo na heshima, umejenga mbinu ya Sawa, ukiimarisha umuhimu wa kujenga uaminifu baada yaa muda pamoja na kutoa mwitikio wa haraka.


Kwa pamoja, uzoefu huu umeongoza shughuli za Sawa. Sawa ilianzisha jukumu maalumu la kushughulikia maombi ya msaada wa vifaa, na hivyo kuwawezesha washauri kuelekeza nguvu zaidi katika kutoa msaada wa afya ya akili, huku pia ikiimarisha mafunzo kuhusu athari za mfadhaiko, kihoro na mwitikio wa hali za dharura. Huduma hii ya simu ya usaidizi imekuwa si sehemu ya mawasiliano pekee, bali mfumo hai wa utoaji wa huduma unaobadilika kila siku, ukiwa umejengwa juu ya mahitaji ya dharura na pia kazi tulivu ya muda mrefu ya kuwasaidia watu wanapopitia migogoro inayoendelea.

## Mwitikio unaojengwa kwa kushirikisha jamii

Chama cha Utamaduni na Mawazo Huru (CFTA) kinatoa mfano mwingine wa uongozi unaoongozwa na wanawake na unaojengwa kwenye ushiriki wa jamii. Kilianzishwa mwaka 1991 na wanawake watano huko Gaza. Chama hiki cha CFTA kimejenga kazi yake juu ya kanuni kwamba jamii hazipaswi kusemewa na wengine, bali zinapaswa kujisemea zenyewe. Mtazamo huu unaonekana katika mtandao wake wa vituo vya jamii, ambapo wanawake, vijana na watoto hutambua vipaumbele vyao na kushiriki katika kubuni na kutekeleza programu mbalimbali.

Kuanzia siku za kwanza za mauaji ya kimbari, CFTA ilijihamasisha bila kusita. Ofisi na vituo vilipoharibiwa, timu zake zilivirekebisha na kuvifungua tena kwa kutumia chochote kilichopatikana, kuanzia mbao hadi mahema na miundo ya muda mfupi, licha ya uhaba mkubwa uliosababishwa na mzingiro. Juhudi hizi zilihakikisha kuendelea kwa elimu, huduma za afya na maeneo salama kwa wanawake, vijana na watoto.

Mwanzoni, watu waliokimbia makazi yao walifika wakiwa na dalili wazi za mateso; baadhi walikuwa wamejeruhiwa, wengine wakiwemo wanawake wajawazito waliokuwa wanahitaji huduma za haraka, na watoto waliodhoofishwa na magonjwa, hali iliyosababisha mahitaji ya dharura ya kibinadamu ambayo hayangeweza kusubiri. Huduma ilijitokeza kwa njia ya asili kutoka ndani ya jamii yenyewe. Miongoni mwa waliokuwepo ni muuguzi, mfanyakazi wa CFTA ambaye hapo awali alikuwa amefanya kazi katika Kituo cha Afya ya Wanawake, aliyeleta uzoefu wake wa kitaalamu katika hali hii mpya. Katika mazingira hayo tete, utaalamu uliambatana na uhitaji wa dharura, na kutoka kwenye kona ndogo iliyofaraguliwa, alianza kurejesha huduma za msingi za afya.  Hatua kwa hatua, kwa ushirikiano na wataalamu wengine, wafanyakazi na watu waliojitolea, kituo cha afya kinachofanya kazi kilibuniwa kutokana na kile kilichoanza kama  mwitikio wa dharura. Kituo ambacho kiliundwa kulingana na mahitaji ya watu, ustahimilivu wao, kujitolea na hatua za pamoja, badala ya kutegemea mfumo rasmi, na hatimaye kikaanza kutoa huduma za msingi za afya pamoja na huduma za afya ya uzazi na afya ya ngono.




**Daktari wa magonjwa ya wanawake katika kliniki ya CFTA iliyo kwenye kituo cha kuhifadhi watu waliokimbia makazi yao nchini Palestina akipitia matokeo ya uchunguzi wa ultrasound. Picha ni kwa hisani ya: Hanibal Zoroub, Kitengo cha Vyombo vya Habari cha CFTA**

## Kukabiliana na majonzi na kiwewe

Majonzi ambayo watu wa Gaza wanastahimili ni mazito zaidi kuliko yale yanayoweza kuitwa majonzi ya kawaida. Ni majonzi ya kupoteza kila kitu, si msiba mmoja tu; ni hali ambapo kila familia imelemewa sana na majonzi yake kiasi kwamba haiwezi kumsaidia mtu mwingine Hayatoi muda wa kupata nafuu. Kuna matarajio ya kudumu ya majonzi zaidi, na majonzi hayo yanagusa jamii nzima.

Wahudumu wa simu za usaidizi husikiliza kwa makini hisia hizi kila siku. Baadhi ya washauri nasaha hupata kiwewe mara ya pili wanaposikiliza simulizi za wapigaji simu ambazo zinafanana sana na majonzi yao wenyewe. Wafanyakazi wa Kipalestina katika sekta ya misaada ya kibinadamu hawatoi huduma tu kwa "wanufaika", bali pia kwa raia wenzao, marafiki zao, na pengine hata ndugu zao, wakiwa na huzuni kubwa na wasiwasi wa kila mara. Baadhi yao hujaribu kuficha hisia hizo ili waweze kuendelea na kazi zao za kila siku. Huku hali ikiendelea kuzorota kila siku pia katika West Bank, majonzi wanayohisi watu Gaza yanafanana zaidi na jeraha la ndani la kisaikolojia ambalo watu wengi hawataki, au hawawezi, kulikubali kikamilifu, hata wanapotafakari kwa kina.

Katika kusaidia hali hiyo, Sawa na CFTA zimekusudia kuanzisha mifumo ya utunzaji ndani ya mashirika yao Sawa imefanya hivyo kupitia mikutano ya mara kwa mara ya kufuatilia hali ya wafanyakazi ofisini, kwa kutoa nafasi kwao kushiriki jinsi wanavyokabiliana na hali hiyo na kupokelewa kwa uelewa badala ya matarajio. Wafanyakazi pia wanapata huduma za msaada wa afya ya akili, ili kuhakikisha hawapitii hali hiyo peke yao. Aidha, Sawa imeimarisha mifumo ya usaidizi kwa wenzao, imeandaa vipindi vya kutafakari kwa pamoja baada ya kushughulikia kesi ngumu, na pale inapowezekana imepunguza kiwango cha kazi ili kupunguza uchovu wa kupindukia.

CFTA imetanguliza ustawi wa wafanyakazi na watu wa kujitolea kwa kuunda maeneo madogo muhimu ya kutoa msaada ndani ya mazingira yenye changamoto nyingi. Kupitia shughuli za kupunguza msongo wa mawazo, msaada wa kisaikolojia na kijamii, vikao vya kutathmini matukio , na mipangilio badilifu ya kazi katika mazingira yasiyotabirika, shirika limejitahidi kudumisha ustawi wa kihisia na kuimarisha uthabiti wa pamoja.

Mbinu hizi zinatambua kwamba kuendelea kuwahudumia wengine kunahitaji kuwajali kikamilifu wale wanaotoa huduma hiyo, hasa katika mazingira ambapo mpaka kati ya huzuni ya kibinafsi na ya kikazi ni finyu mno.

## Hitimisho

Mashirika yanayoongozwa na wanawake nchini Palestina yanaonesha kwamba uongozi wa kibinadamu wa ndani si jambo linalohitaji kujengwa kuanzia mwanzo: tayari upo na tayari unatoa mwitikio hata katika mazingira magumu zaidi.

Huduma ya simu ya msaada ya Sawa na kazi ya kijamii ya CFTA zinaonesha kwamba uongozi ni endelevu, hubadilika kulingana na hali, na umejikita kwa kina katika uhalisia wa maisha ya watu Uongozi huo unafanya kazi katika mwitikio wa dharura na msaada wa kijamii, mara nyingi bila kutambuliwa, bila rasilimali za kutosha, au bila msaada wa kimuundo unaotolewa kwa wadau wakubwa wa masuala kibinadamu.

Kwa watendaji wa kimataifa wa masuala ya kibinadamu, hali hii inaibusha maswali muhimu. Ina maana gani kubuni mwitikio unaojengwa juu ya uongozi ambao tayari upo ndani ya jamii badala ya kuupuuza? Mifumo inaweza kubadilika vipi ili kusaidia mashirika yaliyojikita ndani ya mgogoro, badala ya yale yaliyo nje ya migogoro hiyo? Na ushirikiano unaweza kukua zaidi ya kushauriana tu na kuwa ushirikiano wa kweli wa uongozi?

Huku sekta hii ikipitia mabadiliko mapana, uzoefu wa mashirika yanayoongozwa na wanawake nchini Palestina unatoa ujumbe wazi: mwitikio bora wa kibinadamu hauhusu tu kuwafikia watu walio katika mgogoro, bali pia kutambua na kusaidia wale ambao tayari wanaongoza ndani ya mgogoro huo.

**Ohaila Shomar** ni mwanzilishi wa Shirika la Sawa nchini Palestina na mwanaharakati mashuhuri wa haki za binadamu anayejikita katika masuala ya ukatili wa kingono na wa kijinsia. Ameanzisha huduma nyingi za simu za usaidizi kwa manusura, ameandika programu za kupinga ukatili, na hutoa ushauri kuhusu haki za wanawake na watoto.

**Majeda Saqqa** ni mmoja wa waanzilishi wa Chama cha Utamaduni na Mawazo Huru , kilichoanzishwa mwaka 1991. Yeye ni mwanaharakati anayefanya kazi katika masuala ya haki, uadilifu na uthabiti wa jamii.

# Kuanzia data hadi utawala: kuwaweka wanawake waliohamishwa kutoka kwa makazi yao katika nafasi kuu za maamuzi ya tabianchi na masuala ya usaidizi wa kibinadamu

Anila Noor na Madina Yuni

Majanga yanayohusiana  na tabianchi yanazidi kuwa makali na yanaendelea kutokea mara kwa mara, hali inayoongeza uhamaji katika maeneo dhaifu na yaliyoathiriwa na migogoro. Katika maeneo ambayo ni makazi ya wakimbizi kama vile Dadaab na Hagadera katika Kaunti ya Garissa, nchini Kenya, vipindi virefu vya ukame, mvua isiyotabirika na mafuriko huathiri maisha ya kila siku moja kwa moja. Hata hivyo, hatua za usaidizi wa kibinadamu zinazuiwa na mifumo isiyotosha ya kukusanya data na kutengwa kwa idadi kubwa ya watu walioathiriwa zaidi kunakoendelea, hasa wanawake na wasichana waliokimbia makazi yao. Ukosefu wa data mahususi ya kijinsia na ya data ya mwingiliano wa masuala mbalimbali ni zaidi ya masuala ya kiufundi, hali inayoficha ukosefu wa usawa wa kimuundo katika michakato ya uundaji wa maarifa, uthibitishaji na matumizi. Kwa kurejelea mifano kutoka Kenya, makala haya yanachunguza jinsi mashirika yanayoongozwa na wanawake wakimbizi yanavyobuni mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya tabianchi kupitia uundaji  wa programu kwa ushirikiano, mifumo shirikishi ya data na ushiriki wa kweli. Mbinu hizi zinaonyesha kwamba kuingiza uzoefu wa maisha ya watu katika michakato ya ukusanyaji wa data na ufanyaji wa maamuzi kunaboresha ulengaji, ufanisi na uendelevu wa mipango ya kibinadamu.

## Mwingiliano kati ya jinsia, mabadiliko ya tabianchi na uhamishwaji

Katika maeneo kama Kenya, mabadiliko ya tabianchi, uhamaji na ukosefu wa usawa wa kijinsia huungana ili kuunda kile ambacho baadhi hukiita, 'mkusanyiko wa uwezekano wa kuathirika vibaya.' Matukio kama vile ukame wa muda mrefu au mifumo ya mvua isiyotabirika husababisha uhamishwaji miongoni mwa watu, huku kiwango cha kuhama kikitegemea vipengele vya ukosefu wa usawa uliopo. Wengi wa wale waliohama makazi yao wanaishi katika maeneo yanayoweza kuathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi, ambapo miundombinu haitoshi, rasilimali ni chache, na miundo ya utawala ni dhaifu. Wanawake na wasichana katika maeneo haya hukabiliwa na matatizo mengine zaidi, ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa kupata ardhi na rasilimali za kifedha, kuongezeka kwa majukumu ya utunzaji yasiyolipwa, na hatari kubwa kwa usalama wa mtu binafsi.

Lakini tukiangalia tu uwezekano wa kuathirika pekee tutakosa kuelewa sehemu muhimu ya hadithi hii. Wanawake waliokimbia makazi yao wana jukumu muhimu katika kusaidia jamii zao kusalia imara na kukabiliana na migogoro. Wanawake hawa huwa waitikiaji wa kwanza, wakisimamia mahitaji ya haraka nyumbani na katika jamii zao; wasimamizi wa rasilimali, wakihakikisha kuwa chakula, maji na mafuta au kuni vinapatikana wakati wa uhaba; ni wamiliki wa maarifa na ujuzi wa kijamii, wanatumia uzoefu wa ndani ili kuweza kuishi; na wanawake ni viongozi wa jamii, wakiweka watu pamoja na kutatua migogoro.

Majukumu haya ni muhimu kwa ajili ya kuishi vyema na kwa ustahimilivu wao na jamii zao. Hata hivyo, mifumo ya usaidizi wa kibinadamu mara nyingi huwapuuza, ikiwaona wanawake wakimbizi kama wapokeaji wasiojali. Ukosefu huu wa kuelewa nafasi ya wanawake una madhara makubwa. Hili hupunguza ni nani anayeshauriwa, husababisha programu zinazopuuza hali halisi za ndani ya eneo mahususi, na hupunguza uwezo wa kufikia ufadhili na majukumu ya uongozi. Kwa hivyo, juhudi zinazofanywa zinaweza kushindwa kutumia uwezo uliopo, na kusababisha ukosefu wa ufanisi na kupoteza fursa za kuleta athari ya kudumu.

## Pengo la kimfumo: data, utawala na kutengwa

Changamoto kuu ni kushindwa kwa mifumo katika jinsi data inavyoundwa, inasimamiwa na kutumika katika mifumo ya usaidizi wa kibinadamu. Mara nyingi data huchukuliwa kama chombo kisichoegemea upande wowote cha kufanyia maamuzi. Kwa kweli, Kwa kweli, inaakisi na kuimarisha ukosefu wa usawa katika madaraka. Ingawa programu nyingi za usaidizi wa kibinadamu hukusanya data ya msingi isiyogawanywa kijinsia, mara nyingi programu hizi hukosa data yenye uelewa zaidi, data inayoonyesha miingiliano ya hali mbalimbali ambazo zinaakisi jinsi mambo kama vile umri, ulemavu, hadhi ya kisheria na kuhamishwa yanavyounda uzoefu tofauti. Kisha programu hutatizika kuwafikia wale wanaohitaji usaidizi zaidi. Muhimu zaidi, suala sio tu ni data gani inayokusanywa lakini pia ni nani anayeidhibiti. Kwa kawaida, wahusika wa nje huweka vipaumbele, hukusanya data bila kushikirikisha jamii kikamilifu, na kuichanganua mbali na hali halisi ya eneo husika. Wale walioathirika hupokea maoni na majibu machache.

## Kuibuka kwa 'Kente Threads'

Katika mazingira ya mabadiliko ya tabianchi nchini Kenya, mradi wa ‘Kente Threads’ unashughulikia masuala ya kimfumo kikamilifu. Mradi huu uliundwa kwa pamoja na wanawake waliohama makwao na kwa ushirikiano wa mashirika ya wanawake. Mradi huu, uliochochewa na kitambaa cha kitamaduni cha Kente cha Afrika Magharibi, unaonyesha wazo kwamba kila aina ya nyuzi huashiria hadithi, utambulisho au historia mahususi. Mradi unatambua kuwa wanawake na wasichana waliohama makwao wanapitia hali mbalimbali za maisha badala ya kuwa na hadithi moja inayofanana. Mradi huu unatumia mbinu inayounganisha uhalisia mbalimbali wa kibinafsi, ukitambua na kuheshimu kila ‘uzi’, ambao umeathiriwa na mambo kama vile jinsia, uhamishwaji, ulemavu, mwelekeo wa kijinsia, umri na majukumu ya kijamii. Mradi unaleta pamoja uhalisia tofauti wa kibinafsi wa makundi mbalimbali ya wakimbizi yanayoongozwa na wanawake, ikiwa ni pamoja na wanawake na wasichana wenye ulemavu, na wanawake wasagaji, mashoga, wanawake wanaopenda jinsia zote mbili, wanawake waliobadili jinsia, wanaohoji jinsia yao (LBTQI+), ili kwa pamoja kutoa data inayotokana na uzoefu wao wa maisha.

Kupitia mbinu shirikishi, vikundi hivi vinaongoza ukusanyaji wa data ndani ya jamii zao, hali inayorekodi hali halisi ambayo mara nyingi hupuuzwa au kutengwa. Kisha wanapata usaidizi wa mafunzo ya uchanganuzi wa data, pamoja na uimarishaji wa uwezo wa kishirika unaombatana na mahitaji ya shirika, na hii inawawezesha kuelewa na kumiliki data zao. Mchakato huu unawaweka sio tu kama washiriki, lakini kama viongozi, wanatumia ushahidi ambao wameunda ili kuendesha shughuli za utetezi na kupendekeza suluhisho kwa matatizo ya jamii zao. Hii inapinga mazoea yanayotumika kwa kila mtu, kwa kuunda mbinu moja inayoweza kutumika kwa wote, mbinu ambayo kwa kawaida hutumika katika mifumo ya sasa ya data na inakataa mbinu ambazo zinachukulia mashirika yanayoongozwa na wanawake wakimbizi kama washiriki waliopo tu bila utetezi wowote. Wazo la ‘kukuza’ nyuzi za Kente linaonyesha jinsi wanawake wakimbizi wanavyoendelea kukuza ujuzi huu.

## Kutumia Kente Threads katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

Ili kuongeza uelewa zaidi, mtu anaweza kuchunguza kambi ya Hagadera, ambapo vikundi vinavyoongozwa na wanawake vinaandika kwa njia isiyo rasmi athari za mabadiliko tabianchi kupitia mazungumzo ya kijamii na vikundi vya kuweka akiba vya kijamii, kama vile Vyama vya Akiba na Mikopo vya Vijiji (VSLAs). Majukwaa haya hutumika kutimiza majukumu mbalimbali kama vile njia za usaidizi wa kifedha na majukwaa muhimu ya kubadilishana uzoefu na tafakari ya pamoja. Wakati wa mikutano ya mara kwa mara, wanawake hujadili masuala kama vile uhaba wa maji, kupanda kwa bei ya vyakula, unyanyasaji wa kijinsia (GBV), na mabadiliko ya mifumo ya mvua. Kwa mfano, katika mazungumzo ya VSLA, mara nyingi wanawake husisitiza kwamba misimu ya mvua isiyotabirika na isiyo na uhakika imesababisha hasara ya mara kwa mara ya kupoteza mifugo pamoja na kutatiza maisha ya watu walio katika hatari. Pia wanafuatilia jinsi ukame unavyoongeza hitaji la kwenda masafa marefu ili kutafuta maji na kuni, hali inayoibua wasiwasi kuhusu usalama, huku mvua kubwa ikisababisha mafuriko ambayo yanaharibu makazi na kuchafua vyanzo vya maji. Uzoefu huu tofauti, unaoathiriwa na jinsia, umri, ulemavu na hadhi ya waliiohamishwa, huunda 'nyuzi' za kipekee za data ambazo mara chache hunaswa na mifumo rasmi.

Kwa kuchambua data hii kwa ushirikiano, wanawake hutambua hatari mpya. Ingawa matukio haya yanajitokeza zaidi katika kiwango cha kila kaya, maelezo na kumbukumbu ya matukio haya huwa haiwekwi katika mifumo rasmi ya ukusanyaji wa data. Hata hivyo, matukio haya yanatoa maarifa ya papo hapo, yanayohusiana na muktadha mahususi kuhusu jinsi mabadiliko ya tabianchi huathiri maisha ya kila siku katika hali za uhamishwaji.

Kupitia kwa uchanganuzi wa pamoja wa uzoefu huu, wanawake sio tu kwamba wanatambua hatari zinazojitokeza lakini pia huendeleza mwitikio wa vitendo, unaotokana na hali halisi ya maeneo yao. Mwitikio huu ni pamoja na marekebisho ya mikakati ya kupata riziki, uimarishaji wa mitandao isiyo rasmi ya usalama, na uratibu wa mifumo ya kijamii ya kugawana rasilimali. Kwa namna hii, wanaonyesha kuwa wanawake waliohama makwao sio tu watu wanaotumiwa kupata data bali ni wazalishaji mahiri wa maarifa na wafanya maamuzi ambao maarifa yao ni muhimu kwa juhudi zinazofaa na zinazojumuisha tabianchi na misaada ya kibinadamu.

## Wanawake kama wamiliki wa data zao

'Kente Threads' inafafanua upya mamlaka katika data kwa kuhamisha udhibiti kwa wanawake waliohamishwa kutoka makwao kama washiriki wakuu. Tofauti na mifumo ya kitamaduni inayoona jamii kama vyanzo vya data tu, mbinu hii inawahusisha wanawake kama wabunifu wenza, watafiti wenza na viongozi wenza wanaochagua maswali, wanaoongoza ukusanyaji wa data, wanaotafsiri matokeo na wanaoongoza juhudi za utetezi. Mbinu hii inachukua nafasi ya mifumo ya kupata tu data kwa wanajamii kwa kuhakikisha wanajamii wanashawishi mchakato na maamuzi. Ridhaa, uwajibikaji na mrejesho ni muhimu katika kila hatua, huku data ikiundwa kwa ushirikiano ili kuwezesha jamii kuwakilisha na kuunda masimulizi yao.

Mfano dhahiri wa mbinu hii unaonekana katika kazi ya Mpango wa Wasichana Wafugaji (Pastoralist Girls Initiative- PGI) huko Hagadera. Kwa kushirikiana na Shirika la Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji, PGI inatoa mafunzo kwa wanawake na wasichana kama wakusanyaji data, na hivyo basi kuwapa uwezo wa kusimamia ukusanyaji wa data ndani ya jamii zao. Mkakati huu sio tu kwamba unaongeza ubora wa data lakini pia unaimarisha uwezo wa wenyeji na kukuza umiliki wa mchakato huo. Zaidi ya kukusanya data, wanawake na wasichana hufanya ukaguzi wa usalama unaoongozwa na wanawake katika jamii za wakimbizi na jamii wenyeji. Ukaguzi huu hutathmini hatari mbalimbali za usalama, zikiwemo zile zinazochangiwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi , kama vile uhaba wa maji, ongezeko la uwezekano wa kuathiriwa na vurugu wakati wa kukusanya rasilimali, na hatari zinazohusiana na uhamishwaji na majanga ya kimazingira.



**Ziara ya ufuatiliaji iliyofanywa na wawakilishi kutoka shirika la Pastoralist Girls Initiative (PGI) wakati wa mkutano wa kikundi cha wanawake cha VSLA huko Hagardera, Kaunti ya Garissa, Kenya. Picha ni kwa hisani ya: PGI**

La muhimu ni kwamba, mchakato hauishii na ukusanyaji wa data. Wanawake na wasichana wanasaidiwa katika kufasiri matokeo na wanapewa majukwaa ya kutetea hatua zinazohitaji kuchukuliwa. Kupitia kwa majukwaa haya, wanashirikiana na watendaji wa usaidizi wa kibinadamu, watoa huduma na uongozi wa jamii kuhusu masuala ya kipaumbele yaliyobainishwa kupitia kwa ukaguzi. Muundo huu hauongezei tu umuhimu kwenye data, usahihi wa data pamoja na kuleta matumizi ya data yafaayo, lakini pia unahamisha mamlaka kwa kuhakikisha kwamba wale walioathiriwa zaidi huathiri moja kwa moja maamuzi yanayounda usalama wao, uthabiti na mustakabali wao. Mbinu hii inaufanya mpango kuwa wa kipekee na wenye nguvu. Kwa kutumia Kente Threads kufuatilia athari za tabianchi, mradi unakusanya data inayokosekana kuhusu jinsia na vikundi vya kijamii. Ubadilisha jinsi maarifa yanavyojengwa na kushirikiwa, kwa kuwa wanajamii wanachangia maarifa yao na kuyaunganisha na mifumo ya sasa.

Vikundi vinavyoongozwa na wanawake wakimbizi hukusanya data kupitia michakato iliyokita mizizi na inayoongozwa na jamii, katika maeneo tulivu, yanayofahamika, chini ya miti, majumbani, katika vituo vya kijamii, ambapo wanawake, wasichana na watu wa jinsia tofauti hutafakari kwa pamoja jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri maisha yao, na kuzungumza kwa wakati wao. Vinakusanya hadithi kupitia kwa

ushuhuda simulizi, mazungumzo baina ya vizazi, na kuchora ramani ya pamoja ya mabadiliko ya mazingira, wakichukua uzoefu uliopo kama aina ya ushahidi. Wanashiriki hadithi za mabadiliko ya misimu, mavuno yaliyofeli, joto linaloongezeka na kuhamishwa kutoka kwa makazi. Maarifa yanakusanywa, sio kama hali ya kuchakura data, bali kama kitu kinachomilikiwa kwa pamoja, kupitia usimulizi wa hadithi, usikilizaji wa tafakari zinazovuka vizazi.

## Maarifa ya eneo husika, majibu ya eneo husika

Wanawake hupanga mabadiliko haya kwa mikono yao wenyewe, wakifuatilia vyanzo vya maji ambavyo vimepotea, ardhi ambayo haitoi mazao tena, na njia wanazotumia sasa ili kupata riziki na kuishi. Badala ya kutegemea mahojiano rasmi pekee, wanashirikisha wanajamii wanaoaminika, wakiwemo viongozi wa dini, wakuu wa jamii na viongozi wanawake, katika mahusiano yanayoendelea ya uwajibikaji na matunzo, hali inayohakikisha kwamba maarifa yanayotolewa yana msingi, ni ya pamoja na yanamilikiwa na jamii. Kwa njia hii, data inakuwa kitu ambacho watu wameishi na kukupitia, kinachotokana na utunzaji, kumbukumbu na uzoefu wa kila siku, na mamlaka huanza kurejea mikononi mwa wale ambao wana ufahamu na uzoefu. Wanajifunza uchanganuzi wa data, na kufanya utetezi. Wanatumia ujuzi huu kuonyesha kile kinachohitaji kubadilishwa, na kwa jinsi gani. Data zao huongoza maamuzi ya kivitendo kuhusu makazi, huduma za afya na matumizi ya rasilimali.

Takwimu zao huongoza maamuzi ya kivitendo kuhusu makazi, huduma za afya na matumizi ya rasilimali.

Kwa mfano, wanawake kule Dadaab walipanga mfumo wa haki wa usambazaji wa maji, wakitoa kipaumbele kwa nyumba zilizoathiriwa zaidi na kuratibu ufikiaji ili kupunguza mvutano. Kilichoongoza mfumo huu hakikuwa data rasmi, bali maarifa ya msingiyaliyoshikiliwa na jamii. Wanawake walipata uelewa wa kina wa mahitaji ya kila nyumba: nani alikuwa na wategemezi zaidi, nani alikuwa akitunza watoto, wazee, au watu wenye ulemavu, na nani ambaye alikuwa na ufikiaji mdogo wa vyanzo mbadala vya maji. Walifuatilia hali ya uhaba wa maji kupitia kwa uchunguzi wa kila siku, ikijumuisha ni maeneo gani maji yaliisha haraka sana, maeneo ambapo mivutano ilikuwa ikiongezeka, na ni familia zipi zilikuwa zikiachwa nje. Mazungumzo ndani ya jamii - kusikiliza, kukagua, na kujenga maelewano - yalifanya kazi kama njia ya uthibitishaji wa data ya pamoja iliyokusanywa. Kuaminiana, ukaribu na uwajibikaji vilichangia katika kufanya maamuzi, hali iliyowaruhusu kutoa kipaumbele kwa waliathirika zaidi na kuratibu usambazaji kwa njia ambazo zilipunguza migogoro na kuhakikisha ufikiaji wa usawa zaidi.

Hakukuwa na mifumo ya nje inayoongoza hili, wala dashibodi zozote za data za kunasa jambo hili, na bado ilifanya kazi. Na hapa ndipo shida ilipo. Uzoefu huu, suluhisho hizi, maarifa haya mara nyingi hubakia kutoonekana katika mifumo inayoelekeza mwitikio wa usaidizi wa kibinadamu. Data hukusanywa, lakini mara nyingi data hii haikusanywi na wale wanaoishi katika uhalisia wa data hiyo. Vipaumbele hufafanuliwa huko nje. Uchambuzi hufanyika mbali na jamii zinazowakilishwa. Watu waliohama makazi yao huwekwa pamoja, tofauti zao hupuuzwa, na uhalisia wa maisha yao hurahisishwa.

## Hitimisho

Tajriba ya wanawake waliohamishwa kutoka makwao, inayoathiriwa na jinsia, uhamisho, ulemavu, umri na majukumu ya kijamii, huunda picha kamili. Wanawake wakimbizi huko Garissa hawakabiliani tu na mabadiliko ya tabianchi; wanaitikia, wanafanya mabadiliko na kuongoza. Hata hivyo, mara nyingi wafanya maamuzi hawawajumuishi. Haki ya tabianchi inahitaji usawa, ufikiaji, ujumuishaji na utambuzi, lakini ufadhili mdogo, uhamaji, na mafunzo hukwamisha maendeleo. Mradi huu unawawezesha wanawake kuongoza mijadala na mazungumzo, kukusanya data, kuchambua na kutetea, na kugeuza data kuwa rasilimali ya jamii. Wanawake wakimbizi wanakabiliwa na hatari kubwa zaidi, lakini maarifa yao yanakosekana kwenye data na maamuzi. Kente Threads inalenga kubadilisha hili kwa kusikiliza, kutambua uzoefu tofauti, na kuujumuisha katika data ya jamii kwa ajili ya uundaji wa sera. Mabadiliko yanahusu kuanza, kuthamini maarifa kwa njia tofauti, na kuangazia sauti mpya, kuanzia kwa wanawake tunaowahudumia. Lazima ulimwengu uone na ufuate muundo wao.

**Anila Noor** ni kiongozi mwenye maono na mtetezi wa haki za wanawake katika Shirika la New Women Connectors

**Madina Yunis** ni Mratibu wa Jinsia na Afya katika Pastoralist Girls Initiative.

# Kuzisaidia jamii badala ya kuzibadilisha: mabadiliko katika mwitikio unaoongozwa na jamii nchini Syria

## Sara Bahsass

Katika migogoro mingi duniani kote, jamii za ndani huonyesha uwezo wa ajabu wa kujipanga na kukabiliana na changamoto, hata kukiwa na huduma dhaifu za umma na rasilimali chache. Wakati wa shida, mitandao ya mshikamano na umoja wa kijamii mara nyingi huwa katika mstari wa mbele kushughulikia mahitaji ya kila siku, iwe ni kupitia kusaidia familia zilizotengwa zaidi au kuandaa juhudi za pamoja za kuboresha hali ya maisha ya ndani.

Uhalisia huu umewafanya wahudumu wa usaidizi wa kibinadamu kufikiria upya kuhusu muundo wa mwitikio wa masuala ya usaidizi wa kibinadamu. Badala ya kuangazia tu programu zilizopangwa na kutekelezwa na mashirika, umakini mkubwa umegeuka kuangazia mwitikio wa usaidizi wa kibinadamu uliojengwa kutokana na mipango na uwezo ambao tayari upo ndani ya jamii zilizoathiriwa na majanga au migogoro. Miongoni mwa mikabala hii, mbinu ya mwitikio unaoongozwa na jamii (CLR) inajitokeza: mbinu hii natokana na msingi wa kuunga mkono uwezo wa jamii kutambua vipaumbele vyao na kupanga mwitikio na suluhisho zao za pamoja kwa changamoto zinazowakabili.

Katika muktadha wa Syria, mbinu hii imeendelea kupata umuhimu unaoongezeka katika miaka mingi ya migogoro, ambayo imeathiri pakubwa hali za kiuchumi, kijamii na huduma katika maeneo mbalimbali. Zikikabiliwa na shinikizo zinazoongezeka, jamii zenyewe zilianza kuzalisha mipango ya kushughulikia changamoto mbalimbali zinazoathiri maisha yao ya kila siku. Juhudi hizi zikawa mwanzo muhimu wa kuendeleza mazoea ya usaidizi wa kibinadamu ambayo yanaimarisha hatua za jamii na kuunga mkono jukumu lake katika kukabiliana na shida.

## Mipango ya kijamii kama sehemu ya kuanzia yenye matumaini

Katika maeneo mengi ya Syria, mipango inayoongozwa na wakazi imeibuka ili kushughulikia masuala yanayoathiri hali halisi za ndani ya jamii. Katika baadhi ya vitongoji, wakazi hupanga kampeni za kusafisha makazi au juhudi za kukarabati maeneo ya umma yanayoharibika. Katika maeneo mengine, mipango inachukua muundo wa kusaidia familia zilizotengwa zaidi au kukabiliana na changamoto za mazingira zinazotishia riziki, kama vile mioto ya misimu inayohatarisha ardhi ya kilimo au maliasili.

Mipango hii inaakisi moyo wa kujitolea uliokita mizizi ya mshikamano wa kijamii ndani ya jamii za eneo husika. Mara nyingi, mipango hii hutokea moja kwa moja kutoka ndani ya jamii yenyewe, kutokana na hisia ya pamoja ya uwajibikaji miongoni mwa wakazi kwa mazingira yao na wao kwa wao. Tatizo linapotokea, watu huanza kulijadili wanapokutana kila siku na majirani au ndani ya mitandao yao ya kijamii, wakipendekeza michango ya kuboresha na kutatua tatizo hilo. Baada ya muda, mazungumzo haya yanatafsiriwa na kuwa hatua na vitendo halisi: wakazi huanza kujipanga, kusambaza majukumu na kuunganisha rasilimali zinazopatikana ndani ya eneo lao ili kutekeleza mipango inayotatua na kushughulikia tatizo hilo.



**Kikundi cha kijamii kinakarabati na kuboresha bustani ya umma katika eneo la Hama, kwa usaidizi kutoka kwa Survivor and Community -Led Crisis Response. Picha ni kwa hisani ya: cha Asasi za Kiraia na Demokrasis (CCSD)**

Moyo wa ushrikiano wa kijamii umekuwa dhahiri hasa wakati wa majanga makubwa. Kwa mfano, tetemeko kubwa la ardhi lilipopiga maeneo ya Kaskazini mwa Syria katika mwaka wa 2023, wakazi wengi walikusanyika mara moja ili kushiriki katika juhudi za utafutaji na uokoaji, kuwahamisha waliojeruhiwa na kusaidia familia zilizoathirika. Katika hali nyingi, timu za kujitolea ziliundwa kutoka kwa jamii hiyo hiyo, huku majirani na marafiki wakifanya kazi pamoja ili kupanga juhudi za uokoaji na kutoa usaidizi kwa familia ambazo zimepoteza makao au wapendwa wao. Miitikio hii haikuwa matokeo ya mipango ya awali au uingiliaji kati uliopangwa; badala yake, ilikuwa maonyesho ya moja kwa moja ya umoja wa jamii, msukumo unaowasukuma watu kusaidiana.

Moyo huo huo inajidhihirisha katika kukabiliana na mioto ya misimu inayoathiri baadhi ya maeneo ya kilimo na misitu ya Syria. Mioto inapozuka na kutishia mimea na misitu, wakazi na wakulima hushirikiana kwa pamoja ili kuzuia kuenea kwa miali ya moto, kwa kutumia zana rahisi zilizopo na ujuzi wa ndani wa ardhi inayowazunguka. Hii yote ni katika juhudi za kulinda ardhi na mali ambazo hutumika kama riziki kwa familia nyingi.

Uzoefu huu unaonyesha kuwa umoja wa jamii nchini Syria si jambo linalofungamana na mipango inayoungwa mkono na mashirika pekee. Hii ni sehemu ya mazoea ya kijamii yaliyokita ndani ya jamii yenyewe. Mara nyingi, uingiliaji kati wa shirika huja baadaye ili kusaidia au kuendeleza juhudi hizi. Kwa hivyo, ni muhimu kuelewa mipango hii ya kijamii na kutambua jukumu lake la kuendeleza mbinu za usaidizi wa kibinadamu ambazo zinaunga mkono kwa dhati mwitikio unaoongozwa na jamii na kuimarisha uwezo wa jamii kukabiliana na changamoto.

## Kuunga mkono mipango inayoongozwa na jamii badala ya kuibadilisha

Kwa kuzingatia mipango hii ya ndani ya jamii, mashirika ya maeneo nchini Syria yameanza kuchunguza njia mpya za kuunga mkono hatua za kijamii badala ya kuchukua nafasi yake. Katika muktadha huu, jukumu la watendaji wa usaidizi wa kibinadamu hubadilika kutoka kutekeleza miradi moja kwa moja hadi kukuza michakato inayowezesha jamii kuendeleza mipango yao wenyewe. Hii kwa kawaida huanza kupitia mazungumzo na wanajamii wenyewe ili kuelewa changamoto na fursa zilizopo ili kuzishughulikia. Kupitia kwa mijadala na mazungumzo haya, wanajamii wanaweza kutambua vipaumbele vyao na kuendeleza mawazo kwa ajili ya mipango ya pamoja inayotoa mwitikio kwa mahitaji yao halisi. Kisha wanaweza kuendelea na kujipanga ili kutekeleza mipango hii, kwa kutumia rasilimali za ndani, juhudi za kujitolea, na mahusiano ya kijamii ambayo yanaunda msingi wa hatua za pamoja.

Kwa mfano, katika mojawapo ya makazi, vikao vya mazungumzo na majadiliano ya kijamii vilifichua kwamba wakazi wazee walikuwa wanahangaika kupata huduma za afya. Kama hatua ya kukabiliana na tatizo hilo, watu binafsi walichukua hatua ya kuunda kikundi ch akujitolea cha eneo hilo ili kuandaa ziara za nyumbani za mara kwa mara na kuratibu na maduka  ya eneo hilo ili kupata dawa muhimu, kwa kutumia mitandao ya kijamii iliyopokatika ujirani wake. Jukumu la shirika lilikuwa dogo na lilihusu kutoa usaidizi wa kiasi ili kununua baadhi ya vifaa, bila kuingilia kati usimamizi wa mpango huo. Hii ilisaidia kuhifadhi umiliki wa jamii na kuimarisha uendelevu wake.

Katika baadhi ya matukio, mashirika yanaweza kutoa usaidizi unaobadilika, unaosaidia kuimarisha juhudi za jamii na kusaidia kutekeleza mipango iliyobuniwa na wanajamii wenyewe. Hii inaweza kujumuisha ruzuku ndogo, nyenzo, au usaidizi mdogo wa kiufundi, huku shirika likihakikisha kwamba maamuzi ya msingi yanasalia mikononi mwa jamii. Hii ni muhimu ili kulinda mwendelezo wa mipango hii na kuhakikisha kwamba inaendelele kuzingatia kwa karibu mahitaji halisi ya watu.

Mashirika ya ndani yana jukumu muhimu katika kuwezesha mbinu hizi. Ukaribu wao na jamii na uelewa wa kina wa muktadha wa mahali hapo huyaruhusu mashirika kuwezesha mazungumzo kati ya wanajamii na kuhimiza maendeleo ya mipango. Katika mfumo huu, wawezeshaji hupanga vikao vya majadiliano ya jamii kwa utaratibu maalumu: wakianza na  mwaliko wa vikundi mbalimbali vya jamii (wanaume, wanawake, vijana na wazee), na kufuatiwa na mjadala wa wazi unaoruhusu kila mtu kueleza changamoto zilizopo. Kisha mazungumzo yanaongozwa kuelekea kwa kutambua vipaumbele vya pamoja, kuzalisha mawazo ya pamoja, na hatimaye kukubaliana kuhusu mpango unaowezekana, huku majukumu na wajibu yakifafanuliwa wazi. Kupitia kwa mchakato huu shirikishi, mipango ya vitendo halisi inafanyika ambayo inaakisi mahitaji ya jamii na kuimarisha uwezo wake wa kujipanga.

Juhudi hizi zinapoanza kutekelezwa, mashirika yanaweza kutoa usaidizi unaoweza kunyambuka, unaoimarisha utekelezaji bila kuchukua nafasi ya jukumu la jamii. Usaidizi huu unaimarisha juhudi zilizopo za kujitolea, iwe kupitia kazi ya kujitolea, ujuzi eneo hilo, au mitandao ya kijamii ambayo jamii hutegemea ili kuandaa mipango yao.

Kwa njia hii, mashirika hayachukui nafasi ya nguvu za jamii; badala yake, yanatekeleza jukumu la uwezeshaji linaloziimarisha jamii na kuongeza ufanisi wake. Hii inachangia mwitikio ambao ni endelevu zaidi na wenye msingi wa karibu zaidi katika muktadha wa eneo hilo.

## Jamii inayoibuka ya kuchukua hatua na mbinu mpya

Juhudi zinazoongozwa na jamii zilipopanuka kote nchini Syria, umuhimu wa kubadilishana uzoefu miongoni mwa wahudumu wa usaidizi wa kibinadamu ulizidi kudhihirika. Nafasi za mazungumzo zilianza kujitokeza, mazungumzo yaliyowaleta pamoja watendaji wa usaidizi wa kibinadamu kutoka mashirika tofauti ili kujadili na kubadilishana uzoefu wa vitendo halisi unaohusiana na kuunga mkono mikakati ya kijamii. Mikutano na warsha hizi za kitaalamu hutoa fursa za kutafakari kwa pamoja jinsi ya kuendeleza mazoea ya usaidizi wa kibinadamu yanayolingana na hali halisi ya eneo la Syria, kupata mafunzo tuliyojifunza kutokana na tajriba na uzoefu mbalimbali, na kuchunguza mbinu bora zaidi za kuunga mkono mipango ya jamii bila kudhoofisha uhuru wao au kudhoofisha umiliki wa jamii hiyo.

Katika muktadha huu, Kituo cha Asasi za Kiraia na Demokrsia kiliandaa warsha ya tafakuri huko mjini Damascus kuanzia tarehe 30 Septemba hadi 4 Oktoba 2025, warsha iliyolenga usaidizi wa pamoja na mbinu ya CLR. Warsha hiyo ilileta pamoja washiriki 30 kutoka mashirika 12, wote wakifanya kazi katika uwanja wa usaidizi wa kibinadamu, pamoja na mashirika ya eneo husika yanayofanya kazi moja kwa moja na jamii katika sehemu tofauti za Syria. Warsha ilifanyika kufuatia kipindi cha majaribio ambacho kiliruhusu mashirika kuchunguza na kuunga mkono mipango iliyopo ya ndani.

Warsha iliongozwa na waelekezi wa Syria na wa kimataifa, ambao walishiriki uzoefu wao wa kutumia mbinu hii katika miktadha mbalimbali na kujadili kanuni zake za msingi. Hii ni pamoja na kuimarisha umiliki wa jamii wa mchakato, kujenga uaminifu, kudumisha mabadiliko katika njia za kutoa mwitikio kwa masuala, na kutegemea rasilimali za ndani ya eneo. Zana za vitendo halisi vya kuunga mkono mipango ya jamii pia zilikaguliwa upya, zikijumuisha vikao vya majadiliano na mazungumzo ya jamii vilivyopangwa, zana za kuweka vipaumbele shirikishi, miundo ya ruzuku ndogo, na mifumo iliyorahisishwa ya ufuatiliaji wa jamii ambayo inaruhusu jamii kutathmini maendeleo ya mipango yao bila kusimamiwa.

Miongoni mwa maeneo muhimu ya warsha hiyo ni pamoja na: kwanza, jinsi ya kutambua mipango iliyopo tayari bila kuivuruga, na badala yake kuendeleza kazi yao kupitia tathmini na uchanganuzi wa wa nyanjani wa moja kwa moja, ; pili, kufikiria jinsi ya kuongeza matokeo kwa kutoa mafunzo yaliyoombwa, kukuza uhusiano, au kutoa usaidizi wa nyenzo ili kuunga mkono kile ambacho tayari mpango huo unacho; na tatu, kuendeleza mbinu ya CLR ili iwe kielelezo cha marejeleo kwa sekta za usaidizi wa kibinadamu, maendeleo na ujenzi wa amani.

Warsha hiyo iliwapa washiriki fursa ya kushiriki uzoefu wao wa nyanjani wa kufanya kazi na jamii wenyeji nchini Syria, kujadili mifano ambapo mipango iliibuka kutoka ndani ya jamii zenyewe, na kutafakari kuhusu jukumu la jinsi mashirika yanaweza kuchukua nafasi katika kuunga mkono mipango hii bila kudhoofisha umiliki wa jamii. Mjadala huo pia uligusia changamoto za utekelezaji wa mipango, ikiwa ni pamoja na vikwazo vya kitaasisi na ufadhili ambavyo vinapunguza uwezo wa mashirika kuunga mkono mipango midogo midogo, inayoibuka.

Kutokana na  ushirikiano huu unaoendelea, jamii ya waeledi inajitokeza katika muktadha wa Syria, ikifanya kazi kuendeleza na kuimarisha utekelezaji aa mbinu ya CLR. Hii inaonyesha mabadiliko makubwa katika jinsi hatua za uingiliaji kati zinavyoundwa na kutekelezwa. Hazikomei tu katika kuitikia kwa mahitaji ya haraka lakini zina mwelekeo zaidi wa kuunga mkono jukumu la jamii kama mhusika mkuu katika kutambua vipaumbele na suluhisho zinazoongoza utatuzi. Mwelekeo huu unafungua nafasi kwa mifumo inayobadilika zaidi na endelevu, inayotegemea ubadilishanaji wa uzoefu, ujuzi na maarifa, na hivyo kuunganisha na kupanua mbinu hii ndani ya muktadha wa Syria.

Kazi ya kikundi inaendelea katika mwaka wote wa 2026 kwa lengo la kupanua utafutaji wa mipango iliyopo ya kijamii, kutafuta njia bunifu za kuiunga mkono, kutathmini na kuboresha mifumo ya kazi nchini Syria, na kushiriki masomo yaliyopatikana na vikundi vya asasi za kiraia na watu wenye ushawishi.

Kwa mfano, tajriba ya SEEN, mradi uliozinduliwa na Action for Humanity, unaonyesha mfano wa utangulizi wa vitendo vya kuwezesha jamii husika. Utekelezaji halisi wa mradi ulianza mjini Idlib mwaka wa 2024, kabla ya kupanuka hatua kwa hatua ili kufikia maeneo kadhaa kutokana na nguvu ya mafanikio yake yaliyopatikana na mahitaji yanayoongezeka ya mbinu hii. Mipango iliyokuwa chini ya SEEN ilijumuisha uingiliaji kati wa moja kwa moja wa miundombinu (ukarabati wa barabara, taa, usafi wa mazingira), huduma za elimu na afya, pamoja na mipango ya kimazingira na kiuchumi, ili kufikia athari inayoonekana katika maisha ya watu. Mradi umejiendeleza tangu 2024 kupitia utegemezi wake wa uhamishaji maarifa na kujenga uwezo kwa wawezeshaji wa ndani na timu za kujitolea, kuwezesha jamii kusimamia na kukuza

mipango kwa uhuru kupitia matengenezo, upanuzi na urudufu katika maeneo mengine. Mbinu hii pia ilisaidia kuanzisha modeli inayoweza kupanuka, ambayo ilienea zaidi ya utekelezaji ili kukuza utamaduni wa utendaji wa jamii na kuunganisha jukumu la watu binafsi kama waanzilishi na mawakala wa mabadiliko. Mambo haya yote yalichangia uendelevu wa mradi, yakibadilisha uingiliaji kati kutoka kwa majibu ya muda hadi njia za maendeleo za muda mrefu.

## Changamoto na fursa kwa siku zijazo

Matumizi ya mbinu iliyoelezwa hapo juu katika muktadha changamano kama vile Syria huleta changamoto kadhaa. Kwa upande mmoja, mashirika yanakabiliwa na matatizo yanayotokana na mifumo ya ufadhili ambayo ina mwelekeo wa kupendelea miradi iliyopangwa mapema yenye matokeo yaliyopangwa mapema, ambapo mipango inayoongozwa na jamii inahitaji kubadilika zaidi katika hatua za kuitambua, kuiunga mkono na kuiendeleza. Kwa upande mwingine, baadhi ya taratibu za kiutawala na kitaasisi mara kwa mara huzuia uwezo wa mashirika kuunga mkono mipango midogo midogo au inayoendelea haraka inayotokea ndani ya jamii.

Kwa kuongeza, wafanyakazi wa usaidizi wa kibinadamu wanahitaji kukuza ujuzi mpya na mbinu za kufanya kazi zinazofaa kwa mipango inayoongozwa na jamii. Mbinu hii inahitaji kuhama kutoka kwa utekelezaji wa mradi na kuelekea katika uwezeshaji wa mipango ya jamii yenyewe. Kujenga uaminifu na mahusiano na jamii wenyeji pia kunahitaji muda na juhudi endelevu, changamoto katika mazingira ya usaidizi wa kibinadamu yenye sifa ya mabadiliko ya haraka na shinikizo kubwa ya uendeshaji shughuli.

Hata hivyo, licha ya hayo yote hapo juu, uzoefu uliokusanywa nchini Syria unaonyesha kwamba kuunga mkono mipango ya jamii kunachangia katika kuendeleza suluhisho za usaidizi wa kibinadamu ambazo zinaunganishwa kwa karibu zaidi na hali halisi eneo husika. Inaonekana wazi zaidi kuwa mipango inayotokana na jamii huwa inaakisi uelewa wa kina wa changamoto zinazowakabili wakazi wa jamii. Wanapoungwa mkono kwa njia zinazohifadhi umiliki wa jamii, wanajamii wanaweza kuimarisha uwezo wa jamii kushughulikia changamoto kwa urahisi na kuendeleza suluhisho endelevu zaidi za maeneo husika ya ndani. Hii inajidhihirisha katika vitendo kupitia uwezo unaokua wa jamii kujipanga, kutambua kwa pamoja vipaumbele, kusimamia rasilimali zilizopo kwa ufanisi zaidi, na katika mwendelezo na maendeleo zaidi ya baadhi ya hatua za uingiliaji kati hata baada ya usaidizi kutoka nje kukamilika.

**Sara Bahsass** ni mtaalamu wa masuala ya kibinadamu na maendeleo nchini Syria. Kazi yake inaangazia upangaji programu wa sekta mtambuka, uratibu, ushirikishaji wa wadau, na mbinu shirikishi.

# Kutoka kwa 'walioathiriwa na mgogoro' hadi viongozi: jinsi wakimbizi wa syria walivyoongoza mwitikio wa kibinadamu usio na kifani nchini Uturuki

Areej Al-Mohammad

Wakimbizi wa Syria walianza kuingia nchini Uturuki mwanzoni mwa mwaka 2012, mara tu baada ya kuzuka kwa mapinduzi ya Syria. Idadi ya watu waliokimbia makazi yao iliongezeka hatua kwa hatua jinsi mzozo ulivyoendelea kuenea na mashambulizi ya kijeshi dhidi ya miji na vijiji vya Syria yakiongezeka. Kufikia mwaka 2016, Uturuki ilikuwa imekuwa nchi inayohifadhi wakimbizi wengi zaidi duniani, ikiwa na takriban wakimbizi wa Syria milioni 2.7 waliosajiliwa. Miongoni mwa sababu kuu zilizochochea ongezeko kubwa la watu waliolazimika kuyakimbia makazi yao katika kipindi hicho ni kuongezeka kwa kampeni za kijeshi zilizofanywa dhidi ya miji na maeneo mbalimbali na vikosi vya utawala wa zamani pamoja na washirika wake, pamoja na kutekwa kwa maeneo makubwa ya Syria na kundi la dola la Kiislamu (Hususan majimbo matatu ya mashariki ya Deir ez-Zur, Raqqa na Hasakah, pamoja na sehemu za majimbo ya Aleppo, Homs na Idlib).

Mtitririko waa wakimbizi wa Syria waliokuwa wakikimbilia nchini Uturuki uliendelea na haukupungua hadi muda mfupi kabla ya kuanguka kwa utawala wa Assad mwishoni wa mwaka 2024.

Idadi kubwa ya wakimbizi wa Syria ilifanya makazi yake katika majimbo ya kusini mwa Uturuki wilaya ya Urfa, Gaziantep na Kilis. Idadi kubwa ya wakimbizi hao ilikuwa imetoka katika majimbo ya Raqqa, Deir ez-Zur, Hasakah na Aleppo.

Sababu kadhaa zinaeleza mkusanyiko huu wa kijiografia. Majimbo haya yapo karibu sana na mpaka wa Syria, jambo lililoyafanya kuwa lango la kwanza la kuingilia. Wakimbizi wengi pia walikuwa na mahusiano ya kijamii yaliyokuwepo awali na jamii za wenyeji wa uturuki wenye asili ya Kiarabu. Na pengine sababu yenye ushawishi mkubwa zaidi ni kwamba wengi wao walikuwa wakifuata wanafamilia na ndugu zao ambao tayari walikuwa wamehamia na kuishi katika maeneo hayo kabla yao.

Makala hii inafuatilia jinsi mipango ya wakimbizi wa Syria nchini Uturuki ilibadilika na ilivyokua kadri muda ulivyopita na kuchunguza namna ilivyojitokeza kama juhudi za kutoa msaada wa kiraia na kibinadamu. Inaendelea kuchambua uingiliaji kati uliotekelezwa na kuangazia namna maarifa na utaalamu uliopatikana ulivyotumiwa kuimarisha uzoefu, kuhakikisha mwendelezo na kuweka msingi wa uendelevu wa muda mrefu.

## Kutoka kwa 'wanufaika' hadi kwa viongozi

Mwanzoni, wakimbizi wa Syria nchini Uturuki walikuwa wapokeaji wa moja kwa moja wa msaada na huduma zilizotolewa na mashirika ya kimataifa na ya Uturuki, pamoja na baadhi ya mipango iliyoanzishwa na jamii zilizowapokea. Kulikuwa na nafasi chache sana, kama zilikuwepo kabisa, zilizokuwa na maana au zilizotengewa wakimbizi kushiriki katika kuongoza au hata kushiriki katika shughuli za mwitikio wa kibinadamu. Hata hivyo, hali hii ilibadilika kwa haraka. Kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2013 na kuendelea, mwongo uliofuata ulishuhudia mabadiliko makubwa yaliyojengeka hatua kwa hatua: ambapo wakimbizi walianza kuchukua nafasi kubwa zaidi katika kuongoza na kutekeleza shughuli za mwitikio, huku wakijengana katika juhudi zao.

Hii ilianza kupitia mipango ya ngazi za chini iliyoanzishwa na vikundi vya kujitolea vilivyolenga kuwapatia wakimbizi mahitaji ya msingi kama vile vitu vya kutumia nyumbani, vyakula vya msingi, mavazi ya majira ya baridi, blanketi, vifaa vya kupasha joto na vifaa vya kutumia shuleni. Vitu hivi vilipatikana kwa kutumia mikakati tofauti, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa michango kutoka kwa wakimbizi wenyewe,[3] kuwasiliana na jamii za Wasyria wanaoishi nje ya nchi hususan katika nchi za Ghuba na Ulaya[4] au kufanya kazi na mashirika pamoja na taasisi za serikali na asasi za kiraia ili kupata na kuifikisha misaada kwaa walengwa.

Sambamba na juhudi hizi, kulitokea mabadiliko muhimu yaliyoashiria kuibuka kwa asasi za kiraia za Syria kama taasisi zenye mifumo rasmi na msingi imara wa kiutendaji. Asasi hizi zilikuja na dira na mbinu wazi za utekelezaji wa kazi za kibinadamu, zikijumuisha majukumu, mifumo na malengo yaliyoelezwa kwa uwazi, na wafanyakazi wake wengi waliokuwa raia wa Syria.

Vikundi vya kujitolea, hususan wanawake na vijana, vilikuwa miongoni mwa makundi ya kwanza ya kijamii ambayo asasi hizi zililenga kushirikisha katika shughuli zake. Viliwapatia msaada wa kiufundi na kiutawala na kuwafungulia fursa za ufadhili, ruzuku, mitandao ya ushirikiano, mafunzo na uimarishaji wa uwezo.

Kipindi hiki kilijithibitisha kuwa hatua muhimu ya mabadiliko na chenye manufaa kwa pande zote mbili. Asasi za kiraia zilipata fursa ya kushirikiana na timu za kujitolea pamoja na mitandao ya kijamii kama washirika wa utekelezaji, jambo lililozisaidia kuendeleza miradi, kuimarisha nafasi za kiraia na kupanua ushiriki wa jamii. Vikundi na timu za kujitolea, kwa upande wao, zilipata manufaa mbalimbali. Walifahamishwa kuhusu dhana na utekelezaji wa kazi za kiraia. Walipata mifumo, mpangilio na uwezo. Walishiriki katika shughuli, mafunzo na warsha.[5] Na pengine jambo muhimu zaidi, kipindi hiki kilichochea kuibuka kwa mahusiano mapya na ushirikiano kati ya wakimbizi waliowasili kutoka majimbo mbalimbali ya Syria, na hivyo kugeuza uhamishwaji kutoka kwa makazi kuwa msingi wa hatua za pamoja.

Ushirikiano huu kati ya pande hizo mbili ulisaidia kuvunja dhana potofu zilizokuwa zikishikiliwa na baadhi ya wakimbizi kuhusu wenzao. Uliimarisha mahusiano ya kijamii na kuimarisha mwelekeo wa kibinadamu na wa kitaifa katika mijadala ya umma, huku ukiweka kwa uthabiti mfumo unaozingatia maadili na haki za binadamu kama msingi elekezi wa shughuli na uingiliaji kati wote. Kutokana na hali hiyo, kati ya mwaka 2014 na 2024, Urfa ilishuhudia kuibuka kwa mazingira yenye nguvu ya ushiriki wa kiraia, shughuli za kijamii na hatua za pamoja za wananchi.

Matokeo yake yalikuwa yenye manufaa makubwa na yenye kutoa funzo muhimu. Timu nyingi za kujitolea ziliweza kutumia fursa hizi muhimu na kujigeuza kuwa asasi za kiraia zilizosajiliwa rasmi na zinazofanya kazi kikamilifu, zikiwa na uwezo wa kupata ufadhili, msaada na rasilimali mbalimbali. Mifano ni pamoja na Homecountry's Flowers, Women of Tomorrow na Euphrates, miongoni mwa nyinginezo.[6]

---

3 Kundi la wanawake wa Syria katika mji wa Şanlıurfa lilianzisha kampeni iliyoitwa "Fungua Kabati Lako", kwa lengo la kukusanya mavazi ya majira ya baridi na kuyagawa kwa wakimbizi waliokuwa na uhitaji.

4 Vifaa vya kupasha joto na vikapu maalumu vya vyakula vya Ramadhani vilipatikana kupitia msaada wa wafadhili wa Syria; mpango huu umeendelea kutekelezwa kila mwaka wakati wa mwezi wa Ramadhani hadi leo.

5 Hii ilijumuisha mafunzo kuhusu uhamasishaji, utetezi, uwezeshaji, uundaji wa vyombo vya kiraia, usimamizi wa nafasi za kazi za kiraia, ujenzi wa mitandao, uandaaji wa sera na ugawaji wa majukumu, pamoja na maeneo mengine mbalimbali.

6 Hii ndio tafsiri ya majina yao rasmi ya Kiarabu, (ورد البلد) ,(نساء الغد) na (الفرات).

Katika mazungumzo nasi, Amal al-Hajj, mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Al-Furat, asasi inayofanya kazi katika mji wa Urfa nchini Uturuki, alieleza nafasi iliyotekelezwa na Kituo cha Asasi za Kiraia na Demokrasia (CCSD) katika kusaidia timu yake ya kujitolea kubadilika na kuwa asasi ya kiraia iliyosajiliwa rasmi. Amal anasema:

'Kabla ya kupata usajili rasmi, Kituo hicho kilichukua nafasi muhimu katika kuiunga mkono timu ya El-Furat kupitia shughuli za kujenga uwezo na mafunzo kuhusu ujuzi wa uwezeshaji na usimamizi wa vikao vya jamii. Msaada huu ulisaidia kuimarisha utayari wa timu kutekeleza shughuli za nyanjani kwa weledi, kuongeza imani ya wanachama kwa uwezo wao wenyewe na uwezo wao wa kuongoza mipango mbalimbali, pamoja na kuboresha ubora wa shughuli zilizotekelezwa. Timu yetu iliweza kutekeleza uingiliaji kati wenye ufanisi na kujibu mahitaji ya jamii yetu kwa namna yenye matokeo makubwa zaidi.'

Baada ya Furat kupata usajili rasmi, ushirikiano wake na CCSD ulipanuka na kujumuisha msaada wa kina wa kuimarisha taasisi. Amal anasema:

> 'Kituo hicho kilitupatia msaada wa kiufundi uliokuwa muhimu katika kuandaa mikakati yetu na kubainisha mwelekeo wetu wa muda mrefu. Kilichangia pia katika kuimarisha sera na taratibu zetu za ndani ili kuimarisha utawala bora na mifumo ya kazi iliyoandaliwa kwa utaratibu na kilitupatia ushauri wa kitaasisi uliotusaidia kujenga mfumo wa usimamizi ulio wazi na wenye ufanisi.

## Nafasi ya ushirikiano

Pamoja na mipango ya jamii za wenyeji, uzoefu wa nafasi ya ushirikiano' uliibuka kama mfano wa mpango ulioongozwa na wanawake, ulianzia nchini Uturuki kabla ya kupanuka na kuwajumuisha wanawake kutoka nchini Syria na maeneo mengine. Mpango huu umejengwa juu ya uratibu na kubadilishana uzoefu miongoni mwa wanawake na unalenga kuunga mkono juhudi zinazoongozwa na jamii, iwe kuna ufadhili wa nje au la. Mtazamo huu umeupa kiwango kikubwa cha unyumbufu na uwezo wa kudumu.

Wakati wa mwitikio wa tetemeko la ardhi la mwaka wa 2023, muungano huu ulitoa mchango muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa shughuli za usaidizi wa kisaikolojia kwa wanawake walioathiriwa na janga hilo, lilkunganisha mipango ya ndani ya jamii na kuwezesha ubadilishanaji wa uzoefu na utaalamu miongoni mwa wanawake walioshiriki kikamilifu. Leo, unaendelea kutetea maslahi ya wanawake wakimbizi wa Syria kwa kuangazia changamoto wanazokabiliana nazo na kuhimiza kuwepo kwa mwitikio unaowajumuisha zaidi.

Uzoefu huu unaakisi mabadiliko muhimu. Majukumu ya wanawake hayajabaki tena katika kushiriki tu shughuli za mwitikio wa kibinadamu - sasa waongoza shughuli hizo na kushiriki katika kuamua vipaumbele vyake, ndani ya mfumo wenye unyumbufu unaovuka mipaka ya kawaida ya kazi za kibinadamu. Ushirikiano huu pia umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha msingi wa kitaasisi wa asasi ya El Furat, kuiinua hadi kufikia kiwango cha juu zaidi cha weledi. Hali hii imekuwa na athari chanya katika ubora wa programu zake na uwezo wake wa kufanya kazi kwa ufanisi pamoja na wafadhili na washirika.

## Mtihani Mgumu: Tetemeko la ardhi la mwaka wa 2023

Kupitia ushiriki wao katika shughuli za kiraia ndani ya mashirika, vikundi vya kazi na mitandao ya kijamii, wakimbizi wa Syria walikuwa wamejibadilika kutoka kuwa wapokeaji wa misaada pekee hadi kuwa 'wadau' wenye uwezo wa kuchukua hatua kwa haraka na kujibu mahitaji yanayojitokeza, wakiwa na uwezo wa kuongoza na kushiriki katika uingiliaji kati mbalimbali wakati wa migogoro. Pengine mifano yenye nguvu zaidi inayothibitisha hoja hii ni kile kilichotokea tarehe 6 Februari mwaka wa 2023, wakati tetemeko kubwa la ardhi lilipoikumba \uturuki pamoja na maeneo ya kaskazini na magharibi mwa Syria.

Chini ya saa 12 baada ya tetemeko la ardhi kutokea, kundi la wakimbizi lilibadilisha moja ya mikahawa mikubwa inayomilikiwa na Wasyria mjini Urfa kuwa makazi ya muda kwa familia zilizohamishwa na janga hilo. Katika kipindi cha mwezi mzima, waliweza kupata vifaa vya kupasha joto na mahitaji muhimu ya chakula kwa zaidi ya familia 40 kupitia ukusanyaji wa michango ya watu binafsi na uhamasishaji wa msaada kutoka kwa jamii za Wasyria wanaoishi ughaibuni. Sambamba na hilo, vikundi vya mawasiliano na uratibu viliundwa katika vitongoji na wilaya mbalimbali ili kuwasaidia walioathiriwa na kuhakikisha wanahamishiwa hadi maeneo salama.

Kwa mfano, wamiliki wa magari waliweka magari yao kwa matumizi ya jamii, wakiwasafirisha wakazi walioathiriwa ndani ya mji wa Urfa na maeneo mengine bila malipo yoyote. Katika maeneo salama zaidi, utamaduni wa kushirikiana makazi uliibuka, ambapo familia kadhaa zilizoathiriwa zilikaa pamoja kwenye nyumba moja, hasa katika wiki muhimu zaidi ya kwanza  baada ya janga hilo. Wakati huo huo, vijana waliokuwa na ujuzi wa lugha ya Kituruki walijitolea kusaidia familia zilizoathiriwa zilizotaka kusafiri nje ya Urfa, kwa kuwasaidia kukamilisha taratibu za kuweka nafasi za safari za ndege na kutoa huduma za ukalimani katika uwanja wa ndege.

Katika upande wa asasi za kiraia, walielekeza upya miradi na rasilimali zao zote za ufadhili katika kusaidia jamii zilizoathiriwa na tetemeko la ardhi kupitia mipango na shughuli za ushirikiano. CCSD, kwa kushirikiana na washirika wake, iliunga mkono mipango ya kuandaa na kusambaza vikapu vya chakula, blanketi, vifaa vya afya na vifaa vya kuandikia. Iliandaa pia shughuli za usaidizi wa kisaikolojia kwa makundi mbalimbali ya jamii, hususan wanawake na watoto.

Matukio ya tetemeko la ardhi yalionyesha kwa uwazi uwezo na ustahimilivu wa mitandao ya uingiliaji kati ya kijamii katika kukabiliana na majanga. Usaidizi wao ulijitofautisha na uingiliaji kati wa kawaida zilizotekelezwa na mashirika ya kimataifa na taasisi rasmi. Tofauti hii ilitokana na nguzo mbili za mitandao hii. Kwanza, wana uelewa wa kina zaidi kuhusu muktadha wa Syria na mazingira yake ya kijamii. Pili, wana uwezo wa kuwafikia watu walioathiriwa kwa urahisi na kwa usalama, kutokana na mahusiano ya kijamii yaliyojengwa kwa muda mrefu ambayo yameunda misingi imara ya kuaminiana kati ya watoa huduma na watu wanaowahudumia.

Katika nyakati za majanga makubwa, mitandao ya kijamii inawakilisha fursa muhimu ya kufanikisha mwitikio wa kibinadamu wa haraka na wenye ufanisi. Mitandao hii hutegemea maarifa, mahusiano na uzoefu uliokita mizizi ndani ya jamii kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine uwezo madhubuti wa kitaasisi katika masuala ya malengo, na mbinu za kazi. Hata hivyo, taswira hii chanya haiondoi uwepo wa changamoto halisi. Asasi na vikundi vya kazi hushindania ufadhili. Wakati mwingine, uratibu kuhusu mahali na wakati wa uingiliaji kati hukosekana. Masuala haya yanahitaji mbinu mpya za ushirikiano na mipango bora zaidi ya uratibu wa pamoja.



**Timu ya wasaidizi wa kujitolea ya Syria ikikidhi mahitaji ya waathirika wa tetemeko la ardhi kusini mwa Uturuki (Kilis). Picha ni kwa hisani ya: Kituo cha Asasi za Kiraia na Demokrasia.**

## 2024: Wakati wa mabadiliko makubwa

Kuporomoka kwa utawala wa Assad nchini Syria mwishoni mwa mwaka 2024 kulipokelewa kwa shangwe. Wasyria walitamani kuona taifa ambalo lingehakikisha usalama na amani ya kudumu kwao wote. Hata hivyo, furaha hiyo ilianza kutoweka polepole kutokana na sababu kadhaa, zikiwemo makundi yenye silaha yaliyokuwa yakifanya shughuli zake bila kuwajibishwa, kuenea kwa matamshi ya chuki, mzozo mkubwa wa kiuchumi, pamoja na kutungwa kwa sheria zinazopuuza haki za binadamu na haki za wanawake. Hali hii ilisababisha kukata tamaa kwingi miongoni mwa wakimbizi wengi wa Syria nchini \uturuki na kuongeza kusitasita kwao kurejea nchini kwao, hasa wale waliotoka katika mikoa ya mashariki.

Aidha, mfululizo wa maamuzi na maendeleo mbalimbali ulikuwa tayari umefanya hali kuwa ngumu zaidi kwa familia zilizotaka na zilizokuwa na uwezo wa kuendelea kubaki. Hali hii ilizidishwa zaidi na kupungua kwa kiwango kikubwa kwa ufadhili na msaada uliokuwa ukielekezwa kwa wakimbizi wa Syria, asasi za kiraia na mashirika ya kibinadamu. Kutokana na hali hiyo, sehemu kubwa sana ya Wasyria nchini \\\uturuki walipoteza njia zao za kupata riziki. Kutokana na hali hiyo, mitandao ya kijamii ilikumbwa na kupungua kwa kiwango kikubwa kwa uwezo wake wa kuingilia kati na kutoa msaada wakati wa majanga ya kibinadamu.

Mabadiliko haya yalizidisha zaidi changamoto ambazo mitandao ya jamii na asasi za kiraia zilikuwa zikikabiliana nazo kwa miaka mingi. Changamoto hizo ni zifuatazo:

1. Kizuizi cha lugha na changamoto za mawasiliano kati ya wakimbizi, jamii mwenyeji na taasisi rasmi zilidhoofisha uwezo wa kufanya tathmini sahihi za mahitaji na kupunguza ufanisi wa jumla wa mwitikio wa kibinadamu.

2. Mitazamo ya uhasama dhidi ya uwepo wa wakimbizi wa Syria nchini Uturuki, ambayo wakati mwingine iligeuka kuwa dhuluma za kisiasa za makusudi iliambatana na ukosefu wa hoja mbadala yenye nguvu.
3. Vikwazo vya kisheria na kiutaratibu vinavyohusiana na usajili wa wakimbizi. Wengi wao walikuwa na kadi za ulinzi wa muda ambazo ziliwazuia kusafiri kati ya mikoa bila kupata idhini ya awali.

Kwa ujumla, changamoto hizi zilizuia kutumika kikamilifu utaalamu wa kiraia na kijamii wa Wasyria nchini Uturuki. Utaalamu huo ulikuwa na uwezo wa kutumika kama nyenzo muhimu ya kuongeza kwa kiwango kikubwa kwa ufanisi wa uingiliaji kati wa kibinadamu wakati wa majanga. Uwezo huo pia ungeweza kuvuka mipaka ya \uturuki na kutoa mfano unaofaa na unaotia moyo kwa kazi za kiraia ndani ya Syria yenyewe.

## Kuelekea kwa ushirikiano wa haki na usawa unaoongozwa na wakimbizi

Ni muhimu kuchunguza jinsi uzoefu wa mitandao ya kijamii ya wakimbizi wa Syria nchini Uturuki unavyoweza kuendelezwa na kudumishwa. Uzoefu huu ni matokeo ya zaidi ya mwongo mmoja wa uwekezaji katika juhudi na rasilimali. Umefanikiwa kujenga mazingira ya kiraia na kijamii yanayostahili kupewa uzito mkubwa na kuendelezwa zaidi. Kufanikisha uwezo huu kunahitaji mchakato shirikishi ambapo wadau wote wanachangia dira, mawazo na mapendekezo. Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo tunayowasilisha katika muktadha huu:

1. Ushirikiano na taasisi rasmi pamoja na asasi za kiraia za Uturuki unapaswa kuimarishwa zaidi. Lengo ni kubainisha, kwa mtazamo wa Uturuki, nguvu na udhaifu wa shughuli za mitandao ya kijamii ya Wasyria. Hili linahudumia malengo kadhaa: kujenga uaminifu wa pande hizo mbili, kubainisha malengo ya pamoja na kuyafuatilia kwa ushirikiano, kufuatilia mabadiliko katika sheria na taratibu rasmi za Uturuki ili kuhakikisha uwepo wa msingi wa kisheria kwa mipango na uingiliaji kati na kukuza ushirikiano na fursa za ufadhili kwa kushirikiana na wadau wa Uturuki.
2. Majadiliano maalumu na mikutano miongoni mwa mitandao ya kijamii ya Wasyria inapaswa kuandaliwa. Lengo lake ni kuweka kumbukumbu za athari za uzoefu huo na kuandaa mapendekezo ya ushirikiano ambayo yanaweza kuwasilishwa kwa mitandao ya asasi za kiraia za Uturuki.
3. Ni muhimu kuangazia juhudi zilizofanywa hadi sasa katika mikutano na wafadhili na kuwahimiza kuongeza na kuimarisha msaada wao kwa mitandao hii.
4. Mazingira ya Wasyria nchini Uturuki yanapaswa kutathminiwa upya kwa kuzingatia mabadiliko ya hivi karibuni ambayo yamebadilisha nafasi ya kiraia ya Wasyria. Lengo ni kuelewa asili na kiwango cha mahitaji ya sasa pamoja na nafasi zilizopo za kuingilia kati na kutoa msaada. Kwa lengo hilo, programu iliyopangwa vizuri ya warsha, mikutano na majadiliano maalumu inapaswa kuandaliwa ili kuzikutanisha asasi za kiraia za Wasyria na mitandao ya kijamii. Vikao hivi vinapaswa kuzalisha maelezo ya wazi kuhusu uzoefu huo, kuweka kumbukumbu za shuhuda za mafanikio, kubainisha changamoto zilizopo na kubainisha mafunzo yaliyopatikana. Matokeo ya mchakato huo yanapaswa kushirikishwa na taasisi rasmi za Syria na Uturuki pamoja na mashirika ya kimataifa, kwa lengo la kuandaa mkakati na mpango wa utekelezaji wa angalau miaka mitano.

Sisi, wakimbizi, hatukuondoka katika ardhi yetu kwa hiari. Hatukuweza kuzuia majanga, misiba na ukiukwaji wa haki uliotupata. Hata hivyo, tulipata nguvu ya kugeuza hali hii chungu kuwa jambo nzuri kwa binadamu. Kupitia kwa jambo hilo, tulipata maarifa, utaalamu na mafunzo ambayo leo tunatamani kuyahifadhi na kuyaendeleza. Lengo letu ni kuwa na jamii iliyojengwa juu ya misingi ya amani, kuishi pamoja, uraia wenye usawa na haki za binadamu.

**Areej Al-Mohammad** ni mwanaharakati wa asasi za kiraia anayeishi Şanlıurfa, kusini mwa Uturuki. Yeye ni mwanachama wa mpango wa Nafasi ya Ushirikiano

## Kutathmini athari za Mfuko wa Kimataifa wa Kutokuwa na Uraia katika upatikanaji wa rasilimali na mamlaka ya kufanya maamuzi kwa jamii zilizoathirika katika eneo la Asia-Pasifiki

Subin Mulmi

Ukosefu wa uraia unabakia kuwa changamoto kubwa ya haki za binadamu iliyoenea duniani kote. Ibara ya 15 ya Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu inathibitisha kwamba kila mtu ana haki ya kuwa na uraia, na kwamba hakuna mtu anayepaswa kunyang'anywa uraia wake kiholela. Hata hivyo, makadirio ya kihafidhina yanaonyesha kwamba angalau watu milioni 15 hawana uraia duniani, huku makumi ya mamilioni ya wengine wakiwa katika hatari ya kukosa uraia. Watu wasio na uraia mara nyingi hunyimwa haki na huduma za msingi kama vile elimu, huduma za afya, ajira, makazi na ushiriki wa kisiasa, hali inayowafanya kuwa miongoni mwa makundi yaliyotengwa zaidi duniani.

Ukanda wa Asia na Pasifiki ni makazi ya baadhi ya idadi kubwa zaidi ya watu walioathirika duniani, ikiwemo jamii kama vile Rohingya, Bajau Laut Malaysia, na jamii za makabila ya maeneo ya milimani nchini Thailand. Ukosefu wa uraia katika eneo hili mara nyingi hutokana na mifumo ya ubaguzi iliyokita mizizi, ikiwemo kutengwa kwa makundi ya makabila madogo, sheria za uraia zinazowabagua watu kwa misingi ya jinsia, na urithi wa mipaka ya kikoloni na urithi wa dola. Licha ya ukubwa na ugumu wa tatizo hili, juhudi za kimataifa za kushughulikia ukosefu wa uraia bado zinaendelea kukabiliwa na uhaba mkubwa wa rasilimali, huku mashirika mengi ya kiraia, hasa yale yanayoongozwa na jamii zilizoathirika, yakiendelea kufanya kazi kwa ufadhili na usaidizi mdogo wa kitaasisi.

Kutokana na hali hiyo, mashirika ya kijamii yanayotetea haki za jamii zisizo na uraia mara nyingi hutegemea ufadhili wa muda mfupi wa miradi au ruzuku ndogo kutoka kwa mashirika makubwa yasiyo ya kiserikali (NGOs), jambo linalopunguza uwezo wao wa kutekeleza mikakati ya muda mrefu au kutekeleza mahitaji ya jamii kwa unyumbufu. Wakati huo huo, kuna kuongezeka kwa utambuzi kwamba lazima juhudi za kushughulikia tatizo la kukoa uraia ziongozwe na jamii zenyewe zilizoathirika, kwa kuwa uzoefu wao wa maisha utatoa maarifa muhimu kuhusu suluhisho madhubuti. Kutokana na hali hii, mipango kama vile Mfuko wa Kimataifa wa Kukabiliana na Ukosefu wa Uraia (GSF) umeanzishwa ili kuelekeza ufadhili unaobadilika kulingana na mahitaji na wa miaka mingi moja kwa moja kwa wanaharakati wa wasiokuwa na

uraia na mashirika yanayoongozwa na watu walioathiriwa, huku ikikuza ushiriki wa wadau katika kufanya maamuzi. Makala hii inachunguza uzoefu wa awali wa mashirika yaliyopata usaidizi kupitia Mfuko huo katika eneo la Asia-Pasifiki, ikieleza jinsi mfumo huu unavyoathiri uwezo wa mashirika, juhudi za utetezi, na nafasi ya jamii zilizoathiriwa katika kuunda na kuelekeza hatua za kukabiliana na ukosefu wa uraia.

## Mfuko wa Kimataifa wa Kushughulikia Ukosefu wa Uraia: Muundo shirikishi wa kufadhili jamii zisizo na uraia


Licha ya kuwa inahusiana kwa karibu na changamoto nyingi kuu za kimataifa za wakati wetu, ikiwa ni pamoja na uhamiaji, ubaguzi, migogoro na utawala wa kidemokrasia, watu wasio na uraia na wale walioathiriwa na sheria za kibaguzi za uraia mara nyingi wameendelea kutengwa katika mijadala ya sera za kimataifa. Sauti zao mara nyingi hukosekana katika maeneo ya kufanya maamuzi au hujumuishwa kiishara tu, wakiwa na fursa chache za kushiriki katika kuunda mikakati inayokusudiwa kushughulikia dhuluma wanazokumbana nazo. Wakati huohuo, ukosefu wa uraia wenyewe kihistoria umekuwa suala ambalo halijapewa kipaumbele cha kutosha ndani ya sekta ya uhisani, mara nyingi likiangukia katikati ya vipaumbele vya wafadhili wanaojikita katika haki za binadamu, uhamiaji, wakimbizi, usawa wa kijinsia au maendeleo.

GSF ilianzishwa ili kujibu tatizo la muda mrefu kuhusu ufadhili mdogo wa utetezi wa watu wasio na uraia na kutengwa kwa jamii zilizoathirika katika mijadala ya sera za kimataifa. Ukiandaliwa kupitia mashauriano kati ya wanaharakati wa watu wasio na uraia, mashirika ya kiraia na wafadhili, Mfuko huu unalenga kushughulikia changamoto hizi kwa wakati mmoja kwa kuongeza rasilimali za utetezi katika ngazi ya jamii au mashinani huku ukibadilisha namna maamuzi ya kiufadhili yanavyofanywa. Mpango huu ni sehemu ya juhudi pana zaidi ndani ya Harakati za Kimataifa za Kupinga Ukosefu wa Uraia zinazolenga kuweka uongozi, maarifa na vipaumbele vya watu wasio na uraia wenyewe katika kitovu cha juhudi za kushughulikia tatizo la kutokuwa na uraia.

Mfuko wa GSF hutoa ufadhili nyumbufu, wa miaka mingi na usio na masharti maalumu kwa mashirika na wanaharakati wanaofanya kazi kushughulikia tatizo la ukosefu wa uraia na sheria za kibaguzi kuhusu uraia. Tofauti na mifumo ya jadi ya utoaji wa ruzuku ambayo mara nyingi hupendelea mashirika makubwa ya kimataifa, Mfuko huu unaipa kipaumbele mipango ya ngazi ya jamii, ikiwemo vikundi visivyo rasmi na mashirika ambayo huenda hayana usajili rasmi au uwezo wa kupata fedha kupitia njia za kawaida za ufadhili.

Tangu kuanzishwa kwa shughuli zake za utoaji wa ruzuku, GSF imeunga mkono mipango 56 katika nchi 29, na kufikia Novemba 2025 ilitenga Dola za Marekani milioni 3.35 kama ufadhili badilifu. Washirika hawa wanaopokea ruzuku hufanya kazi katika mipango mbalimbali, ikiwa ni pamoja na marekebisho ya sheria za uraia, utoaji wa msaada wa kisheria, utafiti na uhifadhi wa nyaraka kuhusu ukosefu wa uraia, uhamasishaji wa jamii, na utetezi wa haki sawa za uraia. Mfuko unalenga kudumisha uwiano wa kijiografia katika utoaji wake wa usaidizi, kama inavyoonyeshwa katika mchoro ulio hapa chini.

**Kielelezo 1 Uwakilishi wa kijiografia wa mipango ya GSF**




Mbali na kutoa msaada wa kifedha, Mfuko unatoa Programu ya Usaidizi inayotoa fursa za kuimarisha uwezo, nafasi ya kujifunza kutoka kwa wenzao, na majukwaa ya kujenga mitandao ili kuwasaidia washirika wanaopokea ruzuku kujenga uongozi, kuimarisha ushirikiano, na kuendeleza mikakati ya utetezi. Mfuko huo pia unatoa kipaumbele kwa mipango inayoongozwa na wanawake na vijana, ukitambua nafasi yao muhimu katika kuleta mabadiliko. Ukisimamiwa kupitia muundo shirikishi unaowahusisha viongozi walioathiriwa na ukosefu wa uraia pamoja na mashirika ya kiraia na washirika wa wafadhili, Mfuko huu unalenga kubadilisha mgawanyo wa mamlaka ndani ya mfumo wa ikolojia wa kushughulikia ukosefu wa uraia. Pia unafanya kazi ya kuondoa vikwazo vya kimuundo vinavyozuia upatikanaji wa ufadhili kwa kusaidia mashirika ambayo hayajasajiliwa rasmi, kwa sasa mipango 20 inayoungwa mkono ni ya makundi ambayo hayajasajiliwa, mengi yao yakifanya kazi katika mazingira yenye changamoto. Kwa pamoja, mbinu hizi zinalenga kuimarisha harakati shirikishi zaidi zinazoongozwa na jamii ili kushughulikia ukosefu wa uraia na sheria za uraia zenye ubaguzi.

## Uzoefu wa mashirika yaliyopokea ruzuku

Ili kuelewa vyema jinsi GSF inavyofanya kazi, mwandishi alifanya utafiti mfupi uliohusisha mashirika manne kutoka eneo la Asia-Pasifiki yaliyoteuliwa kuwa sehemu ya kundi la kwanza la washirika waliopokea ruzuku kutoka Mfuko huo. Ingawa mazingira yao ya utendaji yanatofautiana kwa kiwango kikubwa, mada kadhaa zinazofanana ziliibuka kutokana na uzoefu wao kuhusu mfumo wa utoaji ruzuku wa Mfuko.



**Picha ya pamoja ya moja ya mashirika yaliyopokea ruzuku – Mtandao wa Watu Walioathiriwa na Uraia. (CAPN). Picha ni kwa hisani ya: CAPN**

## Ufadhili badilifu na uthabiti wa mashirika

Mada kuu iliyosisitizwa na washiriki ilikuwa umuhimu wa ufadhili badilifu na wa muda wa miaka mingi. Mashirika yote manne yaliripoti kwamba msaada kutoka GSF uliwapatia kiwango cha uthabiti wa kifedha ambacho hupatikana kwa nadra kupitia mifumo ya kawaida ya ufadhili. Kwa vyovyote vile, ufadhili huo ulisaidia mahitaji ya msingi ya shirika kama vile mishahara ya wafanyakazi, gharama za uendeshaji na mifumo ya kiutawala.

Mashirika matatu kati ya manne yalisisitiza kwamba ubadilifu uliokuwepo katika ufadhili huo uliyaruhusu kugawa rasilimali kulingana na vipaumbele vinavyobadilika badala ya kufungwa na matokeo ya miradi yaliyokuwa yameamuliwa awali. Ubadilifu huu uliwezesha mashirika kuitikia kwa ufanisi zaidi kwa mazingira ya kisiasa yanayobadilika, fursa mpya za utetezi na mahitaji ya dharura ya jamii.

## Kuimarisha uwezo wa taasisi

Mbali na kusaidia shughuli za programu, ufadhili huu pia ulichangia kuimarisha uwezo wa mashirika - kwa kujenga juu ya ujuzi, utaalamu na mifumo iliyokuwepo tayari. Mashirika matatu yaliripoti kuwa GSF iliwawezesha kuboresha taratibu za usimamizi wa fedha, kuimarisha mifumo ya kiutawala na kuwekeza katika uendelevu wa mashirika yao. Katika baadhi ya matukio, mashirika yaliweza kuweka akiba ndogo za kifedha au kuanzisha mifuko ya maendeleo iliyolenga kusaidia shughuli za baadaye.

Mashirika mawili pia yalibainisha kuwa kuimarishwa kwa mifumo ya taasisi kuliimarisha uwezo wao wa kushirikiana na taasisi za serikali, mashirika ya kimataifa na wadau wengine wa asasi za kiraia. Kuongezeka kwa uwezo wa taasisi kulichangia kuongezeka kwa uaminifu wa mashirika hayo katika mijadala ya sera kuhusu haki za uraia na kutokuwa na uraia.

### Kupanua utetezi na ushirikishwaji wa jamii

Majibu ya utafiti pia yalionyesha kuwa ufadhili uliwezesha mashirika kupanua shughuli zao za utetezi na ushirikishwaji wa jamii. Mashirika yote manne yaliripoti kuwa msaada kutoka kwenye Mfuko uliyawezesha kutekeleza mipango iliyopanuliwa ya utetezi. Mipango hiyo ilijumuisha utafiti na uwekaji kumbukumbu kuhusu ukosefu wa uraia, kampeni za uhamasishaji wa umma, utetezi wa kisheria na ushirikishwaji wa watungaji sera. Mashirika matatu pia yaliripoti kuwa ufadhili huo uliyawezesha kuimarisha mitandao ndani ya jamii zilizoathirika na kutoa taarifa kuhusu haki za kisheria na michakato ya kuweka rekodi.

### Utoaji wa ruzuku shirikishi na yenye kuunga mkono

Mada nyingine iliyojitokeza kutokana na utafiti huu ilikuwa hali ya ushirikishwaji na uungaji mkono katika mchakato wa utoaji ruzuku wa Mfuko. Mashirika yote manne yalieleza kuwa mchakato wa kutuma maombi na kuchaguliwa ulikuwa rahisi kufikiwa na shirikishi, huku ukiwa na fursa za mazungumzo na kupokea maoni katika hatua zote za mchakato.

Vilevile, mashirika matatu yalibainisha kuwa mahitaji ya utoaji wa taarifa kwa Mfuko yalikuwa mepesi yakilinganishwa na yale ya wafadhili wengi wa kimataifa. Mahitaji hayo yaliyorahisishwa yalipunguza mzigo wa kiutawala na kuyaruhusu mashirika kuzingatia shughuli za utekelezaji wa programu.

Mashirika mawili pia yalisisitiza umuhimu wa fursa za ushirikiano zilizowezeshwa na Mfuko, ikiwemo mijadala wazi ya kijamii na majukwaa ya kujifunza kutoka kwa wenzao, yaliyowawezesha kuungana na mashirika mengine yanayofanya kazi kuhusu suala la ukosefu wa uraia.

### Changamoto za kimuundo zinazoendelea

Licha ya uzoefu mzuri ulioelezwa na washiriki wa utafiti, mashirika yote manne yalisisitiza kuwa zipo changamoto kubwa za kimuundo. Katika nchi kadhaa za eneo la Asia-Pasifiki, vikwazo vya kisheria na kiudhibiti vinazuia uwezo wa mashirika ya kiraia kupokea ufadhili wa kigeni au vinaweka taratibu ngumu za kupata idhini kwa shughuli zinazofadhiliwa kutoka nje.

Mashirika mawili pia yalieleza kuwa wanaharakati wanaotetea haki za uraia wakati mwingine hukumbana na migogoro ya kisiasa, ukosoaji kutoka kwa umma au hatari za kiusalama katika mazingira wanamofanyia kazi. Changamoto hizi zinaonyesha mazingira mapana ya kisiasa na kiudhibiti ambayo mashirika yanayoongozwa na watu wasio na uraia yanafanyia kazi.

## Kuhamisha madaraka: kutoka ushiriki wa juu juu hadi uongozi wa jamii

Lengo kuu la GSF si kuongeza tu rasilimali za kifedha kwa mashirika ya mashinani, bali pia kushughulikia tofauti za muda mrefu za mamlaka katika sekta ya kushughulikia tatizo la ukosefu wa uraia. Moja ya mifumo hiyo ni Kamati ya Kuchunguza Wanarika, ambayo hufanya kazi kwa kushirikiana na Kikundi Elekezi cha Mfuko ili kusaidia kuandaa vigezo na michakato ya kuchagua makundi yajayo ya wanufaika wa ruzuku.

Moja ya mashirika yaliyoshiriki katika utafiti liliripoti kuwa mwakilishi kutoka shirika lao alishiriki katika Kamati ya Uchunguzi wa Rika na pia alikuwa mwanachama wa Kikundi Elekezi cha Mfuko, jambo lililotoa fursa ya moja kwa moja ya kuchangia mijadala inayohusiana na utoaji wa ruzuku pamoja na mwelekeo wa Mfuko. Ingawa mashirika mengine yaliyoshiriki katika utafiti hayakuhusika moja kwa moja katika vyombo hivyo vya utawala, wahojiwa walisisitiza umuhimu wa mipango inayolenga kuimarisha uongozi wa watu wasio na uraia na jamii zilizoathiriwa ndani ya vuguvugu pana.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa GSF imechangia kwa namna chanya katika kuimarisha utetezi wa kijamii na uwezo wa kiutendaji wa mashirika washirika wake katika eneo la Asia na Pasifiki. Wakati huo huo, uzoefu wa mashirika haya unaonyesha kuwa, ingawa mifumo bunifu ya ufadhili inaweza kuwa na mchango muhimu katika kusaidia mipango inayoongozwa na jamii, haiwezi kuondoa kikamilifu vikwazo vya kisiasa na vya kimuundo vinavyowakabili watu wasio na uraia na mashirika yanayowawakilisha.

## Changamoto na Vizuizi

Ingawa uzoefu wa mashirika washirika yanayoungwa mkono na GSF unaonyesha matokeo kadhaa yaliyo chanya, bado kuna changamoto na vizuizi muhimu. Kiwango cha rasilimali zinazopatikana bado ni kidogo ikilinganishwa na ukubwa wa tatizo la ukosefu wa uraia duniani pamoja na idadi kubwa ya mashirika yanayofanya kazi ya kulishughulikia. Ingawa Mfuko umetoa msaada muhimu kwa baadhi ya mipango ya kijamii iliyochaguliwa, mashirika mengi ya kiraia yanayofanya kazi katika sekta ya ukosefu wa uraia bado yanaendelea kufanya kazi kwa rasilimali chache sana na hutegemea ufadhili wa muda mfupi au unaotolewa kwa misingi ya miradi. Hivyo basi, kupanua upatikanaji wa ufadhili badilifu kwa mashirika yanayoongozwa na watu wasio na uraia bado ni hitaji la msingi linaloendelea.

Wahojiwa pia walieleza mazingira ya jumla ya kimuundo na ya kisheria wanayofanyia kazi. Katika nchi kadhaa za eneo la Asia na Pasifiki, mashirika ya kiraia hukabiliwa na kanuni tata zinazosimamia ufadhili wa kigeni, usajili wa mashirika na shughuli za utetezi. Vizuizi hivi vinaweza kupunguza uwezo wa makundi ya kijamii kupanua shughuli zao hata pale ambapo usaidizi wa kifedha unapatikana Aidha, uanaharakati unaohusiana na haki za uraia unaweza kuwa suala nyeti kisiasa, hasa pale ambapo masuala ya uraia yanapokutana na masuala ya uhamiaji, haki za makundi ya wachache na utambulisho wa taifa. Kutokana na hali hiyo, mashirika na wanaharakati wanaweza kukabiliwa na ukosoaji kutoka kwa umma, upinzani wa kisiasa au hatari za kiusalama.

GSF yenyewe pia inaendelea kubadilika na kuimarika. Kwa kuwa ni mpango unaoendelea kujengeka, mifumo yake ya utoaji wa ruzuku kwa ushirikishaji na programu zake saidizi na ambatano zinahitaji kuakisiwa na kurekebishwa mara kwa mara. Mafunzo yanayotokana na uzoefu wa washirika wanaopokea ruzuku yatakuwa muhimu katika kuunda maendeleo ya baadaye ya mifumo shirikishi ya ufadhili ndani ya sekta ya kupambana na tatizo la ukosefu wa uraia.

## Hitimisho

Uzoefu wa mashirika washirika katika eneo la Asia na Pasifiki yaliyopata msaada kupitia GSF unaonyesha uwezo wa mbinu mpya za ufadhili katika kuimarisha utetezi unaoongozwa na jamii. Ufadhili nyumbufu na unaotolewa kwa kipindi cha miaka kadhaa umewezesha mashirika ya kijamii kuimarisha shughuli zao, kupanua mipango ya utetezi na kuitikia kwa ufanisi zaidi mahitaji ya jamii zisizo na uraia. Vipengele vya ushirikishwaji vilivyomo katika mfumo wa usimamizi wa Mfuko pia vimeunda fursa kwa watu walioathirika kushiriki kwa karibu zaidi katika michakato ya kufanya maamuzi.

Wakati huo huo, matokeo ya makala hii yanaonyesha kwamba ufadhili pekee hauwezi kuondoa vikwazo vya kimuundo na vya kisiasa vinavyokabili jamii zisizo na uraia pamoja na watetezi wao. Mazingira yenye kanuni na sheria zenye vikwazo, hisia za kisiasa zinazozunguka sera za uraia, pamoja na mifumo pana ya ubaguzi, vinaendelea kuathiri mazingira ambayo utetezi unafanyika. Hata hivyo, mipango kama GSF inaonyesha jinsi ufadhili badilifu na utawala unaoshirikisha wadau unavyoweza kuchangia kuimarisha harakati jumuishi zaidi zinazoongozwa na jamii katika kushughulikia tatizo la ukosefu wa uraia.

**Subin Mulmi** ni mwanasheria na mtafiti wa haki za binadamu anayeishi nchini Nepali. Kwa sasa anahudumia Uraia kwa Wote kama Mkurugenzi Mtendaji. Pia ni mwanachama wa Kikundi Kazi cha Asia Kusini cha Mtandao wa Haki za Wakimbizi wa Asia na Pasifiki.

# Uliobuniwa kutenga: jinsi mifuko ya ufadhili iliyounganishwa inavyofichua hali halisi ya ujanibishaji katika utekelezaji

**Amrita Paul**

Fedha zilizowekwa pamoja na mifumo nyumbufu ya utoaji wa ruzuku zinawasilishwa kama njia ya kukuza ufadhili wa misaada ya kibinadamu unaomilikiwa zaidi na wadau wa ndani. Dhana yake ni kukusanya rasilimali kutoka kwa wafadhili wengi, kupunguza gharama za miamala, na kuunda njia zinazowezesha mashirika madogo katika jamii kupata ufadhili ambao hayawezi kuupata kupitia ruzuku za moja kwa moja kutoka kwa mfadhili mmoja. Ingawa hatua hizi zinaendelea kutekelezwa, mafanikio ya mfumo huu na ni nani hasa anayenufaika nao bado ni maswali yanayohitaji kuchunguzwa.

Mashirika yanayoongozwa na wakimbizi (RLO, ikijumuisha pia mipango inayoongozwa na wakimbizi) na mashirika ya kijamii (CBOs) ni muhimu sana. Makala hii inachambua kinachotokea wakati mashirika na jamii hizi zinapojaribu kupata, kusimamia na kutoa taarifa kuhusu matumizi ya mfuko wa fedha zilizowekwa pamoja — hali halisi wanayokutana nayo, changamoto zinazojitokeza, na nyakati ambazo mfumo unawasaidia pamoja na pale unaposhindwa kuwahudumia.

Katika muktadha wa eneo la Asia-Pasifiki, idadi kubwa ya nchi hazina mfumo wa kitaifa unaofanya kazi kushughulikia hifadhi ya wakimbizi. Ulinzi wa kisheria ni dhaifu sana. Mashirika na mipango inayofanya kazi na jamii za wakimbizi mara nyingi huwa si rasmi na kwa kiasi kikubwa haipo ndani ya mfumo rasmi wa ufadhili. Hali ya sasa ya kupungua kwa ufadhili wa kimataifa wa misaada ya kibinadamu—ikiwa ni pamoja na kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kwa fedha kutoka kwa wafadhili wakuu, kupunguza shughuli kwa mashirika makubwa ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGOs) na mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN)—inafanya suala hili kuwa la dharura zaidi.

Mtandao wa Haki za Wakimbizi wa Asia-Pasifiki (APRRN) unaendelea kufanya kazi kama kiunganishi kati ya wafadhili wakubwa wa kimataifa na mashirika madogo sana yanayoongozwa na jamii, ambayo mara nyingi hayajasajiliwa, katika nchi kadhaa za eneo hilo. Yafuatayo yanatokana na uzoefu huo na yanachunguza maswali matatu:

- Mashirika yanayoongozwa na wakimbizi (RLO) yanawezaje kupata ufadhili?
- Baada ya kupokea ufadhili, yanasimamia vipi ufadhili huo?
- Na hatimaye, uzoefu wa kutoa taarifa na kuwajibika unaonesha nini kuhusu mifumo hii na namna ilivyobuniwa, yaani, inawalenga akina nani?

## Kupata ufadhili: si suala la kiutawala tu, bali pia la kisiasa

Mifumo mingi ya mifuko ya fedha iliyowekwa pamoja huhitaji waombaji wawe wamesajiliwa rasmi na mamlaka za kitaifa. Katika sehemu kubwa ya eneo la Asia-Pasifiki, hili ni sharti ambalo mashirika mengi ya wakimbizi yanayoongozwa na wakimbizi (RLO) na mashirika ya kijamii (CBO) hayawezi kulitimiza – si kwa sababu hayana mpangilio au hayawajibiki, bali kwa sababu usajili rasmi haupatikani kwao kisheria. Kwa mfano, nchini Bangladesh, wakimbizi wanakabiliwa na vikwazo vya kisheria vinavyowazuia kuajiriwa rasmi na pia kufungua akaunti za benki. Mazingira hayo hayo ya sera na sheria huwa kikwazo kwa RLO na CBO kujisajili kama mashirika rasmi.



**Maisha kambini hayasimami kusubiri mizunguko ya ufadhili. Cox's Bazar, Bangladesh. Picha ni kwa hisani ya: Mpango wa Vijana wa Khair Ullah/Rohingya**

Mashirika yanayoendeshwa na wakimbizi katika nchi isiyo na mfumo wa hifadhi kwa wakimbizi—na ambapo neno 'mkimbizi' halitambuliki kwa watunga sera na wafanya maamuzi wengi kwa sababu halina hadhi ya kisheria — hujengwa na kutegemea uthabiti wa jamii, uzoefu wa miaka mingi wa utekelezaji wa shughuli, na uwajibikaji wa kweli kwa watu wanaowahudumia. Hata hivyo, mashirika haya hayastahiki kupata ruzuku inayohitaji cheti cha usajili ambacho hayawezi kukipata.

Katika eneo la Asia-Pasifiki, RLO na CBO nyingi hupata mfuko wa fedha kupitia waenda kati pekee. Ni mashirika machache sana yanayoshirikiana moja kwa moja na wafadhili, na hata hayo hilo huwezekana baada ya kutambulishwa na wapatanishi. APRRN mara nyingi hufanya kazi kama mpatanishi wa aina hiyo, ikifanya kazi kama chombo kinachowajibikia ruzuku huku ikitoa ruzuku ndogo kwa vikundi vya kijamii ambavyo havijasajiliwa. Hili linawezekana pale tu ambapo makubaliano ya ruzuku kutoka kwa mfadhili yanaruhusu moja kwa moja utaratibu huo, jambo ambalo huhitaji majadiliano wakati wa kubuni mpango wa ruzuku.

Katika hatua ya kuandaa pendekezo la mradi, APRRN huwasilisha hoja wazi kwa mfadhili kuhusu mtindo huu wa utekelezaji - kwa kutumia mifano ya mafanikio ya awali na ushahidi uliorekodiwa wa utekelezaji unaoongozwa na jamii ili kuonyesha uzoefu wake na thamani ya kuelekeza fedha kupitia RLO na CBO. Hii hufungua nafasi ya kujadiliana kuhusu lugha ya makubaliano ya ruzuku ambayo huruhusu wazi utoaji wa ruzuku ndogo kwa vikundi ambavyo havijasajiliwa. Bila maandalizi haya kufanyika mapema, ubadilifu wa aina hii hutolewa mara chache sana kwa kawaida.

## Kusimamia fedha: usimamizi unaonekanaje katika utekelezaji

APRRN imechukua jukumu la kuwa mpatanishi kati ya wafadhili wakubwa wa kimataifa au mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGOs) na mashirika madogo sana ya ngazi ya kijamii ambayo mara nyingi hayajasajiliwa. Mara shirika linapopata ufadhili, changamoto hubadilika. Sasa msisitizo unaelekezwa katika kusimamia au kutumia fedha kwa uwajibikaji huku shughuli zilizoahidiwa katika ruzuku zikitekelezwa.

Utoaji wa ruzuku ndogo, yaani kuelekeza fedha kutoka mifumo mikubwa ya ruzuku kwenda kwa mashirika madogo, ni mchakato unaotumia muda mwingi na unaweza kukatisha tamaa. Hata hivyo, ni suluhisho linalowezekana na husaidia kuziba pengo lililopo katika mfumo wa sasa wa ufadhili. Wafadhili wakubwa mara nyingi hawawezi kuingia mikataba moja kwa moja na mashirika ambayo hayajasajiliwa au hayana historia rasmi ya usimamizi wa ruzuku. APRRN hufanya kazi hii na huendelea kujifunza jinsi ya kukabiliana na changamoto za mfumo huu unaoendelea kubadilika kwa kuwauliza washirika wake mara kwa mara jinsi ya kuboresha utendaji kwa kupunguza urasimu huku ikiendelea kudumisha uwajibikaji.

Kivitendo, APRRN hubeba sehemu kubwa ya kazi nzito za kiutawala kwa niaba ya washirika wake. Hii inajumuisha kuandika mapendekezo ya miradi, kushughulikia mchakato wa kuhamisha fedha kwa watu walioteuliwa, kuandaa taarifa kwa wafadhili, na kujadiliana kuhusu masharti ya makubaliano ya ruzuku. Hii hufanyika ili kuhakikisha kuwa RLO na CBO hazizuiwi kupata ufadhili kwa sababu ya ukosefu wa uwezo wa kiutawala ambao bado hazijapata nafasi ya kuujenga. Katika hatua ya utoaji wa ruzuku ndogo na utekelezaji, urasimu hupunguzwa zaidi kwa kubuni shughuli kwa ushirikiano wa karibu na RLO na

CBO kwa namna inayolingana na uwezo wao uliopo na kuimarisha uwezo wao wa kitaasisi, badala ya kulazimisha mifumo ya nje inayoongeza mzigo wa kufuata kanuni za kiutaratibu bila kuongeza thamani. Katika mtindo huu, uwajibikaji haujengwi kupitia masharti mazito ya utoaji wa taarifa, bali kupitia mawasiliano ya mara kwa mara yanayojengwa kwa uaminifu. Haya ni mawasiliano ya mara kwa mara kati ya wafanyakazi wa APRRN na wanachama wa RLO na CBO ili kujadili maendeleo pamoja na changamoto zinazojitokeza. Mazungumzo haya ya mara kwa mara hujenga mazingira ambapo changamoto hutambuliwa na kushughulikiwa mapema, na washirika huhisi wanasaidiwa badala ya kufuatiliwa.

## Kuaminiana

Msingi wa yote ni uaminifu—na uaminifu huo lazima uwe wa pande zote mbili. Mashirika madogo yanahitaji kuamini kwamba APRRN si ngazi nyingine ya urasimu kati yao na rasilimali wanazohitaji; kwamba tutawatetea na kutetea maslahi yao badala ya kuwasimamia; na kwamba hatutatoweka mara tu mzunguko wa ruzuku utakapomalizika. Mashirika yanayoaamini mashirika patanishi, huwa tayari kueleza matatizo mapema na kuomba msaada wanapouhitaji. Pia yatashiriki mafanikio yao pamoja na changamoto zao.

Kivitendo, uaminifu huu huonekana katika uwazi ambao RLO na CBO huonyesha wakati wa mikutano ya mara kwa mara na APRRN. Kupitia mazungumzo hayo, washirika wameeleza changamoto mbalimbali, kuanzia mabadiliko ya sera katika kambi za wakimbizi yanayoathiri utekelezaji wa programu, vikwazo vya kisheria vinavyozuia kazi zao, hadi mapungufu ya kiuwezo ya ndani yaliyosababishwa na hali ambazo hawawezi kudhibiti, kama vile kumpoteza ghafla mwanachama muhimu wa timu. Pale ambapo APRRN inaweza kufanya kazi pamoja na washirika wake—iwe ni kwa kutetea maslahi yao mbele ya mamlaka, kurekebisha mipango ya kazi, au kutoa msaada wa moja kwa moja wa kiusimamizi kwa shirika—hufanya hivyo. Pale ambapo changamoto ni za kimfumo na haziwezi kutatuliwa mara moja, kuzitaja wazi kunatimiza lengo muhimu: husaidia juhudi pana za utetezi za APRRN na kuhakikisha kuwa taarifa kwa wafadhili zinaonyesha hali halisi ilivyo badala ya kuwasilisha picha ya mafanikio pekee. Uwazi huu wa pande mbili kuhusu mafanikio na changamoto ni ishara kwamba uhusiano huo unafanya kazi kama ulivyokusudiwa.

Kujenga kiwango hiki cha uaminifu kunahitaji muda na hupitia mizunguko kadhaa ya ruzuku. Kunahitaji ushirikiano endelevu, uaminifu kuhusu vikwazo na changamoto zilizopo, pamoja na utayari wa kukubali mashaka badala ya kutegemea mifumo migumu inayotenga mashirika ambayo wafadhili wanafaa kusaidia.

## Uwajibikaji unaolingana na muktadha

Moja ya changamoto zinazojitokeza mara kwa mara ni jinsi ya kupatanisha mahitaji ya uwajibikaji ya wafadhili—ambayo mara nyingi huwa yameundwa kwa ajili ya mashirika makubwa na yaliyoimarika kitaasisi—na hali halisi ya mashirika madogo ya kijamii. Kiolezo cha ripoti kinachochukua timu ya mawasiliano siku tatu kukamilisha si tu tatizo dogo kwa shirika linaloendeshwa na timu ndogo ya viongozi wa wakimbizi na watu wa kujitolea. Ni kikwazo.

APRRN imejitahidi kukuza kile kinachoweza kuitwa kanuni zinazozingatia muktadha wa migogoro: mbinu ya uwajibikaji inayozingatia kwa dhati hali halisi ambazo mashirika washirika hufanyia kazi. Hii inahusisha kutoa ripoti rahisi inayolenga kile kilichotokea kwa kweli na mafunzo yaliyopatikana; nyakati badilifu za kuwasilisha ripoti; na mazungumzo ya mara kwa mara ya kujadili changamoto badala ya kusubiri hadi muda rasmi wa kuwasilisha ripoti ndipo changamoto zielezwe. Hii haimaanishi kutozingatia uwajibikaji, bali kubuni mifumo ya uwajibikaji inayochochea uhusiano kati ya washirika badala ya kuchukua nafasi yake.

Kwa mfano, APRRN iliandaa muundo wake wa kutoa ripoti kwa miradi iliyopokea ruzuku ndogo —muundo ambao kimakusudi unaondoka katika lugha ya uzingatiaji wa masharti inayotumika katika ripoti kwa wafadhili, ambayo mara nyingi mashirika madogo huiona kuwa ngumu na ya kuwatenga. Muundo huo huunganisha taarifa za masimulizi na taarifa za kifedha, lakini umejengwa kuzunguka kile kilichotokea kwa kweli, mafunzo yaliyopatikana, na changamoto zilizojitokeza—badala ya kuzingatia tu ikiwa shughuli zilitekelezwa kwa wakati na kulingana na bajeti. Muhimu zaidi, muundo huo unatenga nafasi wazi na kuwapa washirika umiliki wa kuripoti masuala nyeti ambayo huenda wasijisikie huru kuyaeleza katika ripoti rasmi kwa wafadhili. Masuala hayo ni pamoja na changamoto za kiutendaji, masuala ya ulinzi, au mabadiliko ya kimuktadha yanayoathiri utekelezaji wa mradi. Pia unawahimiza washirika kurekodi suluhisho walizobuni, ukitambua kwamba kutatua matatizo katika mazingira yenye rasilimali chache ni aina ya ujifunzaji ambao unastahili kuhifadhiwa.

Matokeo yake ni mchakato wa utoaji ripoti unaofanya kazi zaidi kama mazungumzo yaliyopangwa kuliko ukaguzi rasmi. Mchakato huu huiwezesha APRRN kubaini maeneo yanayohitaji usaidizi wa haraka huku ukiyapa Mashirika Yanayoongozwa na Wakimbizi (RLO) na Mashirika ya Kijamii (CBO) sauti halisi kuhusu jinsi kazi yao inavyoeleweka na kuwasilishwa.

Mfano mwingine wa hali kama hii unatokana na tajriba ya APRRN ilipotoa ruzuku ndogo kwa shirika la vijana nchini Bangladesh lililokuwa likitekeleza mradi wa kuongeza upatikanaji wa elimu kwa wanawake na wasichana. Mwanzoni mwa mradi, shirika hilo lilieleza katika mazungumzo ya ufuatiliaji kwamba baadhi ya wazazi walikuwa na wasiwasi kuhusu kuwaandikisha binti zao katika vipindi vya kujifunza kusoma na kuandika. Hawakuwa na uhakika wa manufaa ya vipindi hivyo au walikuwa na hofu kuhusu usalama wao. Badala ya kuruhusu hali hiyo iathiri takwimu za mahudhurio na kuonekana tu katika ripoti ya mwisho, timu ilikabiliana nayo kwa pamoja. APRRN na timu ya shirika walikubaliana kwamba mazungumzo ya kijamii—kukutanisha familia ambazo tayari zilikuwa zikishiriki katika mradi pamoja na zile zilizokuwa na mashaka—kungeweza kubadili mitazamo kwa urahisi zaidi kuliko kuwafikia watu mmoja mmoja. Pia walipendekeza kumteua mtu wa kuwasindikiza wasichana wanapokwenda na kurudi darasani, hatua ambayo ilishughulikia moja kwa moja wasiwasi wa wazazi kuhusu usalama. Hatua zote mbili zilitekelezwa. Matokeo yalikuwa ya kuvutia: mahudhurio yaliongezeka, na wazazi ambao mwanzoni walikuwa na mashaka waligeuka kuwa baadhi ya watetezi wakubwa wa programu hiyo. Kama alivyosema mzazi mmoja baada ya binti yake kukamilisha vipindi hivyo: “Sikudhani jambo hili lingekuwa na manufaa kwetu, lakini sasa ninaona kile ambacho limempa.”

Aina hii ya mazungumzo—ya wazi, ya wakati muafaka na yaliyojengwa kwenye uaminifu—ndiyo ambayo miundo ya kawaida ya utoaji ripoti haijaundwa kutilia mkazo, na ndiyo ambayo mbinu ya APRRN imekusudiwa kuilinda.

## Kinachowezesha utoaji ripoti kwa uaminifu

Ripoti za kiuaminifu na zenye manufaa kutoka kwa mashirika yanayoongozwa na wakimbizi (RLO) na mashirika ya kijamii (CBO) kwa kawaida hutokana na uaminifu wa kweli katika uhusiano na matumizi ya mifumo rahisi ya kuripoti, pamoja na kuwa na uhakika kwamba taarifa hizo zitatumika; yaani, kuna mtu atakayezisoma, atazijibu, na atazitumia kuongoza maamuzi ya baadaye. Mifumo ya uwajibikaji inapaswa kubuniwa kwa kuzingatia shirika na uhusiano uliopo, badala ya kuweka rekodi ya ukaguzi kama lengo kuu.

## Umuhimu wa kuwa na vyanzo mbalimbali vya ufadhili

Somo jingine ni umuhimu wa kuwa na vyanzo mbalimbali vya ufadhili, kwa APRRN kama mpatanishi, na pia kwa mashirika tunayoshirikiana nayo na kuyaunga mkono. Kutegemea mfadhili mmoja au aina moja ya ufadhili ni udhaifu wa kimuundo. Chanzo hicho kinapoondoka—kama ilivyotokea katika mwaka uliopita katika sekta nzima—mashirika ambayo hayana vyanzo mbadala huporomoka, jambo ambalo tayari limekumba mashirika mengi. Kujenga msingi imara zaidi wa ufadhili, ikiwa ni pamoja na kupitia mifuko ya pamoja, wafadhili wadogo wa ndani na mifumo badilifu, ni usimamizi mzuri wa fedha na pia njia ya kuokoa mashirika.

## Hitimisho

Uzoefu wa kupata, kusimamia na kuripoti kuhusu mifuko ya pamoja unaonyesha mambo kadhaa kwa uwazi: vikwazo vinavyokabili mashirika yanayoongozwa na wakimbizi (RLO) na mashirika ya kijamii (CBO) si matukio ya kawaida ndani ya mfumo unaofanya kazi vizuri. Haya ni maamuzi ya kisiasa na ni ya kimuundo—yamejengwa ndani ya mifumo ambayo haikubuniwa kwa kuzingatia mashirika haya, na ambayo huendeleza ubaguzi wao isipokuwa pale hatua za makusudi zinapochukuliwa kuubadilisha.

Masharti yanayowezesha mafanikio pia yanaeleweka vizuri. Haya ni pamoja na wapatanishi wanaoaminika, mifumo iliyorahisishwa, uwajibikaji unaojengwa katika mahusiano, na msaada wa kweli wa kujenga uwezo. Hakuna maarifa mapya kati ya haya. Pengo lililopo halihusu kujua kinachofanya kazi na kutokujua. Inahusu kujua na kutekeleza kwa uthabiti, katika kiwango cha usanifu wa mifumo, sera za wafadhili na utendaji wa taasisi.

Kubadilisha mamlaka katika sekta ya misaada ya kibinadamu hakufanyiki mara moja. Lugha hubadilika kwa kasi zaidi kuliko vitendo. Lakini uzoefu ulioelezwa hapa unaonyesha wazi kile kinachohitaji kubadilika—na kwamba mashirika yaliyopitia uzoefu huu yako tayari kwa mazungumzo tofauti.

**Amrita Paul** ni Afisa wa Programu katika Mtandao wa Haki za Wakimbizi wa Asia na Pasifiki. Anajikita katika mifumo ya upatikanaji wa haki, ulinzi wa wakimbizi na wanaotafuta hifadhi katika nchi ambazo hazijaridhia mikataba husika, na kuhakikisha upatikanaji wa msaada bora wa kisheria kwa raia wa kigeni katika eneo lote.

Makala hii imejengwa juu ya uzoefu wa pamoja wa kazi ya APRRN ya kutoa ruzuku ndogo, pamoja na ukarimu wa mashirika yanayoongozwa na wakimbizi na mashirika ya kijamii yaliyoshiriki mafunzo na uzoefu wao katika mchakato huo. Mwandishi pia anapenda kuwashukuru Hafsar Tameesuddin na Klaus Dik Nielsen kwa mchango wao, usaidizi wao na maoni yao katika kipindi chote cha mchakato.

Humanitarian Practice Network

ODI Global

Toleo hili la **Humanitarian Exchange** lilihaririwa na Sara Hussain

**Humanitarian Practice Network (HPN)**
ODI
Four Millbank
London SW1P 3JA
United Kingdom

Simu: +44 (0)20 7922 0300
Barua pepe ya HPN: hpn@odi.org
Tovuti ya HPN: www.odihpn.org